BREAKING NEWS
CHEZA SUPA JACKPOT
TZS 1,000,000,000
KWA 1000/- TU!
SportPesa.CO.TZ PIGA *150*87#



UKURASA 3

**MSAJILI** atangaza hatua mpya sakata la NCCR-Mageuzi



Nipashe 11
HOTUBA
JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
HOTUBA YA WAZIRI WA ARDHI,
NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI

HOTUBA YA WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI, MHESHIMIWA DKT. ANGELINE S.L. MABULA (MB.), AKIWASILISHA BUNGENI MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA KWA MWAKA WA FEDHA 2022/23

MHE. DKT. ANGELINE S.L. MABULA (MB.)
WAZIRI

MHE. RIDHIWANI JAKAYA KIKWETE (MB.)
NAIBU WAZIRI

DKT. ALLAN H. KIJAZI
KATIBU MKUU

BW. NICHOLAS M. MKAPA
NAIBU KATIBU MKUU

Dodoma
26 Mei, 2022

UKURASA 11

**Nipashe**
Ijumaa Mei 27, 2022 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-
ISSN 0856 • Na. 0580958
MWANGA WA JAMII
www.ippmedia.com
www.twitter.com/nipashetz
www.facebook.com/nipashetz
www.instagram.com/theguardian_newspaper
LIKE & FOLLOW US

## KIKOKOTOO KIPYA

# Hivi ndivyo mafao yatakavyokuwa

**KUNA** tabasamu, kununa kwa wastaafu...*Endelea Ukurasa 2*




Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Dk. Angelina Mabula, akiwasilisha hotuba ya makadirio ya mapato na matumizi ya wizara yake kwa mwaka wa fedha wa 2022/2023, Bungeni, jijini Dodoma jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

## Majaliwa apokea maoni wananchi wa Ngorongoro

UKURASA 3

**MICHEZO** YANGA SC YAFUNGUKA KWA SAIDO, AMBUNDO UK.24
**MAONI, KATUNI** UK.6



Katibu Mkuu Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Ajira, Vijana na wenye Ulemavu, Prof. Jamal Katundu, akizungumza na waandishi wa habari, jijini Dodoma jana, wakati akitoa taarifa kuhusu kanuni mpya za kikokotoo cha mafao ya watumishi nchini. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Hivi ndivyo mafao yatakavyokuwa

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

HATIMAYE serikali imetangaza kikokotoo kipya cha mafao ya wastaafu, safari hii kukishuhudiwa kuwapo kwa usawa na uwiano kati ya watumishi wa umma na sekta binafsi.

Kutangazwa kwa kanuni hizo ni hitimisho la sintofahamu ya mafao hayo iliyodumu kwa takribani miaka nne tangu mwaka 2018 serikali ilipositisha utekelezaji wa kanuni mpya za mafao kwa wastaafu zilizotaka kiwango cha mkupuo kiwe asilimia 25.

Kutokana na kuwapo kwa malalamiko ya wadau dhidi ya kanuni hizo Rais wa wakati huo, Dk. John Magufuli alilazimika kuzisitisha mwaka huo ili kutoa muda kujadili na Mei 14 mwaka huu, Rais Samia Suluhu Hassan aliliridhia ombi la wadau wa hifadhi ya jamii kupandisha kiwango cha kikokotoo kutoka asilimia 25 hadi 33.

Akizungumza na waandishi wa habari jijini hapa jana, mwenyekiti wa kamati elekezi ya kanuni hizo ambaye ni Katibu Mkuu wa Ofisi ya Rais, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu, Prof. Jamal Katundu, alisema waziri wenye dhamana na masuala ya hifadhi ya jamii aliunda kamati hiyo ili kutekeleza maelekezo ya serikali ya kukubaliana kanuni itakayowianisha mafao kwa wafanyakazi wote.

Alisema kamati hiyo ilifanya kazi yake kwa kuzingatia mambo makubwa mawili ambayo ni kuhakikisha kanuni mpya inayopendekezwa inatoa mafao bora kwa wastaafu na pia mifuko inakuwa endelevu kwa manufaa ya wananchi wote.

"Kazi ya kamati ya kuandaa kanuni itakayotumika baada ya kipindi cha mpito imekamilika na kuridhiwa na wadau, kanuni mpya iliyoridhiwa itaanza kutumika rasmi Julai Mosi mwaka 2022," alisema.

**MAFAO YATAKAVYOKUWA**

Prof. Katundu alisema kiwango cha mkupuo cha asilimia 33 ni kwa mifuko yote na kikokotoo limbikizi kitakuwa 1/580 kama ilivyokuwa kwa mfuko wa NSSF na ilivyokuwa mifuko ya PPF, GEPF na baadhi ya wanachama wa iliyokuwa PSPF na LAPF.

"Makadirio ya miaka ya kuishi baada ya kustaafu ni 12.5 kama ilivyo kwa mfuko wa NSSF na iliyokuwa mifuko ya PPF, GEPF na baadhi ya wanachama wa iliyokuwa PSPF na LAPF," alisema.

Alisema mshahara wa kukokotolea mafao ya pensheni utakuwa wastani wa mishahara bora ya miaka mitatu ndani ya miaka 10 kabla kustaafu na umri wa kustaafu kwa lazima utaendelea kuwa miaka 60.

"Pia niwafahamishe kuwa pensheni za wastaafu watakaotumia kanuni hizi zitakuwa zikihuishwa mara kwa mara kwa kuzingatia mfumuko wa bei na uwezo wa mifuko hiyo ya pensheni," alisema.

**FAIDA ZA KANUNI MPYA**

Katibu Mkuu huyo alisema kanuni hizo zitaongeza kiwango cha malipo ya mkupuo kutoka asilimia 25 iliyokataliwa mwaka 2018 hadi asilimia 33 kwa wanachama 1,364,050 sawa na asilimia 81 ya wanachama wote 1,690,187 wa mifuko ya pensheni.

Pia alisema inaongeza pensheni ya mwezi kutoka asilimia 50 ya sasa hadi asilimia 67 kwa waliokuwa wanachama wa PSPF na LAPF ambao ni asilimia 19 ya wanachama wote wa mifuko ya pensheni.

"Faida nyingine ni mifuko ya pensheni ya PSSSF na NSSF itaimarika na kuwa endelevu, pia kwa kuwa kanuni mpya inaimarisha mifuko na kuwa endelevu, mifuko itaweza kuongeza pensheni ya kila mwezi kwa kuzingatia tathmini zitakazofanyika kila baada ya miaka mitatu," alisema.

Vilevile, alisema wanachama wote wanaochangia kwenye mifuko ya pensheni watatumia kanuni moja ya mafao na hivyo kuweka uwiano na usawa wa mafao baina ya wastaafu.

Katibu huyo alisema serikali imeweka utaratibu wa kutoa elimu kwa wanachama na umma kuhusu kanuni hizo ili kuhakikisha wote wanakuwa na uelewa sahihi na faida zake.

"Nitoe rai kwa wananchi kuendelea kuiamini serikali sikivu inayoongoza na nishukuru wadau wa utatu kwa kazi nzuri ya pamoja iliyofanyika kwa weledi na uzalendo," alisema.

**KAULI ZA WADAU**

Rais wa Shirikisho la Vyama vya Wafanyakazi (TUCTA), Tumaini Nyamhokya, alisema upangaji wa kanuni hizo umekuwa shirikishi na zimeridhiwa na wadau na hakuna eneo walilofichwa.

Alisema pamoja na hayo walikubaliana wasiende chini ya asilimia 35 lakini serikali na wataalamu kutoka nje walishauri kufikia asilimia 33 ili wafanyakazi wasiongeze michango ya kuchangia na mifuko iendelee kuwa endelevu.

"Tulikuwa tunapata asilimia 50 ya mkupuo halafu asilimia 50 nyingine tulikuwa tunapata malipo ya kila mwezi, lakini sasa imebadilishwa asilimia 33 ya mkupuo halafu asilimia 67 tutaipata kwa mwezi, hakuna namna inabidi tulipokee, wafanyakazi zoezi hili limekuwa shirikishi, sekta binafsi tumechukua TUICO wameshiriki ndani," alisema.

Alisema watumishi wanaochangia mifuko ya NSSF, PPF, GEPF, mkupuo wao umepanda kutoka asilimia 25 na kufikia asilimia 33.

"Kwa wao ni furaha kubwa sana sisi tulikuwa tunapata asilimia 50 tumeshuka na sasa itakuwa asilimia 33, niwasihi tulipokee hili wafanyakazi kwetu sisi ni gumu kumeza lakini ni kwa mustakabali wa uendelevu kwa vizazi vinavyokuja, tusimame pamoja kwenye hili," alisema.

Mkurugenzi Mtendaji wa Chama cha Waajiri Nchini (ATE), Suzanne Ndomba, alisema waajiri, wafanyakazi na serikali walikaa wote kwa pamoja kutengeneza kanuni hizo ambazo zimezingatia utaalamu na wataalamu walikuwa wa pande wote.

"Niwasihi wafanyakazi na waajiri, serikali itaendelea kutoa elimu na kwa wale waajiri wenye maswali waje ATE tutasaidia kuchukua na kupeleka serikalini ili kupata ufumbuzi,"alisema.

Kaimu Rais wa Chama cha Walimu (CWT), Dinnah Mathamani, alisema jambo hilo limefanyiwa kazi kwa muda mrefu na wameshirikishana.

"Kwa upande wetu ambao kikokotoo kilikuwa asilimia 50 na kushushwa kuwa asilimia 33 nadhani tutapata mshtuko lakini hali ndivyo ilivyo kwa kuwa tumeelezwa kwanini tumefikia hapa, faida zake bila kujali waliokuwa asilimia 50, au asilimia 25 lakini kubwa ni mifuko kuwa endelevu," alisema.

Aliwaomba walimu wawe na utulivu, watapewa elimu na kuelewshwa, akisema: "Tukipata elimu kwa ujumla hakutakuwa na shida, sisi tumeshirikishwa kwenye kamati elekezi na tumepitishwa na wataalamu, sisi walimu tumelipokea na tutaendelea kutoa elimu kwa ambao hawajaelewa."

# Yajayo Ardhi yanafurahisha

**Na Romana Mallya,** DODOMA

YAJAYO Ardhi yanafurahisha! Ndivyo unavyoweza kusema kutokana na mikakati mbalimbali iliyowekwa na Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa mwaka ujao wa fedha.

Wizara hiyo imeliomba Bunge kuiidhinishia Sh. bilioni 110.3 ili kutekeleza mambo mbalimbali katika mwaka huo wa fedha, ikiwa ni pamoja na kukamilisha miradi ya ujenzi inayofanyika chini ya Shirika la Nyumba la Taifa (NHC).

Akiwasilisha bungeni jana hotuba ya makadirio ya mapato na matumizi ya wizara hiyo mwaka ujao wa fedha, Waziri wake, Dk. Angelina Mabula, alisema mipango yao mingine ni kuhuisha na kutunza kumbukumbu za wamiliki ardhi katika mfumo wa kielektroniki ili kurahisisha shughuli mbalimbali.

Waziri Mabula alisema wizara imepanga kujenga ofisi za ardhi mikoa 25 zitakazokidhi utoaji huduma kwa Mfumo Unganishi wa Kuhifadhi Taarifa za Ardhi (ILMIS).

"Wizara itaandaa na kutoa vyeti vya ardhi ya vijiji 100, hati za hakimiliki za kimila 250,000, hatimiliki 500,000 na sehemu ya jengo 1,000," alisema.

Waziri huyo pia alisema watasajili miamala ya hatimiliki na nyaraka za kisheria 100,000.

"Ninatoa rai kwa wabunge ambao ni wajumbe wa baraza la madiwani kuhakikisha halmashauri zinatenga fedha za bajeti zao kwa ajili ya kutekeleza shughuli za sekta ya ardhi," alisema.

Waziri Mabula alibainisha kuwa hadi Mei mwaka huu, jumla ya mashamba 106 yametambuliwa na kukaguliwa na katika mwaka wa fedha 2022/23 wizara itaendelea kuyakagua 230 ili kubaini uzingatiwaji wa masharti ya uendeshaji wake.

**MIGOGORO ARDHI**

Waziri Mabula alimshukuru Rais Samia Suluhu Hassan kwa kuridhia utekelezaji wa utatuzi wa migogoro ya ardhi kwa vijiji 975 ambapo 920 vitarasimishwa kwa njia shirikishi na kuendelea kufanyiwa tathmini vijiji 55 ili kuishauri serikali hatua ya kuchukua.

Alisema hadi Mei 15 mwaka huu, wizara imeidhinisha taarifa za uthamini 46,910 ambapo wa kawaida ni 18,881 na wa fidia ni 28,029.

"Malalamiko yaliyopokelewa ni 51 ya uthamini wa fidia na kushughulikia, udhamini wa maeneo 15 ya miradi umefanyiwa uhakiki ili kutatua migogoro ya fidia," alisema.

Waziri huyo alisema wizara imekuwa ikipokea malalamiko mengi ya kutoka kwa wananchi yanayohusiana na kuchelewesha, kulipwa fidia pungufu au kutolipwa.

"Ninazisihi taasisi za serikali na kampuni binafsi kulipa fidia kwa wakati ili kuepuka ulipaji wa riba na malalamiko yanayotokana na ucheleweshaji. Kamwe serikali haitaruhusu utwaaji wa ardhi bila kulipa fidia," alionya.

Alisema katika mwaka wa fedha 2022/23 wizara itaratibu na kusimamia uandaaji wa taarifa za uthamini 54,000. Kati yake, wa kawaida ni 20,000 na fidia 34,000 na kushughulikia malalamiko.

**KODI YA PANGO**

Waziri huyo alisema muda mrefu kumekuwa na malalamiko kutoka kwa wananchi yanayotokana na takwa la kisheria la kutoza riba baada ya miezi sita ndani ya mwaka wa fedha ambao kodi ya pango la ardhi inapaswa kulipwa.

"Ili kuondoa malalamiko hayo, wizara inakusudia kufanya marekebisho ya Sheria ya Ardhi kupitia Muswada wa Sheria ya Fedha ili riba ya kuchelewa kulipa kodi ya pango la ardhi ianze kutozwa baada ya kuisha kwa mwaka wa fedha," alifafanua.

Alisema kuwa hadi Mei 15, mwaka huu, kati ya fedha zilizoidhinishwa, wizara imepokea Sh. bilioni 5.6, hivyo kufanya kuwa na jumla ya Sh. bilioni 55.6 kwa ajili ya utekelezaji wa programu ya kupanga, kupima na kumilikisha ardhi ambazo zimekopeshwa halmashauri 92, vyuo vya ardhi vitatu (3) na Ofisi ya Ardhi ya Mkoa wa Iringa ili kuwezesha upangaji, upimaji na umilikishaji wa viwanja takriban 373,155 na inatarajia kupata Sh. bilioni 51.6 baada ya urejeshwaji mkopo kwa mwaka wa kwanza.

Waziri Mabula pia alisema wataendelea kutekeleza miradi ya kimkakati ambayo ni ujenzi wa Bwawa la Kuzalisha Umeme la Julius Nyerere, Ujenzi wa Bomba la Mafuta kutoka Hoima, Uganda hadi Chongoleani - Tanga, Tanzania na ujenzi wa Reli ya Kisasa (SGR).

Waziri huyo alisema NHC imepanga kukusanya Sh. bilioni 268.03 kutoka kwenye vyanzo mbalimbali vya mapato; kuendelea kukamilisha mradi wa ujenzi wa nyumba 300 kati ya nyumba 1,000 za gharama nafuu jijini Dodoma kwa ajili ya kuuza na kupangisha na kukamilisha ujenzi wa mradi wa Morocco Square.

*SOMA HOTUBA UK. 11-16

# Majaliwa apokea maoni wakazi Ngorongoro

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI Mkuu Kassim Majaliwa amepokea mapendekezo kutoka kwa wananchi wa Tarafa za Loliondo, Ngorongoro na Sale kuhusu namna bora ya kulinda uhifadhi wa maeneo hayo.

Maoni hayo yaliwasilishwa juzi na wawakilishi wa wakazi wa wilaya hiyo akiwamo Mbunge wa Ngorongoro, Emmanuel Shangai, malaigwanani, madiwani, wenyeviti wa vijiji, wawakilishi wa wanawake na vijana, ofisini kwake Mlimwa, Dodoma.

Taarifa iliyotolewa jana na Ofisi ya Waziri Mkuu ilisema kwamba baada ya kupokea mapendezo hayo, Waziri Mkuu aliwasisitiza wananchi hao waendelee kuiamini serikali kwa kuwa haiwezi kuwa na mipango mibovu kwa wananchi wake.

"Msisikilize maneno maneno ya watu wa pembeni," alisema Waziri Mkuu.

Akizungumzia kuhusu eneo la Msomera lililoko wilayani Handeni, Tanga ambako yanaandaliwa makazi kwa ajili ya kuwahamishia wakazi wa Ngorongoro waliokubali kuhama kwa hiari, Waziri Mkuu Mjaliwa alisema ujenzi unaendelea vizuri.

Kadhalika, Majaliwa alisema ujenzi wa nyumba za makazi 103 upo mbioni kukamilika na pia, serikali imepanga kuongeza nyumba nyingine lengo likiwa ni kufikia nyumba 500 kwa ajili ya wakazi hao.

Majaliwa alisema serikali inaendelea kuimarisha sekta ya mifugo ili kuhakikisha wafugaji wote nchini wanapata tija kupitia shughuli hiyo.

Machi 22, mwaka huu Waziri Mkuu Majaliwa alipokea orodha ya majina ya awali ya kaya 86 zenye watu 453 ambao wamekubali kuondoka kwenye Hifadhi ya Ngorongoro kwa hiari huku wengine walikuwa wakiendelea kujiandikisha.

Serikali imetenga eneo la kilometa za mraba 400,000 wilayani Handeni ambalo kati ya hizo kilometa za mraba 220,000 zilitumika kwa kujenga nyumba , kupima viwanja na kutenga maeneo ya malisho.

# Ofisi ya Msajili yabariki uamuzi NCCR-Mageuzi

**Na Mwandishi Wetu**

OFISI ya Msajili wa Vyama vya Siasa imesema baada ya kutangaza kumsimamisha Mwenyekiti wa NCCR-Mageuzi, James Mbatia, hatua inayofuata ni kuliondoa jina la kiongozi huyo kwenye orodha ya viongozi wa chama.

Imesema nafasi iliyokuwa inashikwa na Mbatia itaongozwa na Makamu Mwenyekiti NCCR-Mageuzi Zanzibar kuanzia sasa.

Msajili Msaidizi wa Vyama vya Siasa nchini, Sisty Nyahoza, aliyasema hayo jana wakati akizungumza na kituo cha habari cha East Africa Radio.

Nyahoza alisema: "Sisi baada ya kuwaandikia barua NCCR-Mageuzi kinachofuata sasa ni kusajili mabadiliko ya uongozi, ndiyo sheria inavyosema, kwa hiyo sasa hivi tunaweka pembeni jina la Mbatia na nafasi yake anakaimu yule Makamu Mwenyekiti Zanzibar."

Alisema Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa ina orodha ya viongozi wa NCCR-Mageuzi ambayo ndiyo itafuatwa kisheria.

Nyahoza alisema mkutano wa Halmashauri Kuu ya NCCR-Mageuzi uliofanyika ulikuwa sahihi na Mbatia aliondolewa kihalali, hivyo, alimshauri Mbatia kukaa pembeni kuliko kuendelea kuongea na vyombo vya habari kila siku.

"Sisi tumesema ule mkutano ulikuwa sahihi na Mbatia ameondolewa kihalali, ndiyo jambo la msingi akae pembeni, mtu ukiona kabisa wenzako hawakutaki ndani ya chama shida yako nini, anaongea na vyombo vya habari badala ya kuja Ofisi ya Msajili, tunamkaribisha sana hata leo aje."

Nyahoza alisema sio kazi ya Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa kugharamia mikutano ya vyama, ofisi ilialikwa kuangalia kile kinachokwenda kufanyika.

"Mbona tulialikwa vya CHADEMA hawasemi tulifadhili, NCCR-Mageuzi wana matatizo yao ndani ya chama wasituletee sisi, kama wana shida zao sisi kazi yetu ni kuangalia nani yupo kwa mujibu wa sheria," alisisitiza Nyahoza.

Alivishauri vyama vya siasa kuheshimu sheria na katiba zao.

Alisema vyama vingi vya siasa vina migogoro mingi kwa sababu wanabishana kugombea madaraka, wanakuwa na tamaa ya mali.

"Kama NCCR-Mageuzi walikuwa na masuala ya migogoro ya mali za chama, mambo yameanza siku nyingi na sio sisi tuliyapeleka huko ni wao wenyewe walianzana huko."

Mmoja wa wajumbe wa NCCR-Mageuzi, Joseph Selasini jana akizungumza na waandishi wa habari alisema wakati wanaitisha mkutano wa Halmashauri Kuu na kubaini Mbatia na Makamu Mwenyekiti wake hawapo walichukua hatua mbalimbali.

Alisema wajumbe wa Halmashauri Kuu walianza kujitambulisha, kujiorodhesha majina, kuweka sahihi zao sambamba na kupigwa picha na kurekodiwa.

"Hivyo maneno kwamba Selasini amempindua Mbatia ni uchochezi, hayana maana. Ule mkutano kwa kuwa Makamu Mwenyekiti Zanzibar alikuwapo kikao kiliamua uendelee na kufikiwa maamuzi.

"Mimi niliteuliwa tu kusoma maamuzi ya mkutano yaliyofikiwa, maamuzi yalitolewa na mkutano, hakukuwa na mapinduzi yoyote," alisema.

Selasini alisema Halmashauri Kuu ya NCCR-Mageuzi au chama chochote hakina mamlaka ya kumfukuza mwenyekiti ya chama bali kina mamlaka ya kumsimamisha.

Kadhalika, alisema Halmashauri Kuu ya NCCR-Mageuzi imemsimamisha Mbatia na mamlaka yake yamewekwa chini ya Makamu Mwenyekiti Zanzibar.

Alisisitiza kuwa Mkutano Mkuu wa NCCR-Mageuzi uliitishwa ndipo ataweza (Mbatia) kujitetea na kujibu tuhuma zinazomkabili.

NMB FOUNDATION

## JOB ADVERTISEMENT
### General Manager - NMB Foundation

**Who we are**

NMB Foundation (NMBF) is a not-for-profit corporate social investment arm of NMB Bank Plc, which was established in 2021 to scale up its intervention in carefully chosen pillars that impact the lives of the majority of Tanzanians. As a good corporate citizen, NMB Bank is committed to addressing some of the UN SDG's.

NMB Foundation programs are designed to address issues of relevance specifically within the thematic areas of Education, Health, Agriculture, Environment, and Entrepreneurship. Through focused efforts towards the aforementioned areas, the foundation seeks to promote sustainable and wider economic inclusion. In order to accelerate the impact, we envision that the Foundation support model will comprise a combination of funding, social innovation and technical expertise. We leverage our network of branches and partners, our strong digital capabilities, and our resources to scale up our reach in the country.
Our Commitment.

NMB Foundation is committed to use various capabilities in partnerships, digital innovation, and expansive ecosystem to ensure notable impact and sustainable economic growth in our communities.

**Position Description** - General Manager NMB Foundation

**Contract Duration** - 3 years

Reporting to the Board of Trustees, this is an extraordinary opportunity for an individual with extensive program management experience to grow and further develop programs that will make significant impact.

**Key duties and responsibilities:**

- Foster accountability, leadership, diversity, and transparency of operations with the Senior Leadership Team as well as other advisory and decision-making bodies.
- Develop a high quality and innovative strategic plan, based on thorough contextual analysis, and using an inclusive and participatory process. Monitor and revise as required.
- Ensure proper alignment on priorities for NMB strategic initiatives (Education, Agriculture, Environment, Health, Entrepreneurship, and Innovation)
- Work in partnerships with others inside and outside of NMBF to achieve broad scale impact.
- Work with senior staff to generate a viable program pipeline in line with NMBF strategy and lead the development of an appropriate fundraising strategy for those programs.
- Ensure effective and efficient implementation of all programs and projects.
- Identify and secure adequate funding for ongoing and future program activities
- Ensure good stewardship of the funding, negotiating acceptable terms and conditions.
- Monitor NMBF's financial position and ensure the best use of available resources. This includes overseeing the development and review of NMBF annual budget, proper allocation of shared program costs (cost pools), development of unrestricted requests, review of financial transactions and reports, maximizing cost recovery from restricted grants and follow-up on audit recommendations.
- Establish a strong Human Resource strategy in line with NMBF Strategic Plan and ensure that systems are in place and being properly implemented for recruitment, staff development, performance management and compensation.
- Lead talent management and succession management in NMBF through the implementation of a comprehensive leadership development plan.

**Competencies**

- A strong self-motivated work ethic and action oriented, entrepreneurial, flexible, and innovative approach to operational management.
- Excellent organizational management skills with ability to coach senior-level staff to manage and develop high-performance teams and develop and implement program strategies.
- Strong human resource management skills including capacity building, coaching and conflict management.
- Deep experience in program budgeting and financial management with the ability to manage complex budgets.
- Strong written and verbal communication skills; a persuasive and passionate communicator with excellent public speaking skills.
- Strong interpersonal skills in establishing and maintaining collaborative relationships with donors and government counterparts.

**Qualifications and Experience**

- Bachelor's degree from an accredited university.
- Master's degree in Business Management, Economics, Social Science, or any other related field.
- At least 5 years in a senior management position in the development field.

Please send your application letter and curriculum vitae to **executives@nmbbank.co.tz** by **08/06/2022.**

***NMBF is committed to creating a diverse environment and is proud to be an equal opportunity employer.***

168739

# Babu ahukumiwa miaka 90 gerezani

**Na Said Hamdani,** LINDI

MAHAKAMA ya Wilaya ya Lindi imemhukumu mkazi wa Kijiji cha Namkongo, Kata na Tarafa ya Mipingo mkoani hapo, Salum Mtopa (70), kutumikia kifungo cha jumla ya miaka 90 gerezani baada ya kukutwa na hatia kwa makosa matatu, likiwamo la kumiliki shamba lenye bangi.

Hukumu hiyo ilitolewa jana na Hakimu Mkazi Mfawidhi wa Mahakama hiyo, Maria Batraine, baada ya kuridhishwa na ushahidi uliotolewa na upande wa mashtaka.

Kabla ya kutolewa kwa hukumu hiyo, Hakimu Batraine alimuuliza mshtakiwa kama ana sababu ya msingi itakayoishawishi mahakama isimpe adhabu kali, mshtakiwa huyo akiomba isimpe adhabu kali kwa madai ni mkosaji wa mara ya kwanza, umri wake umeshakwenda, pia anayo familia inayomtegemea yenye mke na wajukuu watano.

"Mheshimiwa hakimu, kama unavyoniona mimi sasa ni mzee na nina wajukuu wanaonitegemea, ukinipa adhabu kubwa watakosa huduma zangu," alijitetea Mtopa. Mwendesha Mashtaka, John Ijumba, alipoulizwa na hakimu kama mshtakiwa huyo ana rekodi ya kufanya makosa, alidai kuwa hana, huku akiiomba mahakama itoe adhabu kali ili iwe fundisho kwake na wengine walio na tabia ya aina hiyo.

"Mheshimiwa hakimu sina kumbukumbu ya makosa ya zamani kwa mshtakiwa, kupitia mahakama yako tukufu ninaomba impe adhabu kali ili kukomesha hii tabia kwa ajili ya kunusuru nguvu kazi ya Taifa letu," alidai.

Hakimu Batraine akitoa hukumu katika kesi hiyo ya jinai Na. 46/2021, alisema makosa aliyofanya mshtakiwa yapo kwa mujibu wa sheria, hivyo hana uwezo wa kubadilisha na kumuhukumu kosa la kwanza kukutwa na bangi kutumikia kifungo cha miaka 30 jela.

Pia kutumia kifungo cha miaka 30 kwa kosa la pili la kushiriki kilimo cha bangi na kukutwa na mbegu na adhabu ya aina hiyo kwa kosa la tatu la kusafirisha bangi. Kwa kuwa adhabu zinakwenda kwa pamoja, mshtakiwa atatumikia kifungo cha miaka 30 gerezani.

Hakimu alisema nafasi ya kukata rufani ipo wazi kama atakuwa hajaridhishwa na hukumu iliyotolewa na mahakama hiyo.

Ilidaiwa mahakamani huko na Mwendesha Mashtaka Ijumba kuwa mshtakiwa alifanya makosa hayo Julai 20, 2021 huko Namkongo, akidaiwa kukutwa na jumla ya Kg 151.99 za dawa za kulevya aina ya bangi. Kati yake, kilo 132.94 ni mbegu.

Ijumba pia alidai mshtakiwa alikutwa akimiliki shamba la kilimo cha bangi lenye ukubwa wa ekari 5.54 kinyume cha sheria za nchi.



Kamishna wa Sensa Tanzania Bara, Anna Makinda, akizungumza wakati akifungua kikao cha viongozi wa dini kuhusu maandalizi ya sensa ya watu na makazi ya mwaka 2022, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# EU, Aga Khan zatoa mil. 188/- kwa wajasiriamali

**Na Gwamaka Alipipi**

UMOJA wa Ulaya (EU) kwa kushirikiana na Mtandao wa Maendeleo wa Aga Khan (AKDN) umetoa ruzuku ya Sh. milioni 188.32 kwa ajili ya kuwawezesha wajasiriamali wadogo katika mikoa ya Lindi na Mtwara.

Fedha hizo zitawasaidia kukabiliana na athari za kiuchumi zilizowakumba wakati wa mlipuko wa UVIKO- 19.

kwa mujibu wa taarifa iliyotolea na msimamizi wa mradi huo Tanzania kutoka Aga Khan Foundation, Tarcile Mballa, ruzuku hiyo ni sehemu ya Mradi wa EU na Aga Khan wa kukabiliana na athari za UVIKO-19 katika mataifa ya Tanzania, Kenya Uganda na Msumbiji.

Mballa alisema muundo wa mradi huu walijifunza kutoka Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF) lakini taasisi nyingine ambazo zinatoa ruzuku.

Alisema kwa zaidi ya muongo mmoja Aga Khan Foundation imekuwa ikifanya kazi na vikundi vya kutunza akiba, kukopeshana, kwamba wakati UVIKO-19 shughuli zao ziliathirika.

"Lengo la mradi huu ni kuhakikisha vikundi vinarudi katika hali yake ya awali, lengo si kutoa ruzuku tu bali tunatarajia kuimarika kwa vikundi na kushuhudia ukuaji," alisema Mballa.

Mratibu wa mradi huo, Japhet Wangwe, alisema pamoja na kutolewa kwa ruzuku hiyo, Aga Khan Foundation kwa kushirikiana na wadau wengine wameanzisha mfumo wa kidijitali wa kuratibu shughuli za vikundi ili kuongeza usalama wa urahisi wa kufanya shughuli hizo nyakati zote.

Mkuu wa Wilaya ya Lindi, Shaibu Ndemanga, alisema ugonjwa wa UVIKO-19 ulileta athari mbili ambazo ni kiafya na kiuchumi.

Alisema walichokifanya Aga Khan Foundation ni kuunga mkono serikali ambayo imekuwa ikifanya juhudi za kuhakikisha kuwa wananchi wanajikwamua kiuchumi kupitia shughuli mbalimbali.

Serikali, alisema inatamani kuona ruzuku hiyo ikiongeza tija zaidi kwa wajasiriamali na kuwafanya kuwa wakubwa kwa kuwa inawatazama kama wafanyabiashara wakubwa wa siku zijazo na walipa kodi.

Mmoja wa wanufaika ruzuku hiyo, Deograsia Mbiku, alisema wakati wa UVIKO-19 biashara zao ziliathirika, hivyo hawakufanya marejesho kama ilivyo kawaida jambo ambalo liliathiri shughuli za kikundi chao.

# Mafunzo JKT yawe lazima kwa mbunge

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

MBUNGE wa Viti Maalum, Ester Bulaya, ameshauri mafunzo ya Jeshi la Kujenga Taifa (JKT) kwa wabunge vijana yawe ya lazima ili kuwajengea uzalendo na ukakamavu.

Wakati Bulaya akishauri hivyo, Mbunge wa Geita (CCM), Joseph Musukuma, ameshauri mafunzo hayo yawe kwa wabunge wote, wakiwamo wazee.

Hoja za wabunge hao zilitokana na tangazo lililotolewa bungeni jana na Mwenyekiti wa Bunge, Najma Murtaza Giga, kwamba wabunge vijana wanaohitaji kushiriki mafunzo hayo wajiandikishe kwa Katibu wa Bunge.

"Ofisi ya Bunge inatoa fursa kwa wabunge vijana ambao hawajapata mafunzo ya JKT kupata mafunzo hayo kwa lengo la kujenga nidhamu, uadilifu, utii, ukakamavu, uhodari, uvumilivu na uzalendo kwa nchi yao," alisema.

Kiongozi huyo wa Bunge alisema mafunzo hayo hufanyika katika Kikosi cha Makutupora kwa siku 38 na wapo wabunge wa Bunge hilo waliowahi kushiriki kwenye kambi mbalimbali.

"Kwa kuwa ofisi inakusudia kuomba nafasi kwa ajili ya kundi lingine kuanzia Julai 2022, wabunge vijana wenye nia na utayari wanaombwa kujitokeza kujumuishwa kwenye kundi hilo kushiriki mafunzo hayo," alisema.

Kutokana na tangazo hilo, Mbunge Bulaya alihoji kwanini mafunzo ya JKT kwa wabunge vijana yasiwe lazima ili wajengewe uzalendo na ukakamavu na nchi iwe na askari wa akiba kuanzia bungeni hadi mtaani.

"Kutokana na tangazo uliloltoa Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba mwongozo wako ni kweli wabunge vijana walikwenda JKT, kwanini sasa haya mafunzo yasiwe hiyari, yawe ya lazima? Na sisi wengine tulienda ni 'service girls' mwenyekiti," alisema.

Mbunge Musukuma alisema JKT ni sehemu ya kufundishwa uzalendo na kuhoji "kwanini wanabagua waende vijana badala ya wote na wazee?"

Akijibu miongozo hiyo, Mwenyekiti Giga alisema kuwa kwa sababu ilikuwa ni tangazo, atalirudisha kwa ajili ya kukaa na kutafakari vizuri jambo hilo.

Alisema kwa ambao hawajapata nafasi, wakiwamo wazee kama litaafikiwa, na yeye atakwenda kwa kuwa hajapata mafunzo hayo.

HABARI KITAIFA

# Waziri Gwajima aingilia kati sakata mtoto kudhalilishwa



**Na Jenifer Gilla**

WAZIRI wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Doroth Gwajima (pichani) ameagiza maofisa Ustawi wa Jamii wa Kata ya Bunju A waandike ripoti ya kisa cha mtoto (jina linahifadhiwa) aliyepigwa na baba yake kutokana na kufanyiwa ukatili wa kijinsia ili jamii ifahamu na kujifunza.

Waziri Gwajima alitoa agizo hilo jana, baada ya kutembelea kata huyo kushuhudia na kuongea na wazazi wa mtoto huyo aliyefanyiwa ukatili baada ya kupata taarifa ya tukio hilo kutoka kwa msamaria mwema.

"Naelekeza maofisa ustawi wa jamii wa kata hii, wilaya hii, na mkoa huu wakiandike kwa ushirikiano na huyu mama kijulikane, hii case report (kisa) tunaiita ambayo itasaidia vyombo vingine vinavyofanya kazi ya kufuatililia kisa hiki na sisi wote kama wataalam pamoja na jamii kuzidi kuelimishana kwa mifano sahihi," alisema. Gwajima amesema aliguswa na tukio baada ya juzi kupokea taarifa kutoka kwa raia mwema kuwa kuna mtoto amepigwa na baba yake kutokana na kufanyiwa ukatili wa kijinsia mara kwa mara na watu mbalimbali katika jamii anayoishi huku wazazi hao wakitafuta msaada bila mafanikio.

"Kwa hiyo wazazi wakaona kuwa huyu mtoto hawasikii wakaanza kumuadhibu, raia huyu hakufurahishwa ndipo nikatumiwa ujumbe nami nikaona kuwa hiki ni kisa kwa sababu unafanyiwa ukatili mtaani kisha unakuja kufanyiwa tena ukatili na wazazi. Nikaamua nije mimi mwenyewe nione, lakini nijifunze na nizame kwenye jamii nizungumze nao nione kuna kitu gani kinaendelea huku," alisema.

Hata hivyo, Waziri Gwajima aliwasihi wazazi pamoja na kuhangaika kwa ajili ya masuala ya kiuchumi wasisahau watoto wao kwa kuwa ukatili wa kijinsia kwa watoto unachochewa na wazazi kutumia muda mwingi wakitafuta pesa na kuwaacha wajilee wenyewe.

"Baada ya kusikiliza kisa chote kwa huyu mzazi nimejiridhisha kwamba mambo haya yalianza toka huko nyuma na ilitokana na kwamba mtoto anatoka shule anarudi nyumbani anajikuta yupo peke yake wazazi wote wameenda kwenye mihangaiko ya kiuchumi. Mtoto huyu amefanyiwa ukatili na watu wa ndani. Yupo mtu pamoja na wengine wanaoishi pale ambapo mtoto akirudi shule anafungua mlango anadakwa anafanyiwa vitendo vya ukatili," alisema.

Alisema chanzo kingine cha kuenea vitendo hivyo ni kutokuwa na ulinzi wa kutosha au kutokuwa na uelewa wa kutosha katika maeneo ambayo watoto hao wanaishi ikiwamo shuleni hali inayowapa mwanya watu wenye nia ovu.

Waziri alizitaka kamati za ulinzi wa wanawake na watoto kuanzia ngazi ya kata kuwa imara na kushirikiana na wazazi kutoa elimu kwa jamii ili ifahamu kamati hiyo na kubaini watoto waishio kwenye mazingira hatarishi.

Mama wa mtoto aliyefanyiwa vitendo hivyo (jina tunalihifadhi), alisema kuwa alimgundua mwanawe baada ya kumuona ana hofu muda wote na kuamua kumchunguza.

"Mienendo yake ilibadilika akawa ana hofu muda wote nikapata wasiwasi nikaanza kumfuatilia ndipo akagundua kuwa anafanyiwa vitendo hivyo na nilipomuuliza alikiri na kunitajia mtu aliyemfanyia ambaye ni jirani yetu," alisema.

Baada ya kupata taarifa hiyo, alisema alikwenda mamlaka husika kutoa taarifa bila kupata msaada wowote, lakini anashukuru msamaria mwema kutoa taarifa kwa waziri husika na sasa ana uhakika wa kupata haki ya udhalilishaji aliofanyiwa mtoto huyo.

"Ninaishukuru Wizara ya Maendeleo ya Jamii, kupitia Waziri Gwajima kwa kujitokeza na kusimamia suala hili sasa nipo kwenye mchakato wa kupata haki ya mtoto wangu," alisema.

Mama huyo mwenye watoto wawili aliwashauri wazazi kuwa karibu na watoto wao kwa kuwa umbali waliokuwa nao kwa mtoto wao ndiyo uliowapa mwanya watu wasio na malengo mema kumfanyia vitendo vya udhalilishaji mtoto wao.

"Ninaomba wanawake wenzangu tuwe karibu na watoto wetu, tusiruhusu mtu yeyote atuharibie watoto wetu, tujenge urafiki na watoto ili pale wanapofanyiwa au kutaka kufanyiwa vitendo hivyo watoe taarifa kwetu," alisema.

Mtendaji wa Mtaa wa Kata ya Bunju, Oinesy Ndalanda, alisema baada ya kupata taarifa ya kuwapo kwa mtoto anayepigwa walifika eneo husika na kumchukua kumpeleka hospitali kwa ajili ya matibabu.

Alisema baada ya kumhoji mtoto huyo alikiri kufanyiwa vitendo vya udhalilishaji na watu tofauti akiwa katika maeneo ya shule na watu hao wakimtisha asitoe taarifa ya vitendo hivyo kwa mtu yeyote.

Naye jirani aliyetuma ujumbe kwa Waziri Gwajima (jina tunalihifadhi), alisema alichukua uamuzi huo baada ya kuona mateso anayopitia mtoto huyo ikiwamo kupigwa na wazazi wake wakidhani kuwa anapenda kufanyiwa vitendo hivyo.

"Niliona kuwa hili tatizo linahitaji kumfikia waziri ili aingilie kati kwa sababu wazazi walionekana kuzidiwa na kutokujua wafanye nini baada ya kuhangaika kutafuta msaada wa kumnusuru mtoto wao dhidi ya ukatili huo bila mafanikio, sasa zile hasira zao wakawa wanazitoa kwa kumpiga mtoto," alisema.

Jirani huyo alimshukuru Waziri Gwajima kwa kuitikia wito mara moja na kulishughulikia tatizo hilo na kuisihi jamii kuchukua hatua pale wanapoona vitendo visivyostahili vinaendelea katika jamii.

Mpaka gazeti hili linaingia mitamboni, baba wa mtoto huyo alikuwa ameshikiliwa na polisi kwa kosa la kumpiga na kumsababishia maumivu.

NMB
Karibu yako

TAARIFA YA MKUTANO MKUU WA 22 WA WANAHISA WA BENKI YA NMB

**Taarifa inatolewa kwamba Mkutano Mkuu wa 22 wa mwaka wa wanahisa wa NMB utafanyika katika ukumbi wa Julius Nyerere International Convention Centre, Dar es Salaam saa 4 asubuhi siku ya Ijumaa, Juni 3, 2022. Agenda itakuwa kama ifuatavyo:**

22.1 MATANGAZO NA AKIDI

22.2 KUPITISHA AJENDA ZA MKUTANO

22.3 KUTHIBITISHA KUMBUKUMBU ZA MKUTANO MKUU WA 21 ULIOFANYIKA TAREHE 4 JUNI 2021

22.4 YATOKANAYO NA MKUTANO WA 21 WA WANAHISA

22.5 KUPOKEA, KUJADILI NA KUPITISHA RIPOTI YA WAKURUGENZI NA TAARIFA ZA FEDHA KWA MWAKA ULIOISHIA 31 DISEMBA 2022

22.6 KUIDHINISHA GAWIO KWA MWAKA ULIOISHIA 31 DISEMBA 2021

22.7 KUPOKEA NA KUIDHINISHA MALIPO YA WAKURUGENZI

22.8 KUJIUZULU NA UTEUZI WA WAKURUGENZI

22.9 KUPOKEA NA KUTHIBITISHA UTEUZI WA WAKAGUZI WA HESABU KWA MWAKA UNAOMALIZIKA 31 DISEMBA 2022

22.10 MENGINEYO

**MAELEZO MUHIMU**

1. Mwanachama anayetarajia kuhudhuria Mkutano lazima aje na nakala yake ya risiti ya uwekezaji wa hisa (Depository receipt) au kitambulisho chake au kadi yake ya benki.
2. Mjumbe anayeruhusiwa kuhudhuria na kupiga kura kwenye Mkutano anaruhusiwa kuchagua mwakilishi kuhudhuria na kupiga kura kwa niaba yake kwa kufuata /kuzingatia taratibu na Sheria za Kampuni kama zilivyorekebishwa. Fomu ya uwakilishi lazima iwasilishwe kwenye ofisi iliyosajiliwa ya Kampuni kabla ya saa 4 asubuhi Alhamisi ya tarehe 2 Juni 2022.
3. Mwanachama anayetarajia kuhudhuria kikao atatakiwa kuhudhuria kwa gharama zake mwenyewe. Nakala za taarifa ya mwaka na fomu za mwakilishi zitapatikana matawini.
4. Wakurugenzi wamependekeza ulipwaji wa gawio la shilingi 193 kwa kila hisa, inayoleta jumla ya shilingi 96.7 bilioni kutokana na faida ya mwaka 2021.

**Tarehe za kuzingatia:**

| | |
|---|---|
| **Tarehe ya tangazo:** | **- 13 Mei 2022** |
| **Hisa kuuzwa pamoja na gawio :** | **- 13 Mei 2022** |
| **Mwisho wa hisa kuuzwa pamoja na gawio :** | **- 1 Juni 2022** |
| **Hisa kuanza kuuzwa bila gawio:** | **- 2 Juni 2022** |
| **Daftari la wanahisa kufungwa:** | **- 6 Juni 2022** |
| **Malipo ya gawio kwa wanahisa: kuanzia tarehe** | **- 15 Juni 2022** |

Lilian R. Komwihangiro
**Katibu wa Kampuni**

13 Mei 2022

168742

www.nmbbank.co.tz

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Ushauri wa Chongolo kwa vijana usipuuzwe

**JUZI** Katibu Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Daniel Chongolo, alipokuwa mkoani Pwani, aliwaeleza vijana njia ya kusaidia kutatua tatizo la ajira kwa kutumia nguvu kazi yao katika uzalishaji.

Ajira kwa vijana limekuwa tatizo kubwa si kwa Tanzania pekee bali ulimwenguni.

Vijana ambao ni tegemeo kubwa katika nguvukazi ya uzalishaji, wengi wao wanazagaa mitaani kwa kukosa ajira licha ya baadhi yao kuhitimu elimu ya chuo kikuu.

Akiwa mkoani humo, Chongolo aliwaasa wanafunzi wa Shule ya Uongozi ya Mwalimu Julius Nyerere, kuhakikisha wanashirikiana na viongozi wao kutumia nguvu kazi iliyoko hasa ya vijana katika uzalishaji ambayo itasaidia kutatua tatizo la ajira.

Vijana 120 kutoka vyama sita vya ukombozi Kusini mwa Afrika wanashiriki mafunzo hayo kuwajengea uwezo wa kutoa maamuzi kwenye vyama vyao.

Ushiriki wa vijana katika mafunzo mbalimbali huwajengea uwezo na kusaidia kupunguza tatizo la ajira kwenye nchi zao ambalo linasumbua kwa sasa.

Vijana wanatakiwa kutumia vizuri mafunzo wanayoyapata kwenye vyuo wanavyosoma ili wanapomaliza wawe na ujasiri wa kutumia elimu waliyopata kujiajiri.

Vyuo vingi vinatoa elimu ili wahitimu waweze kuitumia kujitegemea katika mambo mbalimbali, iwe kazini au katika jamii.

Mwamko wa vijana kujiunga na elimu ya juu umekuwa mkubwa kwa sababu ya kutambua kuwa bila elimu katika karne hii upatikanaji wa ajira ni mgumu.

Hata waliosoma na kumaliza vyuo wanaonekana mitaani wakihangaika kutafuta kazi kwa sababu nafasi za ajira zimekuwa chache.

Ndiyo maana vijana wanahamasishwa kujifunza kujiajiri ili elimu waliyoipata iwasaidie katika shughuli zao watakazo zianzisha.

Kuna watu ambao wamesomea fani fulani, lakini kwa sababu ya ukosefu wa ajira anaamua kufanya kazi yoyote atakayoipata tofauti na fani yake ili asihangaike mitaani na vyeti kutafuta kazi.

Chongolo alipokuwa katika Chuo cha Mwalimu Nyerere kufungua mafunzo ya awamu ya tatu ya chuo hicho ambayo ni maalumu kwa makada vijana, yatajikita katika uongozi kwenye masuala ya maslahi, itikadi na misingi ya ujamaa.

Makada hao vijana watajifunza namna vyombo vya maamuzi kwenye vyama vyao na serikali vina nguvu kiasi gani na vinafanyaje kazi katika kuisaidia serikali kuhakikisha wanayafikia yale ambayo wananchi wana kiu nayo.

Wametakiwa kujua vyombo vya maamuzi kwenye vyama vyao na kero za wananchi na namna ya kuyashughulikia kulingana na mabadiliko yaliyopo sasa.

Vyama vilivyopeleka vijana wao katika chuo hicho vimetoa nafasi kwa makada hasa wa kizazi cha sasa kukaa pamoja kujifunza masuala ya uongozi kwa kuzingatia mabadiliko ya wakati na nyakati na yatakayosababisha kuboresha vyama vyao.

Chongolo alikishukuru chama tawala cha China kwa kusaidia kufanikisha mafunzo hayo, na kusema kuwa nchi hiyo imekuwa marafiki wa Tanzania kwa muda mrefu na kusaidia katika mambo mbalimbali ya kimaendeleo.


Kabla ya kuanzishwa kwa shule hiyo hapakuwa na sehemu ya kuandaa vijana kuwajenga kistadi ili kuwa tayari na mabadiliko.

Kwasasa dunia inaenda kwa kasi hivyo ni lazima viongozi waandaliwe na kazi inayofanywa kwa sasa ni kutengeneza viongozi wa nchi wanaoendana na mabadiliko yaliyopo.

Mafunzo hayo yanahusisha vijana kutoka katika vyama vya ANC-Afrika Kusini, CCM-Tanzania, FRELIMO-Msumbiji, ZANU PF - Zimbabwe, SWAP-Namibia na MPLA-Angola.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

# Kwa tunayoshuhudia miundombinu ya Dar, Mama Samia pokea tuzo yangu

Na Adam Fungamwango

**UNAPOZUNGUKA** kwenye Jiji la Dar es Salaam kwa sasa utashangaa sana. Ni tofauti na zamani. Miaka ya nyuma, maghorofa yalikuwa maeneo ya Kariakoo tu, Posta na Stesheni. Kwa sasa jiji zima lina maghorofa, hata zile sehemu ambazo zinaitwa uswahilini.

Achana na hilo, serikali iliposema kuwa inataka kujenga barabara ya juu maeneo ya Tazara ili kupunguza foleni, baadhi ya wengi hawakuamini.

Moja, hawakuamini kama Tanzania tunaweza kweli kuwa na aina hizo za barabara ambazo huwa tunaziona kwenye nchi mbalimbali hasa barani Ulaya.

Wengine walikuwa na wasiwasi kuwa huenda mradi huo ukaishia kati na hautokamilika. Ujenzi ukaanza, na mwaka 2018, aliyekuwa Rais Dk. John Magufuli alizindua rasmi barabara hiyo na kuipa jina la Daraja la Mfugale.

Ulibaki kuwa mashangao kwa watu wengi kwa jinsi mradi huo kukamilika, lakini hata kutazama tu mandhari yenyewe ilivyopendezesha eneo lote la Tazara, huku magari sasa yakiwa hayakutani kama zamani, kwenye barabara ya Nyerere na Mandela.

Ile ya Nyerere inayotoka mjini hadi Uwanja wa Ndege wa Julius Nyarere, ikifika maeneo hayo inainuka juu na kuiacha ile ya Mandela inayotoka maeneo ya Ubungo, Tabata na Buguruni ikipita chini kuelekea maeneo ya Temeke, uwanja wa mpira wa miguu wa Benjamin Mkapa, viwandani hadi bandarini.

Ujenzi wa daraja hilo la juu, umesababisha kupungua kwa foleni iliyokuwa ikionekana nyakazi za asubuhi maeneo ya Tabata, Buguruni, Tazara yenyewe na maeneo jirani na hapo, huku ukimaliza kero kwa wasafiri wa ndege ambao kuna wakati walikuwa wanachelewa kufika uwanjani.

Wakati watu wakishangaa daraja hilo, likamalizika la Ubungo ambalo nalo likaitwa la Kijazi. Hili ni la kuunganisha barabara za Morogoro, Mandela na Sam Nujoma. Zamani zilikuwa zinaungana moja kwa moja na kusababisha foleni kubwa.

Ukiwa Manzese, maeneo ya Chuo Kikuu, Mwenge, maeneo ya kuelekea Tabata na hata Kimara ni foleni tupu. Kwa sasa zinapishana kwa juu na chini.

Pande zote zina barabara za juu na chini, pia ambazo hazikutani, hivyo kusababisha kila upande gari zipite bila bugudha ya kukutana na barabara nyingine. Daraja hili nalo limesababisha kupungua sana kwa foleni maeneo hayo.

Tunaipongeza serikali kwa kutekeleza mipango na miundombinu hiyo ambayo imetumia gharama kubwa sana, lakini faida yake ni kwamba imewafanya wananchi wawahi makazini na majumbani kwao.

Pia hata pato la taifa linaongezeka kwa wafanyakazi kuwahi maofisini na mpaka naandika hili, bado kuna maeneo mengine korofi yanaendelea kushughulikiwa, yakiongozwa na makutano ya barabara ya Nyerere na Kawawa.

Hili ni eneo sugu kwa foleni kwa wasafiri wanaotoka mjini kwenda Keko, Temeke, Tandika, Mbagala na maeneo mengine ya huko.

Kunakuwa na foleni kuwa kuanzia maeneo ya Msimbazi Centre, Boma, Karume, mpaka maeneo ambayo reli ya kati inakatisha, kabla ya kuikuta barabara ya Nyerere.

Foleni ya kuanzia Boma hadi kwenye makutano hayo tu, abiria wanaweza kukaa hata masaa mawili. Ni eneo korofi sana. Nadhani kama daraja hilo la juu ambalo pia lipo kwenye matengenezo likiisha, robo tatu ya kero za foleni Dar es Salaam zitakuwa zimeisha.

Na kama mpango wa kujenga daraja la juu kwenye makutano ya barabara ya Sam Nujoma na Bagamoyo maeneo ya Mwenge, Kawawa na Morogoro maeneo ya Magomeni Mapipa utamalizika, nadhani suala la foleni kwenye jiji la Dar es Salaam linaweza kuwa na sura ya historia.

Kwa hili tu ambalo tayari tumeliona kwa madaraja ya Kijazi na Mfugale, hata lile linaloendelea kujengwa pale maeneo ya Keko Veta, serikali yetu ambayo kwa sasa inaongozwa na Rais Samia Suluhu Hassan inastahili sifa na pongezi, kwani ilifika wakati Dar es Salaam kupanda gari, iwe binafsi au daladala ilionekana kero tupu kwa foleni.

Lakini kwa sasa watu wanapita tu mabasi au magari yao kwenye makutano ya barabara kuu, bila ya matatizo juu na chini, kila mmoja akienda anakoelekea bila matatizo.

# Kliniki himofilia kupunguza mzigo matibabu

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

KUZINDULIWA kwa kliniki ya matibabu ya ugonjwa wa himofilia katika Hospitali ya Rufani ya Kanda ya Benjamini Mkapa, kutawezesha wagonjwa wa aina hiyo kupatiwa matibabu hospitalini hapo badala ya Muhimbili kama ilivyokuwa awali. Himofilia ni ugonjwa wa kutoganda damu kwa haraka pale mgonjwa anapopata jeraha katika sehemu ya mwili. Katibu wa afya kutoka Wizara ya Afya, Editha Bakari, alibainisha hayo kwa niaba ya Kaimu Mkurugenzi wa Tiba wa Wizara hiyo, Dk. Paulo Mhame, wakati wa uzinduzi wa kliniki hiyo uliofanyika jana hospitalini hapo.

Bakari alisema kuletwa kwa kliniki hiyo Dodoma, kutasaidia kwa kiasi kikubwa kuwapunguzia gharama wagonjwa wa himofilia na selimundu ambao walikuwa wakisafiri kutoka mkoani hapa na mikoa jirani kwenda Hospitali ya Taifa ya Muhimbili, kwa ajili ya kupata matibabu hayo.

"Tunashukuru wafadhili wa mradi wa Novo Nodisk Haemophilia Foundation kwa msaada waliotoa kwa Hospitali ya Taifa ya Muhimbili na hospitali zingine nchini ikiwamo ya Benjamini Mkapa kwa kutoa mafunzo kwa wataalamu 313 wa afya," alisema Bakari.

Hata hivyo, alisema Tanzania inasadikiwa kuwa na zaidi ya wagonjwa 6,000 lakini waliopo kwenye kanzidata ni 172 ambao hupatiwa matibabu hivyo aliwataka wataalamu waliopata mafunzo kuendelea kutoa elimu ili kuhakikisha jamii inaelewa na kuwaleta wagonjwa kupata matibabu.

Awali, akimkaribisha mgeni rasmi, Dk. Hedwiga Swai kutoka Hospitali ya Taifa ya Muhimbili alisema serikali inaendelea na jitihada mbalimbali za kuhakikisha wagonjwa wa himofilia wanaendelea kupata matibabu yao katika hospitali zote. Alisema wanafanya hivyo ili kuhakikisha wanaboresha huduma ya wagonjwa wa himofilia na selimundu nchini na kwamba tangu kuanzishwa kwa mradi huo wa kuongeza kasi ya upatikanaji huduma kwa wagonjwa wa damu umeleta tija kubwa kwa wananchi.

Alitaja baadhi ya mafanikio yaliyopatikana kupitia mradi huo kuwa ni pamoja na ukarabati wa kliniki kubwa ya himofilia nchini katika Hospitali ya Muhimbili pamoja na samani za ofisi. Mgaza Mhina kutoka chama cha wagonjwa wanaoishi na ugonjwa wa damu kutoganda haraka pale wanapopata majeraha (HIMOFILIA) aliiomba serikali kuongeza nguvu katika kugharamia matibabu yao ili kupunguza vifo na ulemavu wa kudumu kwa wale wanaoshindwa kumudu gharama za matibabu. Mhina alisema matibabu ya ugonjwa huo yako juu sana na yanapatikana kwa gharama kubwa hivyo ni vema serikali ikaliangalia hilo ili kuwanusuru wagonjwa waliopata maradhi hayo.

# Wenye ulemavu wataka nao kushirikishwa sensa

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

WATU wenye ulemavu jijini Mbeya, wameiomba serikali kuwakumbuka kwenye mchakato wa Sensa ya Watu na Makazi inayotarajiwa kufanyika Agosti 23, 2022 ili kuhakikisha hakuna mtu atakayeachwa katika jambo hilo.

Wakizungumza na Nipashe jana, baadhi ya wenye ulemavu hao walisema ni vyema kila mtu akahusishwa kwenye sensa hiyo kwa kuwa linamhusu kila raia wa Tanzania.

Lilian Mwakitalima, ambaye ni kiziwi alisema hawajapewa mwongozo wa aina yoyote na serikali namna watakavyoshiriki kwenye sensa ya watu na makazi huku akisema taarifa kuhusu mwenendo huo anazipata kupitia vyombo vya habari.

Katika mahojiano na Nipashe, Mwakitalima akiongozwa na mkalimani wake wa lugha ya alama, alisema si viziwi wote wamepata taarifa sahihi kuhusu suala hilo angalau wale wenye uelewa kama yeye ndio wanafahamu mchakato huo.

"Tuna hofu namna tunavyoshirikishwa. Sisi tupo wengi lakini hatujapewa elimu ya namna ya kushiriki. Binafsi hizo taarifa nimezipata kupitia vyombo vya habari, lakini si wote wanazipata kwa kuwa vyombo vingi vya habari havina wakalimani. Hata kama wapo kwa mfano kwenye runinga wanaonekana kwenye picha ndogo ambayo inawapa shida viziwi kufuatilia," alisema.

Alisema kuna umuhimu wa kuwashirikisha viziwi angalau kwa uwakilishi ili iwe rahisi kuwatambua na kuwasiliana na wenzao wakati wa mchakato huo ili kupata taarifa zote muhimu kwa kila kiziwi.

Mwenyekiti wa Chama cha Watu wenye Ulemavu wa Viungo jijini Mbeya, Damas Mwambeje, alisema kupitia umoja wao wameanza kukutana mara kwa mara kwa ajili ya kupeana hamasa ya kushiriki kwenye sensa.

Alisema kwa sasa hakuna takwimu halisi za watu wenye ulemavu, hivyo kupitia sensa serikali itajua idadi yao ili iwe rahisi kuwapa mahitaji yao ya msingi ikiwepo kuratibu swala mikopo ya asilimia mbili zinazotolewa na halmashauri.

"Tumekuwa tukifanya vikao kila baada ya miezi mitatu ili kuhamasishana lakini hata vikao vya kawaida tunapokutana walemavu watatu hadi kumi lazima tusisitize swala la kujiandaa kushiriki suala hilo," alisema Mwambeje.

Mkuu wa Wilaya ya Mbeya ,Dk. Rashid Chuachua, alisema hakuna mtu atakayeachwa kuhesabiwa huku akisisitiza kila mtu ajiandae kwa ajili kushiriki na kwamba swala la uratibu linakwenda vizuri.

Aliongeza kuwa kundi la watu wenye ulemavu lina wawakilishi kwenye kamati zote zinazohusika na masuala ya uratibu wa maandalizi ya sensa katika wilaya yake hivyo anauhakika kupitia uwakilishi huo.

"Zoezi hili linawahusu watu wote hata kama wana matatizo lazima wahesabiwe, hivyo niiombe jamii itusaidie ili tuweze kuwapata wote, asitokee mtu hata mmoja ambaye atamficha ndani mtu mwenye ulemavu,' 'alisema Dk. Chuachua.

"Sensa haiangalii tu idadi ya watu peke yake bali pia rasilimali za watu wanazomiliki, nyumba kwa maana makazi, vyoo pamoja na kujua aina ya walemavu kwenye jamii husika. Mfano kuna wenye ulemavu wasiosikia, viziwi na wengine hivyo ni lazima wote wahesabiwe,' 'aliongeza Dk. Chuachua.

Kuhusu viziwi, alisema alikutana nao ili kujua ni kwa namna gani watashiriki kwenye jambo hilo na walikuja na hoja ya kupata mkalimani kwa ajili ya kurahisisha mawasiliano wakati wa kuhesabiwa, akiahidi kuwa swala hilo linashughulikiwa na serikali lengo likiwa ni kuondoa vikwazo vyote ili zoezi lifanyike kwa ufanisi.

# NOTISI/TANGAZO

**MUDU COMPANY LTD, NUTMEG AUCTIONEERS & PROPERTY MANAGERS CO.LTD,LEGENDS AUCTION MART LTD ,SALEI AUCTION MART LTD,CHAMPION AUCTION MART,MAKI RECOVERIES LTD,PSALM AUCTION MART,MALAPA AUCTION MART,HEDANE ENTERPRISES LTD,KILICRAALS AUCTIONEER, DESTENI COMPANY LIMITED, MASE INTERNATIONAL LTD,TAUSI AUCTION MART,MASETO AUCTIONEER AND DEBT COLLECTORS,JY AUCTIONEERS CO.LTD, SMARKCORE GROUP LTD, WAUNGWANA AUCTION MART LTD, BEST GROUP LTD, NGOMENI AUCTION MART,MOPEH COMPANY LTD,KOTI BROTHERS LTD,MBUZAX AUCTION MART** kwa mamlaka tuliyopewa na Jamhuri ya Muunganowa Tanzania, chini ya benki ya **AKIBA COMMERCIAL BANK PLC**, tunatoa notisi ya kulipa madeni kwa wadaiwa wafuatao ndani ya siku 14 kuanzia tangazo hili, Vinginevyo, tutafanya Minada ya hadhara kama ratiba inavyoonyesha.

| TAWI ALILOKOPA | JINA LA MTEJA | AINA YA DHAMANA | JINA LA MWENYE DHAMANA | MAHALI DHAMANA ILIPO | TAREHE YA MNADA |
|---|---|---|---|---|---|
| MBEYA | KIVAULA MLIMKA LUHANGA | NYUMBA (2) | KIVAULA MLIMKA LUHANGA | MBEYA MJINI NA TUNDUMA | 24/06/2022 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| MBEYA | VENANCE JISKAKA MWAKYABALA | NYUMBA | VENANCE JISKAKA MWAKYABALA | MWANJELWA , MBEYA MJINI | 23/06/2022 SAA 4:00 ASUBUHI NAKUENDELEA |
| MWANZA | MALALE COSTANTINE KISAKA | NYUMBA | MALALE COSTANTINE KISAKA | NYAMHONGORO-MWANZA | 10/06/2022 SAA 4:00 ASUBUHI NAKUENDELEA |
| MWANZA | FELISTER MATOKE NYANGWE | NYUMBA | FELISTER MATOKE NYANGWE | KISEKE-MWANZA | 11/06/2022 SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| MAIN | ANSELEM JEROME SINDATO | NYUMBA | SAID ISSA MKONINGO | PUGU KINYAMWEZI | 15/06/2022 SAA 4:00 ASUBUHI NAKUENDELEA |
| DODOMA | STEPHANO CHACHA NYAMHANGA | NYUMBA | STEPHANO CHACHA NYAMHANGA | MIYUJI-DODOMA | 10/06/2022 SAA 3:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| DODOMA | SESILIA MALTIN MAGOMBA | PAGALE | SESILIA MALTIN MAGOMBA | CHIDACHI-DODOMA | 16/06/2022 SAA 4:00 ASUBUHI NAKUENDELEA |
| TEMEKE | RASHID SAID NGOMBO | NYUMBA | RASHID SAID NGOMBO | CHANIKA GOGO-ZINGIZIWA | 17/06/2022 SAA 4:00 ASUBUHI NAKUENDELEA |
| TEMEKE | SALUM MOHAMED MBEGU | KIWANJA | SALUM MOHAMED MBEGU | TUNDWI SONGANI-KIGAMBONI | 15/06/2022 SAA 04:00 ASUBUHI NAKUENDELEA |
| TEMEKE | ZAINABU RASHIDI LUKWELE | NYUMBA | OMARI SAIDI MAINGO | MKURANGA | 16/06/2022 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| TEMEKE | JOSEPH PATRICK NCHIMBI | NYUMBA | JOSEPH PATRICK NCHIMBI | KAZOLE-VIKINDU | 16/06/2022 SAA 4:00 ASUBUHI NAKUENDELEA |
| KIJITONYAMA | ISAYA MELKIOR MBOYA | NYUMBA | ELIZABETH MGONZO | KING'AZI B | 10/06/2022 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| ARUSHA | HEALSUN PRE AND PRIMARY SCHOOL | NYUMBA | LILIAN PHILEMAN LAIZER & EDWARD N. LAIZER | SEKEI-ARUSHA | 14/06/2022 SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| ARUSHA | RAHIM BAKARI SAID | NYUMBA | BAKARI SAID MSUYA | SOKONI 1-ARUSHA | 15/06/2022 SAA 4:00 ASUBUHI NAKUENDELEA |
| ARUSHA | MARY BALTAZARY SHAYO | NYUMBA | MARY BALTAZARY SHAYO | ARUSHA (SOKONI-ENGOSENGIU) | 15/06/2022 SAA 4:00 ASUBUHI NAKUENDELEA |
| ARUSHA | SOINE LENAISIWAN MOLLEL | SHAMBA | SOINE LENAISIWAN MOLLEL | MESERANI | 17/06/2022 SAA 4:00 ASUBUHI NAKUENDELEA |
| ARUSHA | TAJIRI WAPII LENASIWAN | SHAMBA | TAJIRI WAPII LENASIWAN | MESERANI | 17/06/2022 SAA 4:00 ASUBUHI NAKUENDELEA |
| KIJITONYAMA | MAMII BUSINESS CENTRE | NYUMBA-HATI NAMBA46339 | MARY JAMES MNYUNE | BOKO-KINONDONI | 11/06/2022 SAA 4:00 ASUBUHI NAKUENDELEA |
| MBAGALA | SABRINA ABDALLAH MAKARANI | NYUMBA | HAFIDHU SUREIMAN GITTA | PEMBA MNAZI-KIMBIJI | 13/06/2022 SAA 4:00 ASUBUHI NAKUENDELEA |
| MBAGALA | ISSA SAID NZENGI | NYUMBA | NASSORO RASHIDI LUKINDO | CHAMAZI | 14/06/2022 SAA 4:00 ASUBUHI NAKUENDELEA |
| MBAGALA | MARIAM MOHAMED RAMADHANI | NYUMBA | MARIAM MOHAMED RAMADHANI | CHAMAZI DOVYA | 14/06/2022 SAA 04:00 ASUBUHI NAKUENDELEA |
| MBAGALA | LATIFA MOSHI MLANZI | NYUMBA | SALUMU OMARI AMIRI | MWANDEGE - MKURANGA | 15/06/2022 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| MBAGALA | OBONYO LAWRENCE SEDA | NYUMBA | OBONYO LAWRENCE SEDA | CHATEMBO - MWANDEGE | 15/06/2022 SAA 4:00 ASUBUHI NAKUENDELEA |
| MBAGALA | MARIAM MOHAMED LIKWAYU | NYUMBA | MARIAM MOHAMED NA MATATIZO CHEMBERA | KWA NDEVU- KISEMVULE | 17/06/2022 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| MBAGALA | PAULO JACOB MHAMARY | NYUMBA | HASSAN MOHAMED TINDWA | KIPARANGANDA - MKURANGA | 16/06/2022 SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| MBAGALA | NATHAN MASUMBUKO DANGA | NYUMBA | NATHAN MASUMBUKO DANGA | MKURANGA | 21/06/2022 SAA 4:00 ASUBUHI NAKUENDELEA |
| MBAGALA | ZAINABU LUPA SUDI | NYUMBA | RAJAB MTORO RAJABU& ZAINABU LUPA | MBAGALA ZOMBOKO | 22/06/2022 SAA 4:00 ASUBUHI NAKUENDELEA |
| MBAGALA | TRAZIAS BERNARD ISHENGOMA | NYUMBA | TRAZIAS BERNARD ISHENGOMA | MBAGALA MWANAMTOTI | 23/06/2022 SAA 4:00 ASUBUHI NAKUENDELEA |
| AGGREY | MALIKI MOHAMED MADIGADI | NYUMBA | MALIKI MOHAMED MADIGADI | VIKINDU | 17/06/2022 SAA 4:00 ASUBUHI NAKUENDELEA |
| AGGREY | MPOKI ROWN MWAIPASI | NYUMBA NA KIWANJA | MPOKI BROWN MWAIPASI | GONGOLAMBOTO NA KILUNYA | 29/06/2022 SAA 4:00 ASUBUHI NAKUENDELEA |
| AGGREY | KOKUBELWA PAUL NGAMBEKI | KIWANJA | KOKUBELWA PAUL NGAMBEKI | MPIJI MAGOE | 13/06/2022 SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| AGGREY | NEEMA ERNEST KASILILIKA | NYUMBA | DASTAN SEVERIN CHANDE | MANZESE | 30/06/2022 SAA 4:00 ASUBUHI NAKUENDELEA |
| UKONGA | ROBERT CHACHA NYAMBARI | NYUMBA | ROBERT CHACHA NYAMBARI | KITUNDA MTAA WA KINYANTIRA | 13/06/2022 SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |

**MASHARTI YA MNADA**

1 Mnunuzi atalazimika kulipa 25% ya bei ya Nyumba, Kiwanja au Shamba ,papo hapo baada ya mnada kumalizika na 75% itakayobaki italazimika kulipwa ndani ya siku 14.
2 Ikiwamnunuziatashindwakutimizashartilolote la mnada kuhusiana na malipo yaawali,hatarudishiwapesayoyotealiyokwishailipa.
3 Kwa mawasiliano zaidi; tupigie simu no.0689349477/0719351040/0754497396/0762318636/0621800779/0715363537/0784252048/0768672367
4 Iwapo ndani ya siku 60 mnunuzi hajakabidhiwa nyumba benki itarudisha kiasi cha fedha kilichowekwa na mnunuzi benki bila gharama yeyote.

# Taasisi mpya yatangaza neema mafunzo kitendaji

**Na Mwandishi Wetu**

TAASISI mpya ya Uhusiano na Mawasiliano ya Umma Tanzania (IPRT) imetangaza kutoa mafunzo kuhusu mawasiliano ya kimkakati mahusus kwa watendaji wakuu, maofisa mawasiliano, maofisa utumishi na maofisa mbalimbali katika mashirika.

Akizungumza wakati wa hafla fupi ya uzinduzi wa taasisi hiyo iliyofanyika jijini Dar es Salaam jana na kuhudhuriwa na wadau kutoka taasisi mbalimbali na vyombo vya habari, Mratibu wa Mafunzo kutoka IPRT, Evarist Ngalimuwili, alisema wazo la kuanzishwa kozi hiyo linachagizwa zaidi na uwapo wa vikwazo katika eneo la uhusiano na mawasiliano ya umma kimkakati miongoni mwa taasisi mbalimbali nchini.

Kwa mujibu wa Ngalimuwili, katika kufanikisha mpango huo, taasisi hiyo imejipanga kushirikiana na taasisi mbalimbali zinazotambulika kwa weledi katika ufundishaji wa masuala hayo zikiwapo za ndani na nje ya nchi na kutumia wahariri wabobevu kwenye masuala ya mawasiliano na uhusiano wa umma katika utoaji wa kozi hizo.

"Mpango huu utahusisha ushirikiano baina yetu na Chuo Kikuu cha Daystar cha Kenya ambao ni wabobevu katika masuala haya na kwa kuanzia tunatarajia kuanza na kozi mahususi kwa watendaji wakuu wa mashirika na taasisi mbalimbali, maofisa mawasiliano na uhusiano wa umma, maofisa utumishi pamoja na maofisa mbalimbali katika mashirika hayo kisha tutahusisha wanahabari kutoka kampuni za habari, wakiwamo wanafunzi kutoka vyuo vikuu," alisema.

Alizitaja kozi ambazo zitatolewa kuwa ni pamoja na programu za mawasiliano ya kimkakati kwa taasisi na mashirika kama vile mawasiliano ya biashara, mawasiliano wakati wa mgogoro, usimamizi wa chapa, mawasiliano fanisi, mawasiliano binafsi, mawasiliano ya kitaasisi sambamba na kozi zingine zinazolenga kujenga ujuzi bora kwa wadau wa mawasiliano.

Katibu Mtendaji wa Chemba ya Madini Tanzania (TCM), Benjamin Mchwampaka, alisema ujio wa mkakati huo umekuja katika kipindi ambacho Taifa linahitaji kuwa na waandishi wabobevu katika maeneo mbalimbali ya kimkakati ikiwamo eneo la madini ili taarifa zinazotolewa ziwe na tija kwa wananchi.

Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni ya Mwananchi Communications Limited, Bakari Machumu, alisema ni muhimu kwa wanahabari wote kuendelea kujifunza ili kujijenga taaluma kwa maisha yao yote.

"Mambo mengi yanabadilika katika tasnia yetu, hivyo kuna haja ya kujifunza na kupanua uwezo wetu na kuwa na uelewa mpana kila wakati," Machumu alisema.




Mratibu wa Mafunzo wa Taasisi ya Uhusiano na Mawasiliano ya Umma Tanzania (IPRT), Evarist Ngalimuwili (katikati), akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam jana, wakati wa uzinduzi wa mpango wa kutoa mafunzo kuhusu mawasiliano ya kimkakati mahusus kwa watendaji wakuu, maofisa mawasiliano na maofisa mbalimbali katika mashirika unaoratibiwa na IPRT kwa kushirikiana na taasisi nyingine za elimu ya juu za ndani na nje ya nchi. Kulia ni Mkurugenzi Mtendaji wa Mwananchi Communications Ltd, Bakari Machumu na Katibu Mtendaji wa Chemba ya Madini Tanzania (TCM), Mhandisi Benjamin Mchwampaka. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## TAHILISO yatakiwa kutoa elimu ya sensa

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

JUMUIYA ya Wanafunzi Taasisi za Elimu ya Juu Tanzania (TAHILISO), imetakiwa kuelimisha wananchi umuhimu wa Sensa ya Watu na Makazi, iliopangwa kufanyika Agosti 23 mwaka hapa nchini.

Kamisaa wa Sensa nchini na Spika Mstaafu wa Bunge, Anne Makinda, alisema hayo jana wakati akifungua kongamano la wanafunzi wa vyuo vya elimu ya juu lililolenga kutoa elimu kwa wanafunzi kuhusu sensa ili nao wakaelimishe jamii kuhusu umuhimu wa watu kuhesabiwa.

"TAHILISO mmepewa elimu hii ili mkawe mabalozi wazuri katika maeneo yenu kuhusu umuhimu wa sensa hapa nchini na nyie mkaitoe elimu hiyo katika maeneo mnayotoka ili kuhamasisha jamii kujitokeza kwenye zoezi la sensa," alisema Makinda.

Kuhusu umuhimu wa Sensa ya Watu na Makazi, alisema inasaidia nchi kupanga maendeleo ya wananchi wake na taifa kwa ujumla kwa sababu kutakuwa na takwimu sahihi za idadi ya watu.

Alisema lakini bila kufanya hivyo, itawawia vigumu kufanya hivyo kutokana na kutokuwa na idadi sahihi ya watu na makazi yao.

Mkurugenzi wa Elimu ya Juu kutoka Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Dk. Kenneth Hosea, aliwataka wanafunzi hao kuwa mstari wa mbele kutangaza na kutoa elimu kwa jamii juu ya ushiriki wa sensa ya watu na makazi.

Akitolea mfano Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Dk. Hosea alisema wanahitaji kujua kuna wanafunzi wangapi, wanasoma wapi na ngazi ipi, wangapi wana ajira na wangapi hawana ajira, hivyo zoezi la sensa linawasaidia kupanga mipango ya maendeleo katika kila kundi.

"Sensa ina umuhimu mkubwa sana katika maendeleo ya nchi hivyo TAHILISO saidieni kuwa mabalozi wazuri wa kuelimisha jamii juu ya ushiriki wa sensa ya watu na makazi," alisema.

Dk. Hosea alisema takwimu hizo huwezi kuzipata kwa namna yoyote ile bali kwa kufanya sensa ambayo itatoa idadi ya kila mmoja mahali alipo ikiwamo makazi yake.

# 'Wazazi wasiopeleka watoto shule wabanwe'

**Na Alpius Mchucha,** NJOMBE

WANANCHI wilayani Ludewa mkoani Njombe, wameiomba serikali kuwabana wazazi wanaoshindwa kuwapa haki ya elimu watoto wao na badala yake kuwatumikisha kazi za nyumbani.

Wakizungumza katika Kijiji cha Lufumbu, Kata ya Mlangali katika maadhimisho ya wiki ya elimu, baadhi ya wananchi na wadau walisema suala la elimu kwa mtoto linapaswa kutiliwa mkazo zaidi ili mzazi awajibike kumsomesha kwa kuwa kuna faida siku za baadaye.

"Mtoto usipompeleka shuleni atakuwa mhudumu wa baa huko mijini na baadaye kukupa hasara wewe mzazi ikiwamo kujihusisha katika makundi ya uhalifu nashauri mtoto wa mwenzangu nimuone kama wa kwangu," alisema Asumpta Mahundi.

Kwa upande wake, mdau wa elimu mkoani Njombe kutoka shirika lisilo la kiserikali la SHIPO anayesimamia mradi wa MAMMIE, Nemes Temba, alisema umuhimu wa kuadhimisha juma la elimu wilayani Ludewa ambalo kama wadau wa elimu mkoani hapa ni kusimamia vyema mtoto kupata elimu.

Mkuu wa Wilaya ya Ludewa, Andrea Tsere, akizungumza katika juma hilo, alisema serikali ajenda yake kubwa ni kuihamasisha jamii ili kumwezesha mwanafunzi anapata mazingira rafiki ya kupata elimu na kuhakikisha wanapata chakula shuleni.

"Katika mambo ambayo tumeamua kuimalisha elimu wilayani Ludewa ni kuhakikisha watoto wetu wanakula chakula cha mchana wakiwa shuleni na chakula hicho kiwe bora," alisema Tsere.

Baadhi ya wanafunzi wa Shule ya Msingi Lufumbu ambao walishiriki kwenye maadhimino ya wiki ya elimu walisema wanawashukuru wadau wa elimu kwa jitihada zao kwa kutoa misaada mbalimbali.

"Tunawashukuru wadau SHIPO wametuletea madawati, vitabu, meza za walimu, makabati kwa vitu vyote walivyotuletea hapa shuleni kwetu tunaomba wadau waendelee kutusaidia," alisema mwanafunzi Jenifer Castory.

# Wakulima wapatiwa mikopo ya pembejeo

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

WAKULIMA wa mazao ya chakula na biashara wilayani Kahama mkoani Shinyanga, wametakiwa kuchangamkia fursa za mikopo ya kilimo (Kilimo Biashara) katika Taasisi za kifedha ili kumudu gharama za pembejeo na kuzalisha chakula zaidi.

Kwa sasa mbolea ya kupandia aina ya Dapu mfuko wa kilo 50 unauzwa kwa Sh. 68,000 awali ulikuwa Sh. 60,000 na mbolea ya kukuzia aina ya Urea mfuko wa kilo 50 unauzwa kwa Sh. 145,000, awali ulikuwa Sh. 120,000.

Hayo yalibainishwa jana na Mkuu wa Kitengo cha huduma kwa wateja kutoka Benki ya Equity, Betty Kwaoko, wakati wa uzinduzi wa benki hiyo tawi la Kahama.

Alisema, katika kukuza uchumi wa wakulima, watahakikisha wanatoa mikopo yenye riba nafuu kwa wakulima likiwemo suala la pembejeo.

Alisema, hivi karibuni walizindua mradi na taasisi mbalimbali kwa ajili ya mikopo ya wakulima ili kuunga mkono serikali kuhakikisha wanaipatia nguvu sekta ya kilimo na wameshaingia makubaliano na kampuni zinazozalisha pembejeo ikiwamo Agricom na Yara.

"Tunaamini mikopo yetu tuliyoweka kwa ajili ya wakulima itawainua na kukuza uchumi wao, hii itasaidia kutatua malalamiko ya bei za pembejeo kwa sababu tumeingia ubia na kampuni zinazozalisha pembejeo hususani Agricom na Yara," alisema Kwaoko.

Kadhalika, alisema lengo kuu la kuweka tawi hilo Kahama ni kuwapo kwa biashara zitokanazo na nchi jirani za Rwanda, DRC Kongo, Burundi, Uganda na Kenya.

Awali, Katibu Tawala wa Wilaya ya Kahama, Timoth Ndanya, aliwapongeza kwa mkakati huo ambao utawasaidia wakulima kupata pembejeo kwa bei ndogo na kuwataka kabla ya kuwapatia mikopo hiyo wawapatie elimu ya kulima kisasa.

Ndanya aliutaka uongozi wa benki hiyo kutowasumbua wakulima wanapochelewesha kulipa mikopo hiyo na badala yake wawapatie muda hadi pale watakapouza mazao yao.

Alisema, wafanyabiashara wengi wa Kahama wameshindwa kukua kiuchumi na kimtaji baada ya ukosefu wa mikopo ambayo ndiyo msingi wa kuwainua kibiashara na kuwataka wahakikishe mikopo itakayotolewa iwe rafiki na riba nafuu.

Akizungumza kwa niaba ya wateja wa benki hiyo Mkurugenzi wa Halmashauri ya Ushetu, Mwalimu Mwageni, aliiomba benki hiyo kuwekeza vijijini katika kilimo cha alizeti kwa kuwa kimesahaulika mjini humo ikilinganishwa na kilimo kingine.

# Sababu kupungua sangara Ziwa Victoria yawekwa wazi

**Na Romana Mallya,** DODOMA

WAZIRI wa Mifugo na Uvuvi, Mashimba Ndaki, amesema kupungua kwa uvuvi katika Ziwa Victoria hususani samaki aina ya sangara kunatokana na sababu mbalimbali, kubwa ikiwa ni uvuvi haramu.

Aliyasema hayo juzi wakati akijibu hoja mbalimbali za wabunge zilizotolewa baada ya wizara yake kuwasilisha makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka wa fedha 2022/23.

Waziri huyo alisema hali ya upatikanaji wa sangara ni mbaya ziwani huko na mkakati wao ni kudhibiti uvuvi haramu, akibainisha kuwa tangu mwaka uliopita wamekuwa wakishirikisha wadau wote wa uvuvi.

"Ni kweli tumefanya operesheni kubwa, kufanya operesheni peke yake tumegundua kwamba haitoshi, tukaona ni vizuri tushirikishe wadau wote kuanzia wavuvi wanaovua kwenye maziwa na bahari.

"Kushirikisha serikali za mitaa, halmashauri na mikoa zihusike moja kwa moja kwenye masuala haya ya kudhibiti uvuvi haramu kwa sababu serikali ni moja, huwezi kuwa na serikali inayotoka Dodoma kwenda kudhibiti uvuvi haramu Bunda au Rorya," alisema.

Waziri Ndaki alisema mkakati wao kwa sasa ni serikali nzima kuwa shirikishi na wadau nao wahusike ili wadhibiti hilo.

Alisema wanafahamu samaki ni rasilimali inayomsaidia kila Mtanzania na wakisaidia leo halafu kesho wasifanye hivyo, ni bahati mbaya.

Alisema wanaendelea kutoa elimu ya uvuvi endelevu kwa wavuvi na kufanya maboresho ya kanuni ili wadhibiti sawasawa suala hilo.

Kuhusu viwanda vilivyofungwa, alisema siyo lazima vifungwe kwa sababu sangara hawapo, bali vipo vilivyofungwa kwa matatizo ya uongozi na uendeshaji. "Siyo sawa kusema viwanda vimefungwa kwa sababu sangara walikuwa kidogo," Waziri Ndaki alitoa angalizo.

Awali, akichangia bajeti hiyo, Mbunge wa Viti Maalum, Mariam Ditopile, alisema hali ya upatikanaji wa samaki aina ya sangara katika Ziwa Victoria ni mbaya na hafahamu kama kwenye vipaumbele vya wizara hiyo wameliona hilo.

"Kwanini ninasema hali mbaya, sangara ni bidhaa katika soko la samaki la duniani, Ulaya ndiyo soko kubwa ambalo zaidi ya asilimia 70 ya mazao ya samaki yanayotoka Afrika yanakwenda huko.

"Mwaka 2014/15 Tanzania tulikuwa tunatoa tani zaidi ya 45,000 za minofu ya sangara na mazao yake lakini mwaka 2021 tumetoa tani 14,000 tu , lakini viwanda vyetu vimekuwapo mwaka 2014/15 tulikuwa tunaajiri zaidi vijana 12,000 kwenye sekta hii. Akiendelea kujibu hoja mbalimbali, Waziri Ndaki pia alizungumzia leseni za uvuvi wa bahari kuu, akisema kuwa kwa mujibu wa kanuni ya usimamizi na uendelezaji wa uvuvi wa bahari kuu ya mwaka 2021, bei za leseni za uvuvi eneo hilo kwa meli za Kitanzania zilipunguzwa kati ya asilimia 70 hadi asilimia 86 kulinganishwa na za leseni kwa meli za kigeni.

Waziri Ndaki alisema wana mpango wa kutoa boti 320 ambazo zitakuwa na upekee, ndani yake zikikuwa na vifaa mbalimbali ikiwamo GPS, vifaa vya ubaridi, 'fishing finder' zitakuwa na uwezo wa kubeba tani 1.5.



Makamu wa Rais wa AngloGold Ashanti Geita Gold Mining Ltd anayeshughulikia miradi endelevu kwa nchi za Tanzania na Ghana, Simon Shayo (katikati), akikabidhi kadi ya gari kwa Mkuu wa Wilaya ya Ilemela, Hassan Masala (wapili kushoto) na Kaimu Mkuu Mkurugenzi Mkuu wa Veta Kanda ya Ziwa, Charles Kaugele, wakati wa hafla ya kukabidhi msaada wa magari manne yaliyotoewa na GGML kwa Chuo cha VETA tawi la Mwanza. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# GGML yatoa msaada wa magari kwa VETA

**Na Mwandishi Wetu**

KAMPUNI ya uchimbaji madini ya Geita Gold (GGML) imetoa msaada wa magari manne aina ya Toyota Land Cruiser kwa Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi (VETA) Tawi la Mwanza.

Kutolewa kwa magari hayo ni mwendelezo wa msaada wa kampuni ya GGML kwa taasisi mbalimbali nchini katika kuzisaidia kutekeleza majukumu yake ya kila siku.

Akizungumza katika hafla fupi ya makabidhiano ya magari hayo juzi, Makamu wa Rais wa AngloGold Ashanti Geita Gold Mining Limited anayeshughulikia miradi endelevu kwa nchi za Tanzania na Ghana, Simon Shayo, alisema msaada huo umetolewa muda mwafaka na unaendana na malengo endelevu yaliyowekwa na Umoja wa Mataifa (UN).

"Tumeunga mkono juhudi za VETA kwa sababu kwa kiasi kikubwa wanafunzi wanaotoka VETA wanakuwa na ujuzi ambao unamfanya mtu akitoka akafanye kile kitu ambacho amejifunza.

"Kwa upande wa mafunzo ya udereva na ufundi wa magari tunadhani kwamba janga kubwa lililopo la ajali ni ujuzi mdogo wa watu wanaotumia vyombo vya moto yakiwamo magari, kwa hiyo mtu akipitia mafunzo kama haya ya VETA, akitoka hapo atakuwa dereva bora zaidi," amesema na kuongeza:

"Huu ni mwendelezo wa ubia wetu na VETA wa muda mrefu ambapo tumekuwa tukifadhili mradi wa kufunza wanagenzi kwa ajili ya sekta ya madini, tumefadhili karibu watu 130 kutoka kwenye jamii inayotuzunguka na wameajiriwa kwenye migodi kama mafundi wakubwa ikiwa ni mwendelezo wa kuongeza ajira kwa Watanzania," alisema.

Kiongozi huyo alisema GGML ina wajibu wa kuinufaisha jamii kutokana na shughuli zake za uchimbaji dhahabu. Mwanza ni majirani zetu na wakati tunaanza uchimbaji mwaka 2000, Geita ilikuwa Mkoa wa Mwanza.

"Baada ya kuona changamoto ya usafiri kwa Mamlaka ya VETA jijini Mwanza, tumeamua kutoa msaada wa magari haya ili kuboresha mazingira ya utoleaji wa elimu kwa vijana wetu wanaosomea ufundi lakini pia kuendana na lengo la nne la Malengo Endelevu ya Umoja wa Mataifa linalosisitiza ubora wa elimu," alisema Shayo.

Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa VETA Kanda ya Ziwa, Charles Kaugele, aliipongeza GGML kwa msaada huo akisema utasaidia pia kutoa mafunzo kwa vitendo wanafunzi wanaosomea udereva chuoni huko.

Tangu mwaka 2006 GGML imekuwa ikishirikiana vizuri na VETA kwa kusomesha vijana 130 katika mafunzo jumuishi ya ufundi katika madini.

Idadi kubwa ya vijana hao wameajiriwa na GGML na wanatoka katika mitaa ya Geita ikiwamo Uwanja wa Kambarage, Compound, Bugulula, Ujamaa, Mwatulole, Mission na Nyerere Road.

GGML imekuwa ikiwekeza kwenye jamii tangu kuanzishwa kwake mwaka 2000 ambapo vipaumbele vikuu vimekuwa ni miradi ya elimu, afya, maji, barabara, miradi ya kukuza kipato na miradi mingine ya kijamii ili kuhakikisha jamii mwenyeji inapata maisha bora.

Mapema mwaka huu, GGML iliibuka mshindi wa jumla katika kampuni zinazofanya vizuri kwenye sekta ya madini nchini kwa mwaka wa fedha 2020/21 baada ya kunyakua tuzo katika vipengele vya uwajibikaji wa kampuni kwa jamii, mazingira, usalama, mlipaji bora wa mapato (kodi) na uendelezaji wazawa.

# Serikali: Hakuna haja kuifumua Sheria ya Utakatishaji wa Fedha

WIZARA ya Fedha na Mipango imesema hakuna sababu ya kurekebisha Sheria ya Kudhibiti Utakatishaji wa Fedha Haramu, Ufadhili wa Ugaidi na Ufadhili wa Silaha za Maangamizi, Sura ya 423.

Naibu Waziri wa Fedha na Mipango, Hamad Hassan Chande, aliliambia hayo Bunge jana alipojibu swali la Mbunge wa Njombe Mjini (CCM), Deodatus Mwanyika.

Mbunge huyo alihoji ni lini serikali itarekebisha sheria hiyo ambayo inazuia dhamana kwa watuhumiwa hata kwa makosa ya kawaida.

Akijibu swali hilo, naibu waziri huyo alisema hakuna sababu ya kurekebisha kwa kuwa haizuii dhamana kwa watuhumiwa wa makosa ya kawaida.

"Kifungu cha 12 cha Sheria ya Kudhibiti Utakatishaji wa Fedha Haramu, Ufadhili wa Ugaidi na Ufadhili wa Silaha za Maangamizi, Sura ya 423 kinabainisha makosa ya utakatishaji wa fedha haramu pekee," alisema.

Naibu waziri huyo alisema sheria hiyo haihusishi makosa mengine, hususan kuzuia au kutozuia dhamana kwa watuhumiwa wa makosa ya kawaida.

Alisema utaratibu wa dhamana kwa makosa mbalimbali, ikiwamo utakatishaji wa fedha haramu unasimamiwa na Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai, Sura ya 20.




Habari zote na Augusta Njoji



Mbunge wa Viti Maalumu, Zainab Katimba, akisoma tamko la Bunge jijini Dodoma jana, la kumpongeza Rais Samia Suluhu Hassan kuwa miongoni mwa viongozi wenye ushawishi mkubwa duniani na kupewa tuzo ya mafanikio ya ujenzi wa miundombinu huko Accra, nchini Ghana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Viwanda vyang'ara sekta ndogo ya nguo

SERIKALI imesema sekta ndogo ya nguo na mavazi nchini ina viwanda tisa vinavyofanya kazi hivi kwa sasa.

Naibu Waziri wa Viwanda, Biashara na Uwekezaji, Exaud Kigahe, alitoa kauli hiyo jana bungeni jijini hapo alipojibu swali la Mbunge wa Viti Maalum, Esther Matiko.

Katika swali lake, mbunge huyo alihoji mkakati wa serikali kutatua kero zinazokabili viwanda vya kutengeneza nguo nchini kwa kuwa kwa sasa ni viwanda vitatu tu vinavyofanya kazi kati ya 33.

Akijibu swali hilo, Naibu Waziri Kigahe alisema serikali imeendelea kutatua kero zinazokabili viwanda vya nguo, ikiwa ni pamoja na kuboresha mazingira ya ufanyaji biashara nchini.

Pia alisema mkakati huo unakwenda sambamba na kudhibiti bidhaa zisizo na ubora na bidhaa bandia kutoka nje ya nchi, kuongeza ushuru wa forodha kwa kanga na vitenge vinavyotoka nje ya nchi, kuhamasisha taasisi za umma na Watanzania kununua bidhaa za nguo zinazotengenezwa na viwanda vya ndani na kuweka miundombinu wezeshi.

Katika swali la nyongeza, mbunge huyo alisema kumekuwapo na uingizaji wa bidhaa kwa njia za magendo kutoka nchi za nje kunasababisha ukwepaji wa kodi na kusababisha viwanda nchini kutokuwa shindani.

"Serikali ina mkakati gani kuhakikisha inatokomeza biashara hiyo ya magendo ili viwanda vizalishe kwa tija, serikali ina mkakati gani kuhakikisha inatoa dhamana za mikopo kwa viwanda tulivyokuwa navyo awali kama Urafiki na Mwatex?" Alihoji.

Akijibu swali hilo, Naibu Waziri Kigahe alisema sekta hiyo ina vikwazo mbalimbali ikiwamo kuingizwa kwa bidhaa hizo kwa magendo na serikali ilishaanza kuchukua hatua mbalimbali ikiwamo kudhibiti mipaka na bandari bubu.

"Tumeanza kuchukua hatua ya kudhibiti na kuongeza watumishi kwenye taasisi zetu ili kuziba mianya inayoingiza bidhaa hizo," alisema.

Kuhusu viwanda ambavyo havifanyi kazi, alisema serikali imekuwa ikivisaidia kwa njia mbalimbali na zimeongezeka kutoka vitatu na kuwa tisa.

## Waajiriwa wapya 7,600 afya kupunguza uhaba

SERIKALI imesema watumishi wa kada ya afya 7,612 watakaoajiriwa hivi karibuni watagawanywa kwa kuzingatia mahitaji ya maeneo husika.

Naibu Waziri Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), David Silinde, aliyasema hayo jana alipojibu swali la nyongeza la Mbunge wa Kalambo (CCM), Josephat Kandege.

Katika swali lake, Mbunge Kandege alisema kuna upungufu mkubwa wa watumishi kwenye Wilaya ya Kalambo kutokana na hivi karibuni kuhama watumishi 35 ilhali waliohamishiwa kwenye wilaya hiyo ni watumishi watatu.

"Je, serikali katika mgawo huu itakwenda kuzingatia usawa badala ya ubora?" Alihoji mbunge huyo.

Akijibu swali hilo, Silinde alisema baada ya kukamilisha mchakato wa ajira, utafanyika mgawanyo kwenye halmashauri zote nchini na zitazingatia mahitaji ya maeneo husika.

"Hatutakuwa na ile namba ya kugawa kwenye halmashauri zote kwa usawa, tutagawa kulingana na mahitaji, maeneo kama Kalambo yenye uhitaji mkubwa tutayapa kulingana na mahitaji," alisema.

Katika swali la msingi, mbunge huyo alihoji mpango wa serikali kupeleka watumishi wa kada ya afya wilayani Kalambo kwa kuzingatia upungufu uliopo.

Akijibu swali hilo, Naibu Waziri Silinde alisema serikali katika mwaka wa fedha 2021/22, imepanga kuajiri watumishi wa kada ya afya 7,612 watakaopangwa katika halmashauri zote nchini, ikiwamo Halmashauri ya Wilaya ya Kalambo.

## 'Mradi wa umwagiliaji sasa utengewe fedha'

MBUNGE wa Nanyamba (CCM), Abdallah Chikota, ameitaka serikali kutenga fedha kwa ajili ya utekelezaji wa mradi wa umwagiliaji wa Kijiji cha Arusha Chini.

Akiuliza swali bungeni jijini hapa jana, Chikota alisema kuna eneo kubwa linazunguka Kijiji cha Ngonja, Arusha Chini na Arusha Juu na kuhoji kama serikali ipo tayari kujumuisha eneo hilo wakati wa kufanya usanifu wa skimu hiyo ya umwagiliaji.

Akijibu maswali hayo bungeni jana, Naibu Waziri wa Kilimo, Anthony Mavunde, alisema mradi wa umwagiliaji katika kijiji cha Arusha Chini una hekta 120 zinazofaa kwa kilimo cha umwagiliaji.

Alisema kuwa kati yake, hekta 48.5 zinamwagiliwa kwa kutumia mifereji ya asili ambayo chanzo chake cha maji ni chemichem na mvua za msimu.

"Katika mwaka wa fedha 2022/23, serikali imetenga fedha kwa ajili ya kufanya upembuzi yakinifu na usanifu wa skimu hii," alisema.

Mavunde alisema serikali ipo tayari kutoa maelekezo kwa timu itakayofanya usanifu kupitia eneo kubwa la skimu hiyo kadri iwezekanavyo.

"Maelekezo ya Ilani ya Uchaguzi ya CCM ni kwamba ifikapo mwaka 2025, eneo la umwagiliaji liwe hekta milioni 1.2, kwa hiyo wataalamu wataangalia eneo ambalo halijajumuishwa ili lijumuishwe," alisema.

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
HOTUBA YA WAZIRI WA ARDHI,
NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI

# HOTUBA YA WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI, MHESHIMIWA DKT. ANGELINE S.L. MABULA (MB.), AKIWASILISHA BUNGENI MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA KWA MWAKA WA FEDHA 2022/23



*MHE. DKT. ANGELINE S.L. MABULA (MB.)*
*WAZIRI*



*MHE. RIDHIWANI JAKAYA KIKWETE (MB.)*
*NAIBU WAZIRI*



*DKT. ALLAN H. KIJAZI*
*KATIBU MKUU*



*BW. NICHOLAS M. MKAPA*
*NAIBU KATIBU MKUU*

TANZANIA SENSA 23 Agosti 2022 Jiandae Kuhesabiwa

*Dodoma*

*26 Mei, 2022*

# HOTUBA YA WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI, MHESHIMIWA DKT. ANGELINE S.L. MABULA (MB.), AKIWASILISHA BUNGENI MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA KWA MWAKA WA FEDHA 2022/23

**UTANGULIZI**

1. **Mheshimiwa Spika**, kufuatia taarifa iliyowasilishwa leo ndani ya Bunge lako Tukufu na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii iliyochambua Bajeti ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi (Fungu 48) na Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi (Fungu 03), naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu sasa lipokee na kujadili taarifa za utekelezaji wa Bajeti ya Wizara (Fungu 48) na Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi (Fungu 03) kwa mwaka 2021/22. Aidha, naomba Bunge lako Tukufu lijadili na kupitisha makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara (Fungu 48) na Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi (Fungu 03) kwa mwaka 2022/23.

2. **Mheshimiwa Spika**, Baada ya utangulizi huo, napenda nitumiea fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia afya njema na kutuwezesha kushiriki Mkutano wa Saba (7) wa Bunge la 12 la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Aidha, kwa heshima na taadhima naomba kutumia fursa hii kipekee kumshukuru sana Mhe. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuniamini na kuniteua kuwa Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi. Ninaahidi kuwa nitatekeleza majukumu yangu kwa juhudi, maarifa, uaminifu na weledi mkubwa kwa maendeleo ya Taifa letu.

3. **Mheshimiwa Spika,** kwa namna ya pekee, nitumie fursa hii kuwapongeza Mhe. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Philip Isdor Mpango, Makamu wa Rais; Mhe. Dkt. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi na Mhe. Kassim Majaliwa Majaliwa, Waziri Mkuu na Mbunge wa Ruangwa kwa uongozi wao mahiri. Aidha, nawashukuru kwa miongozo, maelekezo na ushirikiano wao unaoniwezesha kutekeleza majukumu ya kuongoza sekta hii vyema.

4. **Mheshimiwa Spika,** nakupongeza wewe binafsi kwa kuchaguliwa kuwa Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Mhe. Mussa Azzan Zungu (Mb.), kwa kuchaguliwa kuwa Naibu Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Ushindi mkubwa wa kishindo mlioupata umetokana na uzoefu mkubwa mlionao katika kusimamia shughuli za Bunge hivyo kukidhi matarajio ya wabunge waliowachagua hongereni sana. Vilevile, nachukua fursa hii kuwapongeza Mhe. Najma Murtaza Giga (Mb.), na Mhe. David Mwakiposa Kihenzile (Mb.), kwa kuchaguliwa na kuendelea kuwa Wenyeviti wa Bunge. Tunawaombea Mwenyezi Mungu awajalie afya njema na hekima katika utekelezaji wa majukumu yenu.

5. **Mheshimiwa Spika**, natoa pole kwako, Naibu Spika na Waheshimiwa Wabunge wa Bunge lako Tukufu kwa kuondokewa na wapendwa wetu Mhe. Elias Kwandikwa, aliyekuwa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa na Mbunge wa Jimbo la Ushetu; Mhe.William Tate Olenasha aliyekuwa Naibu Waziri Ofisi ya Waziri Mkuu (Uwekezaji) na Mbunge wa Ngorongoro; Mhe. Khatibu Said Haji aliyekuwa Mbunge wa Konde Zanzibar na Mhe. Irene Alex Ndyamkama, aliyekuwa Mbunge wa Viti Maalum. Aidha, napenda kutumia fursa hii kutoa pole kwa familia, ndugu, jamaa na marafiki wa marehemu kwa kuondokewa na wapendwa wao. Mwenyezi Mungu azilaze roho za marehemu mahali pema peponi, Amina.

6. **Mheshimiwa Spika,** ninampongeza Mhe. Ally Juma Makoa (Mb.), kwa kuchaguliwa kuwa Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii na Mhe. Shabani Omary Shekilindi (Mb.), kuwa Makamu Mwenyekiti, wajumbe wote wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii, tunaahidi kuwapa ushirikiano katika kutekeleza majukumu yenu ya usimamizi wa Sekta ya Ardhi kwa ajili ya maendeleo ya nchi yetu.

7. **Mheshimiwa Spika,** nampongeza pia Mhe. Ridhiwani Jakaya Kikwete (Mb.), kwa kuteuliwa kuwa Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Dkt. Allan H. Kijazi kuwa Katibu Mkuu na Bw. Nicholas M. Mkapa kwa kuteuliwa na kuendelea kuwa Naibu Katibu Mkuu. Vilevile, nawapongeza Mawaziri, Naibu Mawaziri na Viongozi wengine walioteuliwa kushika nyadhifa mbalimbali katika Serikali ya Awamu ya Sita.

   Aidha, nitumie fursa hii kuwapongeza Mhe. Emmanuel Lekishon Shangai (Mb.), kwa kuchaguliwa kuwa Mbunge wa Ngorongoro, Mhe. Emmanuel Peter Chelehani kuwa Mbunge wa Ushetu, Mohammed Said Issa kuwa Mbunge wa Konde na Mhe. Shamsi Vuai Nahodha (Mb.), kwa kuteuliwa kuwa Mbunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Nawatakia kila la kheri katika utekelezaji wa majukumu yenu na ninaahidi kuwapa ushirikiano hususan kwa masuala yanayohusu Sekta ya Ardhi.

8. **Mheshimiwa Spika,** kipekee nampongeza Mhe. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa dhamira na juhudi zake za kuendeleza Sekta ya Ardhi nchini. Katika kipindi cha mwaka mmoja cha uongozi wake ameiwezesha Sekta ya Ardhi kupata shilingi bilioni 345 kutoka Benki ya Dunia na shilingi bilioni 68.4 fedha za ndani kwa ajili ya kupanga, kupima na kumilikisha ardhi; kuimarisha utunzaji wa taarifa za ardhi; kuandaa taarifa za ramani kidigitali kwa ajili ya Mfumo wa Anwani za Makazi; na kuboresha miundombinu ya upimaji na ramani.

9. **Mheshimiwa Spika,** aidha nampongeza kwa dhati Mhe. Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb.), Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa Hotuba yake ya Bajeti ambayo imetoa utekelezaji wa malengo ya Serikali katika mwaka 2021/22 na mwelekeo wa shughuli za Serikali kwa mwaka 2022/23. Wizara inaahidi kutekeleza maelekezo yote yanayoihusu Sekta ya Ardhi.

10. **Mheshimiwa Spika**, natoa shukrani zangu za dhati kwa Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii kwa ushirikiano na ushauri ambao umetuwezesha kuboresha utekelezaji wa majukumu ya Wizara. Aidha, uchambuzi makini na ushauri walitoa wakati wa kupitia Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Wizara kwa mwaka 2021/22 pamoja na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara (Fungu 48) na Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi (Fungu 03) kwa mwaka 2022/23. Napenda kulihakikishia Bunge lako Tukufu kwamba Wizara yangu, itaendelea kuzingatia maoni, ushauri na maelekezo ya Kamati ili kuboresha utendaji na hivyo kuongeza ufanisi na tija katika utoaji wa huduma za Sekta ya Ardhi.

11. **Mheshimiwa Spika,** Aidha nitumie fursa hii kwa dhati kuwashukuru wananchi wa Jimbo la Ilemela kwa kuendelea kuniamini kuwawakilisha. Naishukuru familia yangu, viongozi wa dini kwa sala na dua zao ambazo zinanipa nguvu ya kutenda kazi zangu nikiwa na hofu ya Mungu.

    Pamoja na shukrani hizo, kipekee pia namshukuru sana mtangulizi wangu Mhe. William V. Lukuvi kwa kuwa Mwalimu mwema, amechangia kwa kiasi kikubwa katika kazi yangu.

12. **Mheshimiwa Spika**, baada ya maelezo ya utangulizi, naomba sasa nieleze kwa ufupi utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Wizara kwa mwaka 2021/22, na makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka 2022/23.

**1. UTEKELEZAJI WA BAJETI YA WIZARA KWA MWAKA 2021/22 NA MALENGO YA MWAKA 2022/23.**
**(Aya 13 – 16)**

13. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2021/22, Wizara iliidhinishiwa jumla ya Shilingi bilioni 97.5. Kati ya fedha hizo, shilingi bilioni 33.9 kwa ajili ya Matumizi Mengineyo (OC); shilingi bilioni 34.0 kwa ajili ya Mishahara ya Wizara (PE); na shilingi bilioni 29.5 kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo. Katika fedha za Miradi ya Maendeleo shilingi bilioni 18.3 ni fedha za ndani na shilingi bilioni 11.3 ni fedha za nje. Aidha, katika mwaka 2021/22, Wizara iliongezewa bajeti ya shilingi bilioni 18.5 ambapo shilingi bilioni 1.0 ilikuwa kwa ajili ya kulipa madeni ya watumishi na watoa huduma na shilingi bilioni 17.5 ni kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo. Ongezeko hilo limefanya bajeti ya Wizara kufikia shilingi billion 116.1

14. **Mheshimiwa Spika**, hadi kufikia tarehe 15 Mei, 2022, Wizara ilipokea jumla ya shilingi bilioni 71.6 kati ya bajeti ya shilingi bilioni 116.1 sawa na asilimia 62 ya bajeti iliyoidhinishwa. Kati ya fedha zilizopokelewa, shilingi 27.6 ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo (OC) ya Wizara na Taasisi sawa na asilimia 77 ya bajeti; shilingi bilioni 30.0 ni Mishahara ya Wizara na Taasisi sawa na asilimia 91 ya bajeti; na shilingi bilioni 14.0 ni fedha za ndani sawa na asilimia 30 ya bajeti ya yote ya Miradi ya Maendeleo ambayo pia ni asilimia 39 ya fedha za ndani.

15. **Mheshimiwa Spika,** vilevile, Wizara ilipokea shilingi bilioni 54.8 fedha za ndani kupitia akaunti ya Amana ikiwa ni nyongeza ya bajeti (Fungu 48). Kati ya fedha hizo shilingi bilioni 50 ni kwa ajili ya kuwezesha Kupanga, Kupima na Kumilikisha Ardhi na shilingi bilioni 4.8 ni kwa ajili ujenzi wa Ofisi ya Makao Makuu ya Wizara katika Mji wa Serikali Mtumba.

16. **Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2021/22, Wizara ilipanga kukusanya shilingi bilioni 221 kutoka kwenye vyanzo mbalimbali vya mapato yanayotokana na Sekta ya Ardhi. Hadi kufikia tarehe 15 Mei, 2022, Wizara imekusanya shilingi bilioni 115 sawa na asilimia 52 ya lengo. Miongoni mwa sababu za kutofikia malengo ni uwepo wa Taasisi na Mashirika ya umma yapatayo 114 kuwa na malimbikizo ya kodi ya shilingi bilioni 78, (35%) wananchi wenye vipande vya ardhi waliopewa ankara kutolipa gharama za umilikishaji na wadaiwa kodi ya pango la ardhi kutolipa kwa wakati. Wizara inaendelea kutoa elimu kwa umma kuhusu umuhimu wa kulipa kodi ya pango la ardhi kwa wakati; kuweka makubaliano na Taasisi za Serikali ya kulipa kwa awamu madeni husika, kuchukua hatua za kisheria dhidi ya wadaiwa sugu na kuweka mifumo ya rafiki ya kielekitroniki ya ukadiriaji na ulipaji ili kuongeza ufanisi. Utekelezaji wa mikakati hii unalenga kuongeza kasi ya makusanyo ili kufikia lengo.

**MWELEKEO WA SEKTA YA ARDHI (Aya 18 – 41)**

17. **Mheshimiwa Spika**, kwa mwaka 2022/23, Wizara imeweka lengo la kukusanya shilingi bilioni 250.1. Lengo hili litafikiwa kwa kutekeleza mikakati mbalimbali ikiwemo:
    - kuhuisha na kutunza kumbukumbu za wamiliki wa ardhi katika mfumo wa kielektroniki ili kurahisisha utumaji wa ankara;
    - kuimarisha miundombinu ya TEHAMA;
    - kuziwezesha Mamlaka za Serikali za Mitaa kukusanya maduhuli;
    - kutoa elimu ya mlipa kodi;
    - kuandaa na kuhuisha viwango vya ukadiriaji kodi; na

- kuhamasisha Halmashauri na Sekta binafsi kupima maeneo mapya ili kuongeza wigo wa makusanyo.

Vilevile, Wizara imeboresha utoaji wa ankara za malipo ya kodi ya pango la ardhi kwa wateja ambapo mteja anaweza kukadiria kodi ya ardhi kupitia tovuti www.landrent.lands.go.tz na kulipa kwa awamu. Nichukue fursa hii kuwakumbusha wamiliki wa ardhi kulipa kodi ya pango la ardhi ili kuepuka kuchukuliwa hatua za kisheria.

18. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2021/22, Wizara iliahidi kuendelea kuimarisha Ofisi za Ardhi za Mikoa. Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa hadi tarehe 15 Mei, 2022, Ofisi za Ardhi za Mikoa ambapo mikoa yote 26 imeimarishwa na ina wataalam wa kada za Mipangomiji, Upimaji na Ramani, Uthamini, Utawala wa Ardhi na Usajili.

Aidha wizara imezipatia ofisi zote za mikoa, vitendea kazi muhimu, kutoa mafunzo kwa watumishi, rasilimali fedha pamoja na kuweka mifumo ya TEHAMA.

19. **Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa fedha 2022/23, Wizara kupitia Mradi wa Uboreshaji wa Milki za Ardhi (LTIP), imepanga kujenga Ofisi za Ardhi katika Mikoa 25 zitakazokidhi utoaji huduma kwa Mfumo Unganishi wa Kuhifadhi Taarifa za Ardhi (ILMIS). Aidha, huduma zote za sekta zitakuwa zikitolewa katika majengo hayo zikiwemo huduma za Mabaraza ya Ardhi na Nyumba ya Wilaya.

20. **Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2022/23, Wizara imepanga kutoa vyeti vya ardhi ya kijiji 100, Hati za Hakimiliki za Kimila 520,000, Hatimiliki 500,000 na Hati za Sehemu ya Jengo 1,000. Vilevile, Wizara imepanga kusajili miamala ya Hatimiliki na nyaraka za kisheria 100,000. Ili kuhakikisha kuwa malengo haya yanafikiwa, Wizara itatekeleza Mradi wa Uboreshaji Miliki za Ardhi (LTIP); itaongeza kasi ya utekelezaji wa Programu ya Kupanga, Kupima na Kumilikisha Ardhi; kuboresha miundombinu ya upimaji; na kuongeza kasi ya uandaaji wa matumizi ya ardhi; kushirikisha wadau mbalimbali na sekta binafsi mathalan UN-Women, LTA - NGO, Ofisi ya Rais kupitia MKURABITA na kuzihimiza Halmashauri kuendelea kutenga fedha kwa ajili ya Sekta ya Ardhi.

Natoa rai kwa Waheshimiwa Wabunge ambao ni wajumbe wa Baraza la Madiwani kuhakikisha Halmashauri zinatenga fedha katika bajeti zao kwa ajili ya kutekeleza shughuli za Sekta ya Ardhi kwa mujibu wa matakwa ya sheria Na. 8 ya mwaka 2007 ya Mipango Miji kama Mamlaka za Upangaji

**Utatuzi wa Migogoro ya Ardhi Kiutawala**

21. **Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2021/22, Wizara ilipanga kutatua migogoro ya ardhi 1,000 kiutawala. Hadi kufikia tarehe 15 Mei, 2022 migogoro 1,635 kati ya migogoro 1,898 iliyopokelewa imetatuliwa na Wizara inaendelea na utaratibu wa kutatua na kudhibiti migogoro ya ardhi kwa kutumia njia mbalimbali na kuhusisha Wizara za kisekta na wadau wa Sekta ya Ardhi. Njia hizo ni pamoja na:
- kutoa elimu kwa umma kwa kushirikiana na wadau mbalimbali,
- kuongeza kasi ya kupanga, kupima na kumilikisha ardhi,
- kubadilisha nyaraka za upangaji, upimaji na umilikishaji ardhi kutoka analogia kuwa za kidigitali kama mpango wa muda mrefu katika kupunguza migogoro,
- madawati ya kushughulikia malalamiko katika Ofisi za Ardhi za Mikoa.
- kuwepo Rejista ya migogoro migogoro ya ardhi kwa kila Ofisi za Ardhi za Mikoa na Halmashauri. Rejista hizo zinayoonesha aina na hali ya mgogoro pamoja na namna ulivyoshughulikiwa.

**Migogoro ya Matumizi ya Ardhi katika Vijiji 975**

22. **Mheshimiwa Spika,** Namshukuru Mhe. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuelekeza na kuridhia vijiji 920 kati ya vijiji 975 kurasimishwa.

Kamati ya mawaziri wa kisekta inashiriki katika zoezi la kuelekeza uongozi wa mikoa kutekeleza zoezi la maagizo ya BLM kwa njia shirikishi na kuendelea kufanya tathmini katika vijiji 55 vilivyobaki ili kumaliza migogoro. Viongozi mbalimbali ngazi ya mikoa, wilaya na taasisi wanashirikishwa pamoja na Viongozi wa Chama Tawala ngazi ya Mkoa na Wilaya. Hadi kufikia tarehe 15 Mei, 2022, Kamati ya Mawaziri wa Kisekta imefanya vikao katika mikoa 13 ya Pwani, Morogoro, Tanga, Mara, Manyara, Mbeya, Geita, Arusha, Tabora, Dodoma, Singida, Kilimanjaro na Kigoma. Aidha, Kamati ya Mawaziri itaendelea kutekeleza uamuzi wa Serikali katika mikoa iliyobaki. Nawasihi wananchi wote kuwa na imani na Serikali yao katika utekelezaji wa zoezi hili na natoa tahadhali kwa wale ambao wamekuwa wakieneza taarifa zisizo sahihi na kusababisha taharuki kwa wananchi kuacha kufanya hivyo mara moja.

**Uthamini na Fidia**

23. **Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2021/22, Wizara iliahidi kuendelea kushughulikia malalamiko 100 ya uthamini wa fidia, kufanya uhakiki wa uthamini wa fidia katika maeneo 20, kuendelea kufanya utafiti na kuandaa viwango vya thamani ya ardhi katika mikoa yote 26 nchini. Hadi tarehe 15 Mei, 2022, jumla ya malalamiko 51 ya uthamini wa fidia yalipokelewa na kushughulikiwa. Pia, uthamini wa maeneo 15 ya miradi mbalimbali umefanyiwa uhakiki ili kutatua migogoro ya fidia. Aidha, Wizara imekuwa ikipokea malalamiko mengi kutoka kwa wananchi yanayohusiana na kucheleweshewa, kulipwa pungufu au kutolipwa fidia.

Nasisitiza taasisi za Serikali na kampuni binafsi kulipa fidia kwa wakati ili kuepusha ulipaji wa riba na malalamiko yanayotokana na ucheleweshaji wa ulipaji fidia. Kamwe Serikali haitaruhusu utwaaji wa ardhi bila kulipa fidia.

**Mabaraza ya Ardhi na Nyumba ya Wilaya**

24. **Mheshimiwa Spika,** Wizara katika mwaka 2021/22 iliahidi kuongeza idadi ya Mabaraza yanayotoa huduma ambapo hadi kufikia tarehe 15 Mei, 2022, Mabaraza mapya 20 yameanza kutoa huduma na hivyo kuwa na jumla ya Mabaraza 80 yanayotoa huduma kati ya Mabaraza 139 yaliyoanzishwa. Katika mwaka 2022/23, Wizara inatarajia kuwezesha Mabaraza mapya 59 kuanza kutoa huduma na hivyo kuwa na Mabaraza yanayotoa huduma katika Wilaya zote nchini.

25. **Mheshimiwa Spika,** Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa ifikapo Juni, 2022 Wizara itakamilisha ujenzi wa Mfumo wa Kusimamia Mashauri katika Mabaraza ya Ardhi na Nyumba ya Wilaya (Intergrated Land Cases Management System)., ambao utaanza kutumika katika mwaka 2022/23. Mfumo huo utarahisisha utendaji kazi wa Mabaraza ya Ardhi na Nyumba ya Wilaya katika kutunza kumbukumbu za mashauri, kufungua mashauri mapya, kufuatilia utendaji kazi wa watumishi wa Mabaraza na upatikanaji wa nakala za hukumu kwa njia ya mtandao.

26. **Mheshimiwa Spika**, kutokana na changamoto ya wazee wa baraza wanapomaliza muda wao, huchukua muda mrefu kupatikana wengine, nitoe rai kwenye mamlaka za mikoa na wilaya kuanza mchakato wa kupata wazee wa mabaraza wapya miezi sita (6) kabla ya waliopo kumaliza muda wao ili kuepuka usumbufu kwa wateja kwa kuahirishwa mashauri yao mara kwa mara kwa kukosa wazee kwa kisingizo cha muda wao wa kuhudumu kuisha.

27. **Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2021/22, Wizara iliahidi kufanya marekebisho ya Sheria ya Mahakama za Utatuzi wa Migogoro ya Ardhi Na. 2 ya mwaka 2002 yanayolenga kubadili mfumo wa ajira za wenyeviti wa Mabaraza ya Ardhi na kuyafanya Mabaraza ya Kata kufanya usuluhishi wa migogoro ya ardhi badala ya kutoa hukumu.

Napenda kuliarifu Bunge lako tukufu kuwa Serikali imefanya marekebisho katika sheria hiyo kwa kurekebisha mfumo wa ajira za Wenyeviti wa Mabaraza kutoka ajira ya mkataba wa miaka mitatu (3) na kuwa ajira za kudumu. Mfumo wa ajira za kudumu kwa Wenyeviti wa Mabaraza utaiwezesha Wizara kupata Wenyeviti kutoka miongoni mwa wanasheria wenye sifa waliopo katika Utumishi wa Umma na kuwezesha usimamizi wa maadili ya Wenyeviti wa Mabaraza kwa kutumia Sheria na Kanuni za Utumishi wa Umma. Aidha, kupitia marekebisho haya Mabaraza ya Kata yameondolewa mamlaka ya kufanya maamuzi na yamebaki na mamlaka ya usuluhishi pekee katika mashauri yanayohusu migogoro ya ardhi.

**Hatua inayofuata ni kuandaa kanuni zinazobainisha utaratibu wa usuluhishi katika Mabaraza ya Kata.**

**TEHAMA (Aya 42 -49)**

28. **Mheshimiwa Spika,** TEHAMA ni nyenzo muhimu katika kuboresha huduma katika sekta ya Ardhi. Katika kufanikisha azma ya matumizi ya TEHAMA, Mfumo Unganishi wa Kuhifadhi Kumbukumbu za Ardhi (Integrated Land Management Information System – ILMIS) umeendelea kuboreshwa na kusambazwa kwa kutumia watalaam wa ndani.

29. **Mheshimiwa Spika,** vilevile, mfumo huo umeboreshwa kwa kuongeza moduli mbalimbali ikiwemo Moduli ya kiganjani (ILMIS Mobile App) ambayo inawezesha uchukuaji wa taarifa za upimaji moja kwa moja kutoka uwandani na kuingizwa katika mfumo. Hatua hii imerahisisha ukusanyaji na uchakataji wa taarifa za utambuzi wa vipande vya ardhi kwa ajili ya utoaji wa Leseni za Makazi na Hati za Hakimiliki za Kimila. Hadi kufikia tarehe 15 Mei 2022, jumla ya Leseni za makazi 18,063 na Hati za Hakimiliki za Kimila 6,861 zimetolewa kupitia mfumo katika mikoa ya Mwanza, Arusha, Mbeya, Rukwa na Singida.

30. **Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2021/22, Wizara iliahidi kuanza kutumia mfumo wa ILMIS na kutoa hati za kieletroniki katika mkoa wa Dodoma na kuendelea kujenga na kusimika miundombinu wezeshi ya TEHAMA kwa awamu katika Ofisi za Ardhi za Mikoa yote nchini. Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa, hadi tarehe 15 Mei, 2022, Hatimiliki za Kielektroniki 6,138 zimetolewa kupitia Mfumo wa ILMIS katika Jiji la Dodoma na ujenzi wa miamala ya upili unaendelea. Aidha, Wizara imeanza kujenga mtandao kiambo (Local Area Network) katika Ofisi za Ardhi za Mikoa ya Iringa, Lindi, Mwanza na Mbeya ambao utakamilika ifikapo Juni, 2022.

**Mitandao hiyo itakapokamilika itaunganishwa na Kituo cha Taifa cha Taarifa za Ardhi.**

31. **Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2022/23, Wizara itaendelea kujenga, kusimika na kuimarisha miundombinu wezeshi ya TEHAMA kwa awamu katika Ofisi za Ardhi za Mikoa na Halmashauri nchini. Vilevile, ukarabati wa mtandao kiambo katika Ofisi za Halmashauri 47 zikiwemo Makao Makuu ya Mikoa ya Iringa, Lindi, Mwanza na Mbeya utafanyika.

32. **Mheshimiwa Spika,** ili kuongeza ufanisi katika utoaji wa huduma kwa kutumia mifumo ya TEHAMA, Wizara imeendelea kuchambua, kufanya nakishi ya michoro (scanning) na kuhifadhi ramani na kumbukumbu za Ardhi katika Ofisi za Ardhi za Mikoa na Halmashauri mbalimbali nchini kwa awamu. Katika kutekeleza azma hiyo, jumla ya Michoro ya Mipangomiji 25,744 yenye viwanja 7,013,474, ramani za upimaji Ardhi 89,512 zenye viwanja 2,842,494, Nyaraka za umiliki 2,388,705 na makadirio ya vipande vya ardhi 1,000,000 katika maeneo ambayo hayajapangwa na kupimwa mijini. Hadi kufikia tarehe

15 Mei, 2022 ubadilishaji wa michoro ya mipangomiji 5,649 yenye viwanja 1,758,424 na ramani za upimaji 31,500 zenye viwanja 598,000 katika Halmashauri 38 umefanyika kutoka analojia kwenda digitali. Aidha, utambuzi wa vipande vya ardhi 52,648 katika Halmashauri za Jiji la Dodoma na Manispaa za Tabora, Shinyanga na Ilemela umekamilika.

33. Mheshimiwa Spika, zoezi la ubadilishaji wa michoro ya mipangomiji, ramani za upimaji na nyaraka za umiliki litakuwa na manufaa makubwa kwa wananchi, wawekezaji wa ndani na nje ya nchi na Taifa kwa ujumla kama ifuatavyo;

(i) Kuwezesha uandaaji wa anwani za makazi na Sensa ya Watu na makazi kwa mwaka 2022;
(ii) Kuwezesha Wizara kuunganishwa na mifumo mingine ya Serikali katika kubadilishana taarifa mathalan, Mfumo wa ILMIS na NaPA;
(iii) Kuwezesha utunzaji wa kumbukumbu za ardhi kidigitali pamoja na utoaji wa Hatimiliki kwa njia ya kielektroniki;
(iv) Kurahisisha usimamizi, utoaji wa huduma na kufanya maamuzi;
(v) Kupunguza udanganyifu na kughushiwa kwa nyaraka mbalimbali za ardhi na hivyo kupunguza migogoro; na
(vi) Kurahisisha ukusanyaji wa mapato ya Serikali ikiwemo utoaji wa ankara kidigitali.

**Upimaji na Ramani (Aya 50 – 55)**

34. **Mheshimiwa Spika,** Wizara ina jukumu la kusimamia na kuratibu upimaji wa ardhi, upimaji wa mipaka ya kimataifa, kutafsiri matangazo ya Serikali ardhini kuhusu mipaka ya kiutawala, pamoja na utayarishaji wa ramani za msingi kwa ajili ya shughuli mbalimbali. Aidha, Wizara ina wajibu wa kutoa miongozo ya upimaji ardhi na uandaaji wa ramani kwa taasisi mbalimbali za Serikali na Sekta Binafsi.

35. **Mheshimiwa Spika,** Wizara imeendelea kuweka miundombinu ya upimaji wa ardhi ikiwemo alama za msingi za upimaji ambazo hurahisisha kazi, kupunguza muda na gharama za upimaji ardhi. Katika mwaka 2021/22, Wizara iliahidi kusimika alama mpya za msingi 80 katika maeneo

36. mbalimbali nchini. Hadi kufikia tarehe 15 Mei, 2022 alama za msingi za upimaji 68 zilisimikwa katika Mikoa ya Dar es Salaam (5), Arusha (8), Dodoma (11), Mara (7), Njombe (8), Simiyu (3), Kigoma (8), Manyara (5), Tanga (5), na Geita (8) na hivyo kuwa na alama za upimaji 935 nchini. Katika mwaka 2022/23 Wizara itasimika alama mpya za msingi 80.

37. **Mheshimiwa Spika,** picha za anga ni nyenzo muhimu katika uandaaji wa ramani za msingi. Kwa mara ya mwisho picha za anga zilipigwa mwishoni mwa miaka ya 1970. Kukosekana kwa picha za anga kumesababisha kutohuishwa kwa ramani za msingi zinazoonesha hali halisi ardhini hivyo kuathiri upangaji wa miji na uwekaji wa miundombinu.

38. **Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2021/22, Wizara iliahidi kununua ndege ndogo isiyotumia rubani (drone) kwa ajili ya kupiga picha za anga zitakazowezesha uandaaji wa ramani za msingi. Napenda kuliarifu Bunge lako kuwa, Wizara imenunua ndege kwa gharama ya shilingi milioni 189 kwa ajili ya kupiga picha za anga. Picha zinazozalishwa zinawezesha kuandaa ramani za msingi zinazotumiwa katika Mfumo Unganishi wa Kuhifadhi Taarifa za Ardhi.

Ndege hii inawezesha upatikanaji wa taarifa zilizopo ardhini pindi zinapohitajika na picha hizo zina ubora kuliko taarifa zinazopatikana kwa picha za satellite. Ndege hii imetumika kupiga picha katika eneo lenye ukubwa wa kilometa za mraba 100 katika Mradi wa Kupanga, Kupima na Kumilikisha ardhi katika Jiji la Dodoma. Aidha, Wataalam wawili (2) wamehitimu mafunzo ya kurusha ndege za aina hiyo na kupata leseni kutoka Mamlaka ya Usalama wa Anga (TCAA).

**Upimaji wa Ardhi Nchi Kavu**

39. **Mheshimiwa Spika,** Wizara ina jukumu la kuratibu na kusimamia upimaji wa viwanja na mashamba unaofanywa na Mamlaka za Upangaji pamoja na sekta binafsi. Katika mwaka 2021/22, Wizara ilipanga kuidhinisha ramani za upimaji wa viwanja na mashamba 500,000 pamoja na kutatua migogoro 25 ya mipaka ya vijiji, hifadhi na Wilaya. Hadi tarehe 15 Mei, 2022, viwanja 298,232 na mashamba 356 ziliidhinishwa na kutunzwa kwenye kanzidata ya Wizara (Jedwali Na. 8). Vilevile, migogoro ya mipaka ya vijiji nane (8) katika Halmashauri ya Wilaya ya Chalinze inaendelea kushughulikiwa na migogoro ya mipaka ya vijiji viwili (2) katika Halmashauri za Wilaya za Nyang'hwale (1) na Nkasi (1) imetatuliwa. Aidha, mgogoro wa Hifadhi za Msitu wa Kalambo na Kijiji cha Kasapa katika Wilaya ya Nkasi umeshughulikiwa. Pia, mipaka ya maeneo ya kupumzishia mifugo ya Mkwese (Manyoni) na Kinyangiri (Mkalama) imehakikiwa.

**2. UPANGAJI MIJI NA MAENDELEO YA MAKAZI (Aya 56 – 72)**

40. **Mheshimiwa Spika,** katika kulinda maeneo yanayochipukia kuwa miji, Wizara imekwisha andaa mwongozo wa kusimamia uandaaji wa mipango ya uendelezaji wa makazi na ujenzi wa nyumba vijiji ambao unaelekeza namna ya kupanga makazi vjijini kwa kuzingatia vigezo vilivyoainishwa. Ili kufanikisha utekelezaji wa mwongozo huo, Wizara itandaa mafunzo kwa wananchi kwa ajili ya kuwajengea uwezo wa upangaji na usimamizi kwa miji midogo katika maeneo ya vijiji. Nazielekeza Mamlaka za Upangaji kuendelea kutambua na kuwasilisha mapendekezo ya vijiji na miji inayokua na kukidhi vigezo vya kutangazwa kuwa maeneo ya upangaji ili kuyaendeleza kimji.

41. **Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2021/22, Wizara iliahidi kuendelea kuboresha taarifa za Nyumba katika kanzidata ikiwa ni pamoja na kuhamasisha uundwaji wa vyama vya ushirika wa nyumba. Hadi tarehe 15 Mei, 2022, taarifa za waendelezaji na wasimamiaji milki 207 ambao wamejenga jumla ya nyumba 25,239 zimeingizwa katika kanzidata ya nyumba. Aidha, Vyama vya Ushirika wa Nyumba 38 vyenye wanachama 2,247 ambavyo vimejenga jumla ya nyumba 1,056 katika Mikoa ya Dar es salaam, Dodoma, Iringa, Kagera, Musoma, Morogoro, Mwanza, na Shinyanga vimeingizwa katika kanzidata.

Katika mwaka 2022/23, Wizara kwa kushirikiana na Tume ya Maendeleo ya Vyama vya Ushirika itaendelea kuhamasisha ujenzi wa nyumba kupitia vyama vya ushirika wa nyumba na kuvijengea mazingira ya kupata mikopo yenye masharti nafuu kutoka taasisi za fedha.

**Sensa ya Majengo**

42. **Mheshimiwa Spika,** Serikali imekuwa ikikabiliwa na ukosefu wa takwimu sahihi za majengo nchini. Sensa ya majengo ambayo itafanyika kwa mara ya kwanza tangu nchi ipate uhuru itawezesha upatikanaji wa takwimu za uhakika na sahihi za majengo kwa ajili ya mipango ya maendeleo ya kiuchumi na kijamii. Upatikanaji wa takwimu sahihi na za uhakika ni sehemu ya utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Maendeleo ya Makazi ya mwaka 2000 na Ilani ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) ya Mwaka 2020 – 2025. Ili kufanikisha zoezi la Sensa ya Majengo Wizara imekamilisha maandalizi ya dodoso la majengo, mwongozo wa Mkufunzi na Makarani, mwongozo wa ukusanyaji taaarifa za majengo na kufanya kikao cha wadau wa sekta ya majenzi. Katika utekelezaji wa sensa ya majengo na anwani za makazi ni vyema maeneo ambayo ni hatarishi, hifadhi za miundombinu mbalimbali pamoja na maeneo yenye migogoro zoezi husika lifanyike baada ya kujiridhisha na uhalali ya maeneo hayo.

Nawahimiza wamiliki wa majengo nchini kushiriki zoezi la sense ya watu na makazi na kutoa taarifa sahihi za matumizi ya jengo, hali ya jengo na umiliki wake. Kwa majengo ambayo hayatumiki, ninaelekeza viongozi wa mitaa na vitongoji kuchukua taarifa za majengo hayo na wamiliki wake kupitia fomu maalum iliyoandaliwa.

**Usimamizi wa Sekta ya Milki**

43. **Mheshimiwa Spika**, kwa muda mrefu Sekta ya Milki imekosa usimamizi, takwimu na taarifa sahihi, uratibu madhubuti kwa waendelezaji, Taasisi za fedha, watumiaji na mawakala wa sekta. Changamoto hizi zimesababisha kutotambuliwa kwa mchango wa sekta hii katika uchumi wa nchi. Dhamira ya Serikali ni kuwa na mfumo madhubuti wa kitaasisi wa kusimamia na kuratibu uendelezaji sekta ya milki nchini. Kwa kutambua umuhimu huo, Wizara imeanzisha Kitengo cha milki (Real Estate Unit) ambacho kitasimamia pamoja na masuala mengine uwekaji wa mfumo wa uwazi na usawa katika biashara na huduma za sekta ya milki nchini, ikiwemo kuhakikisha viwango vya kodi ya pango la nyumba vinatozwa kwa mujibu wa soko na taratibu za ulipaji wa kodi hiyo haumuumizi mlaji. Kitengo hiki kitawajibika kuandaa na kusimamia utekelezaji wa Sera, Sheria, kanuni na Miongozo mbalimbali kwa ajili ya kusimamia na kukuza sekta ya milki.

**Mapitio ya Sera na Sheria ( Aya 74 – 79)**

44. **Mheshimiwa Spika,** ili kuendana na mabadiliko ya kiuchumi, kijamii, maendeleo ya sayansi na teknolojia pamoja na changamoto zinazotokana na mabadiliko ya Tabia nchi; katika mwaka 2021/22 Wizara iliahidi kukamilisha mapitio ya Sera ya Taifa ya Ardhi ya mwaka 1995, kukamilisha uchambuzi wa maoni ya wadau kuhusu mapitio ya Sera ya Maendeleo ya Makazi ya mwaka 2000 na rasimu ya Sera mpya ya Nyumba. Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa mapitio ya Sera ya Taifa ya Ardhi ya mwaka 1995 yako katika ngazi ya maamuzi serikalini. Aidha, marekebisho ya Sera ya Taifa ya Maendeleo ya Makazi ya mwaka 2000 na rasimu ya Sera mpya ya Taifa ya Nyumba yako katika hatua ya kukamilisha uchambuzi wa maoni ya wadau kabla ya kuwasilishwa serikalini kwa maamuzi.

**Utozaji Riba katika Kodi ya Pango la Ardhi**

45. **Mheshimiwa Spika,** kwa muda mrefu kumekuwa na malalamiko kutoka kwa wananchi yanayotokana na takwa la kisheria la kutoza riba baada ya miezi sita ndani ya mwaka wa fedha ambao kodi ya pango la ardhi inapaswa kulipwa. Ili kuondoa malalamiko hayo, Wizara inakusudia kufanya marekebisho ya Sheria ya Ardhi kupitia Mswaada wa Sheria ya Fedha ili riba ya kuchelewa kulipa kodi ya pango la ardhi ianze kutozwa baada ya kuisha kwa mwaka wa fedha.

46. **Mheshimiwa Spika**, utekelezaji wa Programu ya Kupanga, Kupima na Kumilikisha Ardhi unaendelea ambapo katika mwaka wa fedha 2021/22, Wizara iliidhinishiwa shilingi bilioni 8. Aidha, Wizara ilipokea shilingi bilioni 50 kwa ajili ya kukopesha Halmashauri na Taasisi kwa ajili ya utekelezaji wa Programu hii. Hadi tarehe 15 Mei, 2022, kati ya fedha zilizoidhinishwa, Wizara imepokea shilingi bilioni 5.6 hivyo kufanya kuwa na jumla ya shilingi bilioni 55.6 kwa ajili utekelezaji wa Programu. Fedha hizi zimekopeshwa kwenye Halmashauri 92, Vyuo vya Ardhi vitatu (3) na Ofisi ya Ardhi ya Mkoa wa Iringa ili kuwezesha upangaji, upimaji na umilikishaji wa viwanja takriban 373,155. Vigezo vilivyotumika kutoa mikopo ni pamoja na uwepo wa andiko la mradi linaloonesha uwezo wa kurejesha, historia ya Halmashauri/ Taasisi kwenye urejeshaji wa mikopo, uwepo wa vifaa vya upimaji na wataalamu na utayari wa Halmashauri/Taasisi husika kwenye utekelezaji wa miradi.

# HOTUBA

47.**Mheshimiwa Spika**, kupitia programu hii Serikali inatarajia kupata mapato yenye jumla ya shilingi bilioni 51.6 (baada ya urejeshwaji mkopo) kwa mwaka wa kwanza na kuongeza wigo wa mapato kwa wastani wa kiasi cha shilingi bilioni 5.6 kwa mwaka kwa miaka inayofuata, kupunguza migogoro ya ardhi na kuwapatia wananchi fursa ya kuwa na hati miliki za makazi.

Pamoja na jitihada za Serikali za kutoa fedha kwa ajili ya kutekeleza shughuli za Sekta ya Ardhi, Mamlaka za Upangaji zina jukumu la kupanga, kupima na kumilikisha ardhi kwa mujibu wa Sheria. Natoa rai kwa Mamlaka za upangaji kuhakikisha kuwa zinatenga fedha asilimia 40 hadi 60 ya faida ya fedha za mkopo kwa ajili ya Kupanga, Kupima na Kumilikisha Ardhi kwa kuzingatia Mwongozo wa Madaraja ya Halmashauri uliotolewa na Ofisi ya Rais – TAMISEMI.

**Mradi wa Uboreshaji wa Milki za Ardhi – LTIP (Aya 81 – 91)**

48. **Mheshimiwa Spika,** Mradi wa Uboreshaji Milki za Ardhi umesainiwa na Serikali Februari, 2022 na utaanza kutekelezwa na Wizara yangu kwa kushirikiana na Benki ya Dunia katika mwaka 2022/23. Mradi huu utatekelezwa kwa kipindi cha miaka mitano (2022/23 – 2027/28) na unalenga kuimarisha usalama wa milki za ardhi; kuboresha usimamizi wa taarifa za ardhi ikiwemo Mfumo Unganishi wa Kuhifadhi Taarifa za Ardhi (ILMIS); kuimarisha miundombinu ya Upimaji na Ramani; na kujenga majengo ya Ofisi za Ardhi za Mikoa 25.

49. **Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2022/23, Wizara imepanga kujenga majengo ya Ofisi za Ardhi za Mikoa 25; kuboresha mfumo wa ILMIS; kutoa Hatimiliki 150,000 katika Halmashauri 10; kutoa Hati za Hakimiliki za Kimila 50,000 katika Vijiji 50; kuandaa Mipango ya Matumizi ya Ardhi ya Vijiji 50 katika Wilaya sita (6) na Mipango ya Matumizi ya

Ardhi ya Wilaya hizo; na kutoa Leseni za Makazi 250,000. Katika utekelezaji wa kazi hizi, Wizara inatarajia kutoa fursa za ajira za muda mfupi 2,300 na vibarua 4,200.

**Mradi wa Uimarishaji wa Mipaka ya Kimataifa**

50. **Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2021/22, Wizara iliahidi kuendelea na uimarishaji wa mipaka ya nchi kavu yenye urefu wa kilometa 100 kati ya Tanzania na Burundi na kilometa 128 kati ya Tanzania na Kenya kwa kushirikiana na mamlaka za Serikali za nchi hizo. Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa hadi tarehe 15 Mei, 2022, kilometa 83 za mpaka wa Tanzania na Kenya zimeimarishwa na kazi inaendelea. Pia, ramani za msingi za mpaka kwa kipande cha kilometa 238 kutoka Ziwa Viktoria hadi Ziwa Natron ambazo zitatumika kuandaa Mkataba wa mpaka zimeandaliwa.

51.**Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa fedha 2022/23, Wizara itaendelea kuimarisha mpaka wa Tanzania na Kenya kutoka Namanga hadi Tarakea wenye urefu wa kilometa 110 pamoja na kuchora ramani za msingi za kipande cha kilometa 110 kutoka Ziwa Natron hadi Namanga. Aidha, Wizara itaendelea na uimarishaji wa sehemu ya mpaka wa Tanzania na Burundi wenye urefu wa kilometa 100 kutoka ukingoni mwa Ziwa Tanganyika (kijiji cha Kagunga) hadi unapoanzia Mto Malagarasi (kijiji cha Manyovu) mkoani Kigoma.

52.**Mheshimiwa Spika,** pamoja na malengo yaliyopo katika mwaka wa fedha 2022/23, Wizara inatambua umuhimu wa kukamilisha kwa haraka zoezi la uimarishaji wa mipaka ya kimataifa ili kuimarisha mahusiano ya kidiplomasia, ulinzi na usalama, na mahusiano baina ya jamii zinazoishi maeneo ya mipakani. Ili kuongeza kasi na kuhakikisha kwamba kazi ya uimarishaji mipaka inakamilika ifikapo 2027 kama ilivyokubaliwa na Umoja wa Afrika (AU), Serikali inaandaa mkakati utakaowezesha upatikanaji wa rasilimali kwa ajili ya kuimarisha na kuweka miundombinu ya barabara na mawasiliano.

**Miradi ya Kimkakati ya Kitaifa**

53.**Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2021/22, Wizara imeendelea kushiriki kikamilifu katika kuwezesha utekelezaji wa Miradi ya Kimkakati ya Kitaifa. Miradi hiyo ni Ujenzi wa Bwawa la Kuzalisha Umeme la Julius Nyerere, Ujenzi wa Bomba la Mafuta kutoka Hoima nchini Uganda hadi Chongoleani - Tanga nchini Tanzania na ujenzi wa Reli ya Kisasa (SGR).

**Mradi wa Uzalishaji Umeme wa Julius Nyerere**

54.**Mheshimiwa Spika**, hadi kufikia tarehe 15 Mei, 2022 mipangokina mitatu (3) yenye viwanja 2,141 iliandaliwa katika Miji Midogo ya Mloka na Ikwiriri.

Vilevile, Vijiji 69 vimeandaliwa mipango ya matumizi ya ardhi katika maeneo yanayozunguka na kutiririsha maji katika kidakio cha mto Rufiji kwenda katika Bwawa la Ufuaji wa Umeme la Julius Nyerere (JNHPP) katika wilaya ya Mbarali (14), Mufindi (11) Kilolo (8) na Wangingo'mbe (36).

**Mradi wa Ujenzi wa Reli ya Kisasa**

55.**Mheshimiwa Spika**, Wizara imeendelea kushiriki katika utekelezaji wa mradi wa ujenzi wa Reli ya kisasa kutoka Morogoro hadi Makutupora kwa awamu ya pili na Isaka hadi Mwanza awamu ya tano. Usanifu wa michoro ya mipangomiji katika vituo tisa (9) vya Dar es Salaam, Soga, Ruvu, Kwala, Morogoro, Kilosa, Chanzulu, Gulwe na Dodoma umekamilika. Aidha, usanifu wa michoro ya mipangomiji katika maeneo ya vituo vya Igandu (Dodoma), Tura (Tabora), Nkalalo (Mwanza), Isaka na Ishololo (Shinyanga) unaendelea.

Vilevile, uthamini wa mali umefanyika katika kipande cha kuanzia Morogoro hadi Makutupora ambapo wananchi 1,462 wamefanyiwa uthamini wenye thamani ya shilingi bilioni 34.4 na kipande cha kutoka Isaka hadi Mwanza wananchi 5,846 wamefanyiwa uthamini wenye thamani ya shilingi bilioni 20.4 na kazi ya uthamini inaendelea. Pia, vijiji 22 vimeandaliwa mipango ya matumizi ya ardhi katika Halmashauri za Wilaya ya Kibaha (10), Chamwino (8) na Mpwapwa (4).

**Mradi wa Ujenzi wa Bomba la Mafuta**

56.**Mheshimiwa Spika,** hadi tarehe 15 Mei, 2022, Wizara imekamilisha uthamini wa mali katika maeneo 14 ya kipaumbele ya Mradi ambapo wananchi 350 wamefidiwa jumla ya shilingi bilioni 1.6. Aidha, utwaaji ardhi ya Mkuza wa Bomba la Mafuta wenye urefu wa kilometa 1,147 umekamilika. Vilevile, mipangokina 42 yenye viwanja 21,355 pembezoni mwa Mkuza wa Bomba la Mafuta imeandaliwa. Katika mwaka 2022/2023, Wizara itaendelea na utekelezaji wa shughuli zinazohusiana na sekta ya ardhi kwa kushirikiana na Mamlaka za Upangaji katika Mikoa inayopitiwa na Mradi.

**3. SHUGHULI ZILIZOTEKELEZWA NA TAASISI ZILIZO CHINI YA WIZARA**

**SHIRIKA LA NYUMBA LA TAIFA (Aya 96 – 106)**

57.**Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2021/22, Shirika lilipanga kukamilisha Mradi wa Morocco Square Jijini Dar es Salaam. Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa hadi tarehe 15 Mei, 2022, utekelezaji wa Mradi umefikia asilimia 93. Hatua hii imetokana na Serikali kuruhusu Shirika kukopa shilingi bilioni 173.9 ili kukamilisha Mradi huu na miradi mingine iliyokuwa imesimama tangu mwaka 2018 kwa kukosa fedha. Mpaka sasa Shirika limekopa shilingi bilioni 44.7 kati ya fedha hizo kwa ajili ya kukamilisha Miradi ya Morocco Square na Kiwanja Na. 300 Regent Estate.

58.**Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2021/22, Shirika lilipanga kuendelea na ujenzi wa nyumba katika Halmashauri ya Wilaya ya Chamwino (101) na Jiji la Dodoma (Iyumbu - 303) kwa ajili ya kupangisha na kuuza ikiwa ni utekelezaji wa mradi wa nyumba 1,000. Napenda kuliarifu Bunge lako kuwa hadi tarehe 15 Mei, 2022, ujenzi wa nyumba 100 na jengo la maduka katika Wilaya ya Chamwino umekamilika kwa asilimia 80 na ujenzi wa nyumba 300 na majengo matatu (3) ya huduma za kijamii katika Jiji la Dodoma (Iyumbu) umekamilika kwa asilimia 90.

59.**Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2022/23, Shirika limepanga kutekeleza kazi zifuatazo: -

i) Kukusanya shilingi bilioni 268.03 kutoka kwenye vyanzo mbalimbali vya mapato;
ii) Kuendelea kukamilisha mradi wa ujenzi wa nyumba 300 kati ya nyumba 1,000 za gharama nafuu Jijini Dodoma kwa ajili ya kuuza na kupangisha;
iii) Kukamilisha ujenzi wa Mradi wa Morocco square na kuendelea na Miradi katika Kiwanja Na. 711 Kawe, Golden Premier (GPR-Project) na ujenzi wa nyumba 500 katika eneo la Kawe kwa ajili ya wananchi wa kipato cha kati cha chini ambapo nyumba 360 zitajengwa awamu ya kwanza na nyumba 140 zitajengwa awamu ya pili;
iv) Kuendelea na ujenzi wa majengo ya biashara katika maeneo mbalimbali nchini ikiwemo Bukoba, Mwanza, Dodoma, Kahama, Morogoro, Masasi na Lindi;
v) Kuandaa Mpango Kabambe wa matumizi ya ardhi katika maeneo ya Iwambi na Mwashiwawala – Mbeya, Uvumba – Dar es Salaam na Mafuru Village - Morogoro;
vi) Kuendelea na utekelezaji wa miradi ya ukandarasi ikiwemo ujenzi wa Majengo ya Ofisi za Wizara nane (8) Jijini Dodoma, ujenzi wa Jengo la Shule ya Uchumi ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Ujenzi wa majengo matano (5) ya Wakala wa Ununuzi wa Serikali (GPSA), ujenzi wa jengo la TANZANITE Mirerani, ujenzi wa Jengo la Kitengo cha Moyo cha Jakaya Kikwete (JKCI) na miradi mingine itakayojitokeza;
vii) Kununua ardhi ekari 400 katika maeneo mbalimbali ya kimkakati kwa ajili ya ujenzi wa nyumba na akiba ya ardhi;
viii) Kuanza utekelezaji wa Sera ya Ubia itakayoruhusu Sekta Binafsi kushiriki katika uendelezaji wa maeneo ya Shirika;
ix) Kuendelea na ujenzi wa viwanda vya kuzalisha vifaa vya ujenzi hususan kokoto na matofali; na
x) Kuendelea kutoa elimu kwa umma kuhusu masuala ya nyumba na kulitangaza Shirika na Sekta ya Milki nchini kupitia vyombo vya habari.

**Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi ( Aya 107 – 121)**

**Uandaaji wa Mipango ya Matumizi ya Ardhi ngazi ya Wilaya**

60.**Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2021/22, Tume kwa kushirikiana na Mamlaka za Upangaji na wadau wa kimkakati ilipanga kuandaa mipango ya matumizi ya ardhi ya Wilaya tatu (3). Hadi tarehe 15 Mei, 2022, Tume imeandaa Mipango ya Matumizi ya Ardhi ya Wilaya mbili (2) katika Halmashauri ya Tanganyika (Katavi) na Uvinza (Kigoma). Mipango hii imefanya kuwa na Wilaya 44 zenye mipango ya matumizi ya ardhi nchini. Katika mwaka 2022/23, Tume imepanga kuandaa mipango ya matumizi ya ardhi katika Wilaya nne (4) kwa kushirikiana na wadau mbalimbali.

**Uwezeshaji wa Mamlaka za Upangaji**

61.**Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2021/22, Tume ilipanga kuziwezesha na kuzijengea uwezo Timu Shirikishi za Upangaji wa Matumizi ya Ardhi za Halmashauri za Wilaya 20, Wajumbe 3,420 wa Halmashauri za Vijiji 171, Wajumbe 1,368 wa Kamati za Usimamizi wa Matumizi ya Ardhi, Wajumbe 1,197 wa Mabaraza ya Ardhi ya Vijiji pamoja na kutoa miongo-

zo na elimu kwa umma kuhusu masuala ya sheria, kanuni na taratibu za upangaji na usimamizi wa mipango ya matumizi ya ardhi.

62.**Mheshimiwa Spika**, hadi tarehe 15 Mei, 2022, Tume imeziwezesha na kuzijengea uwezo Timu Shirikishi za Upangaji wa Matumizi ya Ardhi za Halmashauri za Wilaya 31 zenye wajumbe 248, wajumbe 4,640 kutoka Halmashauri za Vijiji 232, wajumbe 1,856 wa Kamati za Usimamizi wa Matumizi ya Ardhi na wajumbe 1,624 wa Mabaraza ya Ardhi ya Vijiji.

63.**Mheshimiwa Spika;** Serikali inatambua uwepo wa wadau wanao shirikiana na Tume na Mamlaka zingine za Upangaji katika kuwezesha Uandaaji wa Mipango ya matumizi ya ardhi katika maeneo mbalimbali hapa nchini. Aidha, changamoto inayoonekana ni kwa wadau hawa kutofikia hatua ya kuandaa mipango kina ya matumizi ya Ardhi inayowezesha utoaji wa Hati Miliki za Kimila na Upangaji wa maeneo ya Vijiji. Vilevile, Wadau wengi kuwa na malengo yasiyoakisi matakwa halisi ya Wananchi ya kuwainua kiuchumi na miliki salama ili kutimiza malengo ya Serikali ya kuwezesha Wananchi kiuchumi kupitia rasimali ardhi. Naomba kutoa rai kwa wadau na Mamlaka za Upangaji zinazohusika uandaaji, usimamizi na utekelezaji wa mipango ya matumizi ya ardhi katika ngazi ya Taifa, Kanda, Wilaya na Vijiji kuzingatia Miongozo ya Serikali na Mpango wa Tatu wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka mitano (2021/22 – 2025/26) unaolenga pamoja na mambo mengine kuwezesha wananchi kiuchumi, Kijamii na kuwa na Milki salama.

**Tume ya Taifa ya Mpango ya Matumizi ya Ardhi ( Aya 106 -118)**

64.**Mheshimiwa Spika,** Tume imeendelea kuwezesha Mamlaka za Upangaji kutenga maeneo kwa ajili ya matumizi mbalimbali ya ardhi. Jumla ya ardhi yenye ukubwa wa hekta 487,634 imetengwa kwa ajili ya kilimo, hekta 137,404.37 kwa ajili ya nyanda za malisho, hekta 254,366.59 kwa ajili ya makazi na kilimo na hekta 28,666.10 kwa ajili ya ardhi ya akiba ikiwemo uwekezaji. Katika mwaka 2022/23, Tume kwa kushirikiana na wadau itaendelea kuwezesha uandaaji, utekelezaji na usimamizi wa Mipango ya Matumizi ya Ardhi ya Vijiji 200 katika Mamlaka mbalimbali za upangaji nchini.

**Utawala Bora na Uwajibikaji**

65.**Mheshimiwa Spika,** Wizara inatambua umuhimu wa kuimarisha mifumo ya utawala bora, uwajibikaji na kudhibiti ukiukwaji wa maadili kwa watumishi wa sekta ya Ardhi. Katika mwaka 2022/23, Wizara itaanzisha Mfumo wa Usimamizi wa Sekta ya Ardhi (Land Governance Framework) ambao utaongeza uwajibikaji, uwazi na ufanisi katika kutoa huduma za sekta na itaendelea kusimamia utekelezaji wa ahadi zilizoainishwa kwenye Mkataba wa Huduma kwa Mteja kwa lengo la kuboresha utoaji wa huduma kwa wananchi.

66.**Mheshimiwa spika,** kwa sababu ya muda baadhi ya maswala yanayohusu masuala yetu ya vyuo vya ardhi Tabora na Morogoro, Bodi za wataalam, maswala mtambuka na habari na elimu kwa umma yameelezewa kwa kina katika Aya ya 121 – 131.

**Shukrani (Aya 130 – 134)**

67.**Mheshimiwa Spika**, ninaomba kumalizia hotuba hii kwa kumshukuru Mhe. Samia Suluhu Hassani Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuniamini na kunipa dhamana ya kuiongza Wizara hii. Kwa kipekee napenda kuwashukuru Mhe. Dkt. Phillip Isdor Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mhe. Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb.), Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Vilevile kipekee nakushukuru wewe binafsi Mhe. Spika, Naibu Spika na Wenyeviti wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kazi nzuri na uongozi thabiti katika kusimamia shughuli za Bunge. Kadhalika, naishukuru sana Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii inayoongozwa na Mwenyekiti Mhe. Ally Juma Makoa (Mb.) na Makamu Mwenyekiti Mhe. Shabani Omary Shekilindi (Mb.) na Wajumbe wa Kamati kwa maoni na ushauri wanaotoa katika kuboresha utekelezaji wa majukumu ya Wizara yangu.

Aidha, nawashukuru kwa dhati Waheshimiwa Mawaziri, Naibu Mawaziri na Makatibu Wakuu kutoka katika Wizara mbalimbali tulioshirikiana katika utekelezaji wa majukumu ya Serikali.

68.**Mheshimiwa Spika**, kwa umuhimu wa pekee natambua mchango wa viongozi wenzangu katika kutekeleza majukumu ya Wizara. Ninamshukuru Naibu Waziri, Mhe. Ridhiwani Jakaya Kikwete (Mb.), kwa kunisaidia katika kutekeleza majukumu ya Wizara. Aidha, natoa shukrani zangu za dhati kwa Katibu Mkuu Dkt. Allan H. Kijazi, Naibu Katibu Mkuu Bw. Nicholas M. Mkapa, Mkurugenzi Mkuu wa Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi, Prof. Wakuru Magigi, Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Taifa la Nyumba Bw. Nehemiah Kyando Mchechu, Kamishna wa Ardhi Bw. Nathaniel Mathew Nhonge, Mkuu wa Chuo cha Ardhi Tabora Bw. Biseko Musiba na Mkuu wa Chuo cha Ardhi Morogoro Bw. Huruma Lugalla kwa kazi kubwa wanayoifanya ya kusimamia utekelezaji wa majukumu ya Wizara na Taasisi zake.

69.**Mheshimiwa Spika,** Vilevile, napenda kuwashukuru Wakuu wa Idara na Vitengo pamoja na watumishi wote wa Wizara, kwa kuendelea kufanikisha utekelezaji wa majukumu ya Wizara. Vilevile, nawashukuru Wakuu wa Mikoa, Wakuu wa Wilaya kwa kazi kubwa ya utatuzi wa migogoro ya ardhi wanayoifanya hususan kwa kutenga siku maalum ya kusikiliza wananchi wenye changamoto za migogoro ya ardhi.

70.**Mheshimiwa Spika,** vilevile, napenda kuwashukuru wadau wote wa Sekta ya Ardhi wanaojumuisha Mamlaka za Serikali za Mitaa, sekta binafsi, Bodi za Kitaaluma, Kamati za Ugawaji Ardhi, washirika wa maendeleo wa ndani na nje na wananchi kwa michango yao katika utekelezaji wa majukumu ya Wizara. Tunatambua na kuthamini michango yenu katika kuwezesha utekelezaji wa majukumu yetu kwa maslahi ya wananchi na Taifa.

**4. HITIMISHO**

71.**Mheshimiwa Spika,** napenda kuhitimisha hotuba yangu kwa kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba katika mwaka 2022/23, Wizara itaendelea kufanya mageuzi kwa kuboresha huduma zinazotolewa katika Sekta ya Ardhi kwa kuendelea kuwekeza katika matumizi ya mifumo ya TEHAMA katika utoaji wa huduma na pia kuongeza kasi ya upangaji, upimaji na umilikishaji ardhi pamoja na udhibiti wa migogoro ya matumizi ya ardhi. Mageuzi haya yanalenga kuwapunguzia wananchi gharama, kuimarisha usalama wa milki za ardhi pamoja na kuongeza thamani ya ardhi na hivyo kukuza kipato cha mwananchi mmoja mmoja na pato la Taifa.

**5. MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2022/23**

72.**Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2022/23, Wizara inatarajia kukusanya shilingi bilioni 250.1 kutokana na maduhuli ya Sekta ya Ardhi kwa kutekeleza mikakati ambayo imeainishwa katika hotuba hii.

Aidha, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu lijadili na kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi (Fungu 48) na Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi (Fungu 03) kama ifuatavyo: -

**Fungu 48: Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo Makazi**

| | MAPATO | SHILINGI |
|---|---|---|
| A | Mapato ya Serikali | **250.100.000.000** |
| | **MATUMIZI** | |
| B | Matumizi ya Kawaida: | |
| | Mishahara | 44,383,797,000.00 |
| | Matumizi Mengineyo | 33.918.651.000.00 |
| | **Jumla Ndogo** | **78.302.448.000.00** |
| C | Matumizi ya Maendeleo: | |
| | Fedha za Ndani | 14,006,000,000.00 |
| | Fedha za Nje | 13.147.322.000.00 |
| | **Jumla Ndogo** | **27.153.322.000.00** |
| | **JUMLA MATUMIZI (B+C)** | **105.455.770.000.00** |

Jumla ya Matumizi ya Kawaida na Maendeleo ya Fungu 48 ni shilingi 105,455,770,000/=.

**Fungu Na. 03: Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi.**

| Aina ya Bajeti | | | 2022/23 (Shs) |
|---|---|---|---|
| **1. Mapato** | | | 4,873,704,000 |
| **JUMLA YA MAPATO** | | | 4,873,704,000 |
| **2. Matumizi ya Kawaida** | Mishahara | PE | 1,977,882,000 |
| | **Jumla ya Mshahara** | | **1,977,882,000** |
| | Matumizi Mengineyo | OC | 1,479,822,000 |
| | **Jumla ya Matumizi Mengineyo** | | **1,479,822,000** |
| **JUMLA YA MATUMIZI YA KAWAIDA** | | | **3,457,704,000** |
| **3. Matumizi ya Maendeleo** | Ndani | | 1,410,000,000 |
| | Nje | | 0 |
| **JUMLA YA MATUMIZI YA MAENDELEO** | | | **1,410,000,000** |
| **JUMLA YA MATUMIZI YA KAWAIDA NA MATUMIZI YA MAENDELEO** | | | **4,867,704,000** |

**Jumla ya Matumizi ya Kawaida na Maendeleo ya Fungu 03 ni shilingi 4,867,704,000/=.**

73.**Mheshimiwa Spika,** jumla kuu ya fedha zinazoombwa na Wizara (Fungu 48 na Fungu 03) ili Bunge liweze kujadili na kuidhinisha ni shilingi 110,323,474,000/=

74.**Mheshimiwa Spika,** naomba kuhitimisha hotuba yangu kwa kutoa shukrani zangu za dhati kwako binafsi na kwa Waheshimiwa Wabunge kwa kunisikiliza. Pamoja na hotuba hii yameambatishwa majedwali ambayo yameainisha kwa kina takwimu pamoja na shughuli zilizotekelezwa. Aidha, hotuba hii inapatikana kwenye tovuti ya Wizara ambayo ni www.lands.go.tz.

75.***Mheshimiwa Spika,*** naomba kutoa hoja.



# Kilimo cha viungo jinsi kinavyokuza utalii Pemba

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

KILIMO cha viungo kisiwani Pemba kimechangia kukuza sekta ya utalii kutokana na kuwa kivutio kikubwa cha utalii na wageni kutembelea mashamba yake ili kujionea uzalishaji wake.

Hayo yalielezwa na Ofisa Utalii kutoka Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale Pemba, Khalid Kombo Khamis, wakati akizungumza na waandishi wa habari baada ya ziara maalum ya kutembelea mashamba ya viungo Pemba iliyoandaliwa na jumuiya ya waandishi wa habari za mazingira Tanzania (JET).

Alisema kundi kubwa la watalii wanaofika Pemba hujifunza vitu vingi ikiwamo mashambaya viungo na kujionea uzalishaji wa viungo hivyo.

"Pemba tunazalisha mdalasini mwingi sana, lakini Wazazibari tulio wengi hatuutumii ipasavyo wakati wenzetu watalii wanaamini kuwa mdalasini unapunguza uwezekano wa kupata saratani," alisema.

Ofisa huyo aliwataka wananchi kuitumia fursa ya kilimo cha viungo na kutowaachia wageni pekee kutembelea mashamba hayo kwa sababu viungo hivyo ni lulu kubwa ikiwamo karafuu na vanila.

"Wapo watalii wanaokuja kwa ajili ya starehe, lakini wengine wanakuja kwa ajili ya kujifunza vitu na hali ya kimazingira Pemba ni bikra kabisa hali ya ukijani imetawala bado miti ya asili ipo na imekuwa ni kivutio pekee kwa watalii," alisema.

Khalid alisema Wizara ya Utalii inawahamasisha wakulima kulima kilimo cha viungo na huchangia pia uhifadhi wa mazingira.

Alisema kilimo hicho ni hai na ambacho kinazingatia uhifadhi wa mazingira na hakihitaji utumiaji wa mbolea za kemikali.

Alisema katika mashamba hayo haikubaliki kutumia kemikali au matumizi ya mfuko wa plastiki ili kutunza afya ya mtumiaji na ubora wa mazao hayo.

"Tunataka turejee katika uasilia ambao unaweza kuisaidia jamii yetu na katika uhifadhi wa mazingira tupo katika nyanja tofauti na utalii ni suala mtambuka inagusa kila pande hivyo mazingira bora yanahitajika ili utalii kuimarika," alisema.

Alisema bila ya uhifadhi wa mazingira viumbe hai vitatoweka na ndiyo maana serikali inashajihisha utunzaji wa mazingira ikiwamo uhifadhi wa misitu na rasilimali za bahari na nchi kavu ili wananchi kunufaika na rasilimali hizo.

"Spice zote zinazotoka Pemba ikiwamo karafuu na vanila tunahakikisha zina ubora wa hali ya juu na hata zikipimwa duniani huwa na kiwango cha gredi ya kwanza," alisema ofisa huyo.

Aidha, alisema wanatoa elimu kwa jamii kutokata miti ovyo ikiwamo miti ya mkarafuu ambayo ina uwezo wa kuishi hadi miaka 100 na serikali imechukua jitihada za kuhakikisha miti hiyo inadumu.

"Ukionekana na mti wa mkarafuu na miti mingine ni kosa kubwa na unashtakiwa na serikali inahifadhi mazingira ili kulinusuru taifa," alisema.

Kwa upande wao wakulima wa viungo katika Kijiji cha Mtabwe daya, walisema kuwa kilimo hicho ni mkombozi kwao kwa sababu kimewainua kiuchumi na kuondokana na umasikini.

Muhammed Ali Mmanga ni miongoni mwa wakulima hao alisema kuwa licha ya kulima viungo kwa ajili ya biashara, pia shamba lake ameliandaa kwa ajili ya kivutio kwa watalii ambao hufika kijijini hapo kujifunza.

Alisema kuwa soko la kilimo cha viungo ni la uhakika licha ya kukabiliwa na baadhi ya changamoto ikiwamo kushuka kwa bei ya zao la vanila kutoka Shilingi milioni moja kwa kilo moja hadi Shilingi laki tano.

"Hivi sasa bei ya vanila imeshuka sana tunaiomba serikali ikae pamoja na wanunuzi wa zao hili pamoja na sisi wakulima ili kuendelea kufaidika na kilimo hiki," alisema.



Mkulima wa viungo, Bakari Mataka, akionyesha zao la vanila kwa waandishi wa habari, waliofanya ziara ya mafunzo shambani kwake, eneo la Mtambwe Daya, kisiwani Pemba jana, iliyoandaliwa na chama cha waandishi wa habari za mazingira Tanzania (JET). **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

## Bilioni 8/- kulipa fidia waliopisha ujenzi uwanja wa ndege Pemba

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

SERIKALI ya Zanzibar imesema imetenga Shilingi bilioni nane kwa ajili ya kulipa fidia wananchi mbalimbali waliopisha mali zao ikiwamo mashamba na nyumba kwa ajili ya kuruhusu utekelezaji wa mradi mkubwa wa upanuzi wa uwanja wa ndege wa Pemba.

Hayo yalisemwa katika kikao cha Baraza la Wawakilishi na Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji, Juma Makungu, wakati akitoa ufafanuzi kuhusu nia ya serikali ya ujenzi wa uwanja wa ndege wa Pemba pamoja na mchakato wa kulipa fidia.

Makungu alisema serikali imejipanga kutekeleza mradi huo wa ujenzi wa uwanja wa ndege wa Pemba ikiwa ni sehemu ya mikakati ya kukifunguwa kisiwa cha Pemba kiuwekezaji pamoja na utalii.

Alisema miradi miwili inatarajiwa kutekelezwa katika kipindi cha mwaka wa fedha 2022-2023 ikiwamo upanuzi wa Bandari ya Mkoani Pemba.

Alisema tayari upembuzi yakinifu umefanyika katika masuala ya kulipa fidia kwa watu ambao mali zao ikiwamo mashamba na nyumba kuathirika kwa ajili ya kupisha ujenzi wa mradi wa uwanja wa ndege wa Pemba.

"Mheshimiwa Spika napenda kuwajulisha wawakilishi pamoja na wananchi kwa ujumla kwamba tayari tumetenga Shilingi bilioni nane kwa ajili ya kulipa fidia watu wote ambao mali zao zimeathirika kupisha utekelezajiwa mradi wa uwanja wa ndege wa Pemba," alisema.

Aidha, Makungu aliwapongeza wananchi wa maeneo jirani na uwanja wa ndege wa Pemba kwa kuwa watulivu na kuvumilia kwa muda mrefu katika suala la kulipa fidia ambapo mchakato huo sasa umekamilika.

## Mshindi wa Nobel apongezwa Baraza la Wawakilishi

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

NAIBU Spika wa Baraza la Wawakilishi, Mgeni Hassan Juma, amempongeza Mshindi wa Nobel Professa Abdulrazak Gurna, kwa kuendelea kuipa heshima katika kuitangaza Zanzibar na Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Akimtambulisha mgeni huyo kwa wajumbe wa Baraza la Wawakilishi Chukwani Naibu Spika, alisema wananchi wa Zanzibar wanathamini kazi aliyoifanya mwandishi huyo wa fasihi.

Akitaja baadhi ya sifa zake alisema ni Professa wa Kiingereza na mwandishi wa vitabu mbalimbali vinavyompa sifa katika uandishi wake.

Aidha, akitaja miongoni mwa vitabu alivyoandika na kuorodhesha katika tunzo mbalimbali ni pamoja na Paradise alichokiandika mwaka 1994 ambacho kiliorodheshwa katika tuzo na kitabu cha pili ni Byriced 2001 ambacho kimeorodheshwa katika tuzo za price za dunia

Alisema Wazanzibari ni fahari yao na utambulisho wao na kumuomba kuja Zanzibar mara kwa mara kwa sababu anahitajika katika masuala mbalimbali.

Alisema anahitajika zaidi kusaidia katika utalii na elimu hasa lugha ya Kiingereza ili kuwatengeneza vijana kuitumia kama anayoitumia yeye katika uandishi wa vitabu na mambo mengine.

Kwa upande wake Peofesa Gurna, aliwataka vijana kutokata tamaa na kujikita katika uandishi wa vitabu.

## TANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

### KUPOTEA KWA CHETI



**ASHA OMARY KIBWANA**
Anatangaza kupotelewa kwa cheti cha kidato cha nne chenye **REG NO: CSEES.0332/20** Kilicho tolewa na Baraza la mitihani la taifa kupitia shule Morogoro sekondari mwaka **2001** Yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo cha polisi au piga simu **0655610025 DSM/PHQ/RB/206133/2022**

### KUPOTEA KWA CHETI



**REGAN PAUL CHUWA** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S.0499/0094** kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia **OLALENI SECONDARY SCHOOL mwaka 2015.** Kwa yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo cha polisi. **POLISI TAARIFA: DSM/PHQ/RB/197973/2022**

### KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**MARK SEBASTIAN MOKIMIRYA** anatangaza kupotea kwa kadi yake ya gari yenye namba za usajili **T 932 BSM – TOYOTA COROLLA.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. **Taarifa ya Polisi: ARU/ARU/RB/115783/2022.**

### KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**VICTOR MUJWAUZI KARUGABA** anatangaza kupotea kwa kadi yake ya gari yenye namba za usajili **T 620 AFY – SUZUKI ESCUDO.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. **Taarifa ya Polisi: ARU/ARU/RB/205500/2022**

### KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**ROMAN SABAS NGOWI** anatangaza kupotea kwa kadi yake ya gari yenye namba za usajili **T 744 ADQ – TOYOTA LANDCRUISER.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. Taarifa ya Polisi: **ARU/ARU/RB/205498/2022**

### TANGAZO LA KUPOTEA BARUA YA TOLEO

KIWANJA NAMBA 193KITALU HHH SEHEMU 111MANISPAA YA MOSHI

TAARIFA INATOLEWA KWA UMMA KUWA AFISA ARDHI MTEULE WA HALMASHAURI YA MANISPAA YA MOSHI AMEPOKEA TAARIFA KUTOKA KWA GODILIZENI KITALI MMILIKI WA KIWANJA TAJWA TAARIFA YA POLISI YENYE KUMB .KIL/MOS/RB/49899/2022 KUWA AMEPOTEZA NYARAKA TAJWA NATOA MUDA WA SIKU THELATHINI (30)KWA MTU YEYOTE ANAYEISHIKILIA NYARAKA HIYO KUIWASILISHA OFISIN ZA HALMASHAURI YA MANISPAA YA MOSHI.

KAMA SITAPOKEA TAAFIFA YEYOTE BAADA YA MUDA HUO KUPITA NITATOA NYARAKA NYINGINE KWA MTOA TAARIFA.

### KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI BAJAJ BOXER

**TWALIB YASIN MNYAWAMI** anatangaza kupotea kwa kadi ya pikipiki bajaj boxer yenye **USAJILI NAMBA MC125ASU , ENGINE NAMBA: PFZWFA40155.** Kwa yeyote atakaeiona taoe taarifa kituo chochote cha polisi. **POLISI TAARIFA: ARU/ARU/RB/206884/2022**

**IN THE DISTRICT COURT OF DODOMA**
**AT DODOMA**
**PROBATE & ADMINISTRATION CAUSE**
**NO.1 OF 2022**
**In the matter of the estate of the late CHARLES DAVID MWASAMBUNGU of Image within Dodoma City**
**AND**
**In the matter of the Application for letter of Administration BY ANNA SHEMU MANGULA**

**GENERAL CITATION**
**(RULE 75 OF PROBATE RULES GN 369 OF 1963)**

**All PERSONS** claiming to have any interest in the Estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of Administration is made to the above named Petitioners.
Objections to the grant should be filed on or before the **7th June, 2022.**
**Dated at Dodoma this 25TH day of May, 2022.**

DEPUTY REGISTRAR

### KUPOTEA KWA OFA YA KIWANJA

**PAUL ANDREW MWANGA** anatangaza kupotea kwa offer letter ya kiwanja cha **NEW LIFE CRUSADE PLOT NO. 22 BLOCK "D" ILAZO JIJI LA DODOMA.** Yeyote atakaeiyona atoe taarifa kituo cha polisi, taarifa ya polisi **DOD/DOD/RB/188467/2022.**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA-MWANZA**
**SHAURI NA 22 LA 2022**
**IBRAHIM EMMANUEL DABUYA..............................MDAI**
**DHIDI YA**
- **CHAUSIKU MASASI**
- **JOHN SOLOSOLO @JOHN JUMANNE YAMLINGA**

(Msimamizi wa mirathi ya marehemu Yamlinga Kahili)

- **NGASSA JUMANNE YAMLINGA**
- **LUCAS JUMANNE YAMLINGA**
- **GRACE JUMANNE YAMLINGA**
- **JOHN JUMANNE YAMLINGA**
- **PRISCA JUMANNE YAMLINGA**
- **ALFRED JUMANNE YAMLINGA**
- **MANYAMA JUMANNAE YAMLINGA**
- **MARIA JUMANNE YAMLINGA**
- **BUGULU JUMANNE YAMLINGA**

**WADAIWA**

**KWA: JOHN SOLOSOLO@JOHN JUMANNE,NGASSA JUMANNAE YAMLINGA,LUCAS JUMANNE YAMLINGA,GRACE JUMANNE YAMLINGA,JOHN JUMANNE YAMLINGA,PRISCA JUMANNE YAMLINGA,ALFRED JUMANNE YAMLINGA,MANYAMA JUMANNE YAMLINGA,MARIA JUMANNE YAMLINGA na BUGULU JUMANNE YAMLINGA**

Mnafahamishwa kwamba mleta maombi hapo juu amefungua shauri/ombi dhidi yenu katika Baraza la Ardhi na Nyumba za mkoa wa Mwanza ,Ombi hili limepangwa kutajwa tarehe 02/06/2022 katika chumba cha baraza, Barabara ya Makongoro jengo liko mkabala na Mahakama ya Wilaya ya Nyamagana,Tanzania.
Kwa hiyo mnatakiwa kuhudhuria katika Baraza siku hiyo nyie wenyewe, wakili wenu au mtu mwingine anayehusika kisheria.
KAA-Mkijua kwamba kushindwa kufika,Baraza litasikiliza ombi hilo na kutoa uamuzi bila nyie uwepo.
**Imetolewa nami na Amri na Chapa ya Baraza leo tarehe 20/05/2022.**

### KADI YA GARI IMEPOTEA

**Ndugu HUSSEIN MAGATI MWINJANGA** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari aina ya Mitsubishi Fuso yenye namba za usajili **T.601 BCD.** Yeyote atakayeiona anaombwa atoe taarifa kituo chochote cha Polisi kilicho karibu. **TaarifaPolisi: TAN/PAN/RB/27057/2022.**

### KADI YA GARI IMEPOTEA

**Ndugu HUSSEIN MAGATI MWINJANGA** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari aina ya Mitsubishi Fuso yenye namba za usajili T.779 BUL. Yeyote atakayeiona anaombwa atoe taarifa kituo chochote cha Polisi kilicho karibu. **Taarifa Polisi: TAN/PAN/RB/27062/2022**

### KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**NDUGU MICHAEL PAUL MALLYA** anatangaza kupotelewa na kadi ya Gari yenye namba za usajili **T778ACW aina ya TOYOTA COROLLA,**yenye Chasis **No.AE910209531,** Engine **No.5A43433004.**Kwa yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi kilichopo karibu kwa kumbukumbu namba **GE/TR/RB/2398/2022**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**Katika Mahakama ya Mwanzo ya Wilaya ya GEITA**
**Kituo cha NYANKUMBU Mkoa GEITA**
**Shauri a madai/Ndoa Na 88/2022**
**Jina la Mdai: AMANI IR VICOBA**
**Jina la Mdaiwa: BASHIRU JAFARI**
**KUITWA SHAURINI MDAIWA**
**(Kanuni ya 18 ya kanuni za taratibu Madai katika mahakama za Mwanzo)**

**Kwa: BASHIRU JAFARI**
**WA MTAA WA KATUNDO**

**Kwa kuwa Mdai/Wadai wameleta madai yao ya MADAI YA FEDHA TSH. 4,708,000/- ZA MKOPO**

Kwa hiyo unatakiwa kuhudhuria binafsi katika Mahakama hii Tarehe 27 Mwezi 05 Mwaka 2022 saa 2.30 asubuhi kwa mujibu wa madai hayo na kwa kuwa siku hiyo ni siku ya kusikilizwa shauri hili ni lazima kuleta Shahidi/Mashahidi wako na vielelezo vyote vinavyohusu shauri hili kwa ajili ya kujitetea.
ANGALIZO: Kama hautohudhuria siku iliyotajwa hapo juu na ikithibitika kuwa ulipokea hati ya kuitwa shaurini Mahakama inaweza kusikiliza shauri bila ya wewe kuwepo..
Hati hii imetolewa kwa Amri na Muhuri wa Mahakama hii leo Tarehe 19 Mwezi 05 Mwaka 2022

RESIDENT MAGISTRATE GEITA

HAKIMU

*Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa Tupigie 0782253676*

**KWA HABARI MOTOMOTO USIKOSE GAZETI LAKO LA NIPASHE KILA SIKU**

**OFISI ZA MATANGAZO**
**MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,**
**PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 745 700 710.**
**E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com**

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha au kuingia katika gharasma yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# Jeshi la Russia lapata mafanikio Donbass

**KYIV,** UKRAINE

JESHI la Russia limeanza kupata mafanikio baada ya kuchukua baadhi ya maeneo katika mkoa wa Donbass.

Katika siku chache zilizopita, Russia waliteka miji na vijiji kadhaa, na kuwalazimu Waukraine kurudi nyuma kwenye nafasi zao kwa ulinzi.

Russia imepata mafanikio hayo kutokana na mashambulizi makali ya jeshi la ardhini, makombora kutoka kwenye meli na ndege za kivita.

Asubuhi ya jana, gavana wa mkoa wa Luhansk, alisema kwamba kuna wanajeshi wengi wa Russia wanaosonga mbele.

Alisema kuna vikosi vingi vya Russia vilivyoimarishwa na tayari kwa vita virefu.

Taarifa zaidi kutoka jiji la Severodonetsk, inaeleza wanajeshi wa Russia wameuzingira wakijaribu kupata eneo lote la mashariki mwa Ukraine la Luhansk.

Jiji hilo limekuwa katika mashambulizi ya mara kwa mara kwa wiki moja na nusu iliyopita, kulingana na mkuu wa utawala wa ndani wa kijeshi la Ukraine.

Takriban asilimia 90 ya nyumba zimeharibiwa na mapigano, Oleksandr Stryuk alikiambia kituo cha redio cha NV cha Ukraine.

**MIJI MINGINE 40 YASHAMBULIWA**

Taarifa kutoka jeshi la Ukraine, zinasema vikosi vya Russia vimeshambulia zaidi ya miji 40 katika maeneo ya mashariki huko Donbas na Luhansk.

"Wavamizi walifyatua risasi katika miji zaidi ya 40 katika mkoa wa Donetsk na Luhansk, na kuharibu maeneo 47 ya raia, pamoja na nyumba 38 na shule. Kutokana na shambulio hilo raia watano waliuawa na wengine 12 walijeruhiwa.

Ilielezwa Russia imetuma maelfu ya wanajeshi katika eneo hilo, na kushambulia kutoka pande tatu katika jaribio la kuzingira vikosi vya Ukraine vinavyoshikilia miji ya Severodonetsk na Lysychansk.

Gavana wa Luhansk Serhiy Gaidai, alikuwa ameishutumu Russia kwa kutumia kile alichokiita mbinu ya dunia iliyoungua katika juhudi zake za kukamata Severodonetsk.

Gaidai alionya kuwa vikosi vya Russia vimeharibu daraja lote isipokuwa moja katika mto Donets na kusema kuwa jiji hilo liko katika hatari ya kukatwa. **BBC**




Baadhi ya wanafunzi walionusurika katika shambulio la risasi kwenye Shule ya Msingi Uvalde nchini Marekani wakiondolewa katika eneo la tukio juzi. **PICHA: REUTERS**

# Ruto amwomba msamaha Rais Kenyatta

**NAIROBI,** KENYA

NAIBU Rais wa Kenya, William Ruto, amemwomba msamaha Rais Uhuru Kenyatta, kutokana na tofauti zao zilizojitokeza baada ya uchaguzi wa 2018.

Tofauti kati ya Rais Kenyatta na naibu wake zimekuwa wazi baada ya kiongozi huyo kutounga mkono azma ya Ruto ya kuwania urais katika uchaguzi wa Agosti na badala yake anampigia chapuo Raila Odinga.

Wakati wa mkutano wa maombi ulioandaliwa na bunge, Ruto alimwomba rais msamaha.

"Pia najua kuwa kuhudumu kama naibu wa rais huenda sikufikia matarajio ya bosi wangu, Rais Kenyatta na ninaomba unisamehe," alisema.

Aliendelea kumtakia kiongozi huyo kustaafu kwa amani.

Kenyatta anamaliza muhula wake wa pili mwishoni mwaka huu.

Katiba ya nchi hiyo, Rais hana mamlaka ya kumtimua naibu wake, anaweza kuondolewa madarakani iwapo atapigiwa kura bungeni au kutokuwa na uwezo. **BBC**

## Watu 80,000 wakimbia mapigano Goma

**GOMA,** DRC

WATU 80,000 wamekimbia makazi yao katika Jimbo la Kivu Kaskazini kutokana na mapigano makali kati ya jeshi la serikali na waasi wa M23.

Kulingana na Umoja wa Mataifa, mapigano yalianza katika eneo la Rutshuru kabla ya kuenea kilomita 20 kutoka Goma, ambao ni mji mkuu wa jimbo hilo.

Mapigano siku ya juzi yalisababisha kuteketezwa kwa nyumba na watu 10,000 waliokimbilia katika mazingira ya Goma.

Ofisi ya Umoja wa Mataifa ya masuala ya kibinadamu, OCHA, ilisema kuna idadi kubwa ya watu waliokimbia eneo hilo hilo kutokana na mapigano makali yanayoendelea.

Takriban watu 80,000, wengi wao wakiwa wakimbizi wa ndani, wamekimbilia katika maeneo mbalimbali kama makanisa, na shule kwa ajili ya kujihifadhi.

Mashirika ya kibinadamu yanahofia kuwapo kwa hali mbaya kwa wakimbizi ikiwa uhasama utaendelea.

Katika taarifa ya Jumatano jioni, msemaji wa gavana wa jimbo hilo Jenerali Sylvain Ekenge alisema wanakabiliwa na hali ya wasiwasi.

"Gavana wa kijeshi wa jimbo la Kivu Kaskazini anatoa wito kwa wakazi kuwa watulivu na waangalifu, na wasiache hofu," Jenerali Ekenge aliongeza.

Waasi wa M23 wanaripotiwa kudhibiti baadhi ya maeneo katika umbali wa kilomita 25 kutoka Goma, lakini Jenerali Ekenge alisema mashambulizi ya waasi yamerejeshwa nyuma. **BBC**

## Polisi Nigeria yamkamata mlaghai wa mtandaoni

**Lagos,** NIGERIA

KITENGO cha uhalifu wa mtandaoni nchini Nigeria, kimemkamata mwanamume mwenye umri wa miaka 37 anayedaiwa kuwa kiongozi wa kundi la kimataifa la uhalifu wa mtandaoni.

Kulingana na taarifa kutoka polisi wa kimataifa (Interpol), kundi hilo lilizindua kampeni kadhaa za kilaghai na miradi ya maelewano ya barua pepe za biashara inayolenga makampuni na watu binafsi.

Raia huyo wa Nigeria alikamatwa katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Murtala Mohammed mjini Lagos katika operesheni iliyopewa jina la Delilah, iliyohusisha mabara manne.

"Natumai matokeo ya Operesheni Delilah yatasalia kama ukumbusho kwa wahalifu wa mtandao ulimwenguni kote, vyombo vya sheria vitaendelea kuwafuatilia na kuwakamata ili kuleta faraja kwa waathiriwa wa kampeni zinazodaiwa za mshukiwa," alisema Inspekta Jenerali Msaidizi wa Nigeria, Garba baba Umar.

Interpol ilisema kumekuwa na ongezeko la aina nyingi za uhalifu wa mtandao katika miaka ya hivi karibuni. **BBC**

# GEKULU MGENI RASMI WAFIA DANSI

**Na Sabato Kasika**

NAIBU Waziri wa Sanaa, Michezo na Utamaduni, Pauline Gekulu, anatarajiwa kuwa mgeni rasmi katika onesho la muziki wa dansi liitwalo Wafia Dansi.

Onesho hilo litafanyika jijini Dar es Salaam kesho likishirikisha bendi tano kutoka Morogoro, Arusha na Dar es Salaam.

Akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam jana, mratibu wa onesho hilo, Benard James, alizitaja bendi hizo kuwa ni Msondo Ngoma, Bogos Musica na Mapacha Music, zote za Dar es Salaam.

Alitaja bendi nyingine kuwa ni Waluguru Original kutoka mjini Morogoro na Mjengoni Classic ya jijini Arusha.

"Naibu waziri Pauline Gekulu anatarajiwa kuwa mgeni rasmi katika onyesho hili," alisema James.

Mbali na Naibu waziri, alisema ofisi ya mkuu wa mkoa wa Dar es Salaam, inatarajia kutuma mwakilishi.

Naye Mkurugenzi Mtendaji wa kampuni ya Mo Green inayodhamini onyesho hilo, Patric Kessy aliomba wadau kujitokeza kwa wingi kudhamini muziki wa dansi ili urudi katika hadhi yake.

"Mimi nimeonyesha mfano, ninaomba wadau wengine tuungane kuhakikisha muziki huu unapata nguvu kwani bado unakubalika, ila kuna changamoto ndogo zilizosababisha ukayumba," alisema Kessy.

Alisema, wadau wakiamua kuunga mkono juhudi alizoanzisha za kudhamini muziki wa dansi, ana uhakika utapata nguvu mpya na kuwa na mashabiki wengi wakubwa kwa wadogo.



Mchezaji Ramadhani Chomela wa Tanzania (katikati) anayecheza soka la kulipwa la watu wenye ulemavu nchini Uturuki, akiwa na wachezaji wenzake wa timu ya Kayseri Melkigaz, baada ya kutwaa ubingwa wa Ligi Daraja la Kwanza na kupanda Ligi Kuu. **PICHA: SAADA AKIDA**

# Mabondia kuzichapa usiku wa kisasi

**Na Saada Akida**

BONDIA Ally Ngwando atapanda ulingoni kuzichapa na Hamidu Kwata katika pambano la uzito wa kilo 52 la raundi 10 litakalofanyika Juni 25, mwaka huu katika uwanja wa ndani wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

Akizungumza na gazeti hili jana, muandaaji wa pambano hilo, Selemani Semunyu alisema mabondia hao wanakutana kwa mara ya nne kwa kuonyesha nani mbabe baada ya kutoka sare mara mbili.

"Pambano hili linaweza kutoa nani mbabe hasa baada ya mabondia hao kutoka sare katika mapambano miwili ambayo walicheza," alisema Semunyu.

Alisema baada ya kufanikiwa kupata bingwa wa kitaa sasa wako katika usiku wa kisasi kwa mabondia hao.

Mabondia ambao watasindikiza pambano hilo la usiku wa Kisasi ni Emmanuel Mwakyembe atakayezichapa na Hamis Morinyo katika pambano la raundi 8, Abubakari Kihio atacheza na Ally Kilongora.

Wengine watakaopanda usiku ni Jackson Malinyingi dhidi ya Said Mkola, Omary Mpemba akizichapa na Ally Mgonjwa.

## Kocha KMKM awavulia kofia wachezaji

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

KOCHA wa Mkuu wa KMKM, Ame Msimu amewapongeza wachezaji wake pamoja na benchi la ufundi kwa kazi kubwa waliyofanya na kufanikiwa kutwaa taji la Ligi Kuu Zanzibar.

KMKM imefanikiwa kutwaa Ubingwa wa Ligi Kuu ya Zanzibar Msimu wa 2021/2022 baada ya kuifunga Yosso Boys 3-0 katika muendelezo wa Ligi Kuu hiyo ambayo ipo ukingoni.

Kwa matokeo hayo KMKM imefikisha alama 64 huku ligi hiyo ikiwa imebaki michezo miwili na hakuna timu itakayoweza kufikia alama hizo hata kama KMKM itapoteza michezo iliyosalia

Akizungumza kwa furaha, Msimu amesema wachezaji walifanya kazi kubwa tangu msimu huu ulipoanza kwani ligi ya mwaka huu ilikuwa ngumu kutokana na kuwepo mdhamini wa ligi.

"Shukrani pekee ziende kwa Mungu kwa kuwapa uzima na nguvu wachezaji hadi tukafanikiwa kutimiza jambo letu la kutetea Ubingwa, lakini pia niwapongeze wachezaji na viongozi ," alisema.

Aidha alisema kuwa ligi ya msimu huu ilikuwa na ushindani wa hali ya juu mpaka kupelekea Bingwa kutojulikana licha ya wao kufanya vizuri katika msimu huu.

## Polisi yawazawadia mabao mashabiki

**Na Shufaa Lyimo**

KOCHA Mkuu wa Polisi Tanzania, Malale Hamsini amesema mabao ambayo waliyapata juzi dhidi ya Mtibwa Sugar kwenye Ligi kuu Tanzania bara ni zawadi kwa mashabiki wao baada ya kutofanya vizuri katika michezo iliyopita.

Akizungumza na gazeti hili jana, Hamsini alisema siri ya ushindi huo ni mshikamano uliopo baina ya wachezaji pamoja na uongozi kiujumla.

"Tunashukuru tumepata pointi tatu katika mchezo huo kilichobaki kwa sasa ni kufanya vizuri kwenye michezo yote iliyobakia," alisema Hamsini.

Aliongeza ushindi huo dhidi ya timu ya Mtibwa Sugar umewaondoa kwenye nafasi mbaya waliyokuwepo ikiwa ni pamoja na kulipa deni kwa mashabiki wao.

Alisema kwa wanajiandaa kukutana na timu ya Biashara United mchezo ambao utapigwa Mai 30, mwaka huu.

Alisema hadi sasa hajakata tamaa ya kuendelea kusalia kwenye Ligi Kuu kwani anaamini michezo iliyobaki atafanya vizuri.

## ZISIKUPITE

### NEYMAR KUUZWA
KLABU ya Paris St-Germain itakuwa tayari kumuuza mshambuliaji wa Brazil, Neymar mwenye umri wa miaka 30, ikiwa watapata ofa inayokubalika msimu huu wa joto. ***(Goal)***

### NKUNKU ATAKIWA CHELSEA
KLABU ya Chelsea wanatafakari uwezekano wa kumnunua mshambuliaji wa RB Leipzig Mfaransa, Christopher Nkunku mwenye umri wa miaka 24. ***(Goal)***

### TCHOUAMENI AWINDWA
CHELSEA pia wanaweza kufanya jaribio la dakika za mwisho kumnasa kiungo wa kati wa Monaco na Ufaransa, Aurelien Tchouameni mwenye umri wa miaka 22. ***(Goal)***

### BASTONI AWANIWA
KLABU ya Tottenham Hotspur wanamnyatia kiungo wa Italia na Inter Milan, Alessandro Bastoni mwenye umri wa miaka 23, huku Manchester United pia wakionesha nia ya kutaka kumsajili. ***(Gazzetta dello Sport)***

### FORSTER HUYO SPURS
GOLIKIPA Fraser Forster mwenye umri wa miaka 34, amefanyiwa vipimo vya afya yake ikiwa ni ya hatua ya kukamilisha uhamisho wake wa kwenda Tottenham Hotspurs wakati mkataba wake wa Southampton utakapokamilika mwezi ujao. ***(Mail)***

### MORATA ATAKIWA
KLABU ya Arsenal inamfuatilia kwa karibu mchezaji, Alvaro Morata. Mshambuliaji huyo wa Hispania mwenye umri wa miaka 29, amekuwa Juventus kwa mkopo wa msimju mzima kutoka Atletico Madrid. ***(Tuttosport)***

### TAMMY KUBAKI
TAMMY Abraham amesema "anafurahia zaidi" kuwa AS Roma, lakini mshambuliaji huyo wa kimataifa wa England mwenye umri wa miaka 24 hajaweka bayana ikiwa atarejea kwa Ligi Kuu ya England. ***(Metro)***

### GNABRY ATAKIWA ARSENAL
ARSENAL pia wanataka kumsajili tena winga wa Ujerumani, Serge Gnabry kutoka Bayern Munich, lakini hawana uwezo wa kumnunua mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 26 msimu huu wa joto. ***(Falk Christian)***

### NKETIAH KUBAKI
ARSENAL wametoa ofa ya mwisho kwa mshambuliaji wa England, Eddie Nketiah mwenye umri wa miaka 22 - na kuna hisia kubwa kwamba, atasaini mkataba mpya. ***(Mail)***

### BASSEY ASAKWA
KLABU ya Aston Villa iko tayari kuongeza kasi ya kumsaka beki wa Rangers na Nigeria, Calvin Bassey mwenye umri wa miaka 22. ***(Times)***

### CHUKWUEMEKA NA BARCA
BARCELONA wamekutana na wakala wa kiungo wa kati wa klabu ya Aston Villa na England, Carney Chukwuemeka mwenye umri wa miaka 18. ***(Sport)***

## DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# VAN DIJK FITI KUIVAA REAL MADRID UEFA

**Ni kwenye fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya, baada ya kupona jeraha alilolipata katika fainali ya FA dhidi ya Chelsea**

**LIVERPOOL, England**

MLINZI wa kati wa Liverpool, Virgil van Dijk atakuwa kwenye Ligi ya mabingwa Ulaya dhidi ya Real Madrid, Jumamosi.

Beki huyo aliumia kwenye fainali ya Kombe la FA dhidi ya Chelsea mapema mwezi huu na baadae hakushiriki katika mechi mbili za mwisho za Liverpool za Ligi Kuu ya England.

Liverpool walishinda michezo yote miwili, wakitoka nyuma na kuifunga Southampton 2-1 na Wolves 3-1, ingawa ushindi huo haukutosha kupata taji la Ligi Kuu ya England, ambalo lilikwenda kwa Manchester City.

Wakati matumaini ya Liverpool kupata wachezaji watatu sasa yametimia, timu hiyo ya Jurgen Klopp itawinda taji la tatu la msimu mwingine mzuri watakapomenyana na Real Madrid kwenye Uwanja wa Stade de France Jumamosi, na mmoja wa wachezaji wao muhimu atapatikana.

Van Dijk aliiambia Liverpoolfc.com: "Ndio, niko sawa, sawa kabisa. Hakuna shida na nina furaha kubwa kwa Jumamosi, bila shaka."

Alipoulizwa kama mapumziko ya wiki mbili yamemsaidia kupona, Van Dijk alijibu: "Ndio, nadhani kimwili niko fiti.

"Mwili wangu kwa hakika unafurahia kupumzika kidogo baada ya kucheza michezo mingi, nyakati nyingi, na nadhani baada ya fainali ya Kombe la FA labda ilikuwa ishara kwamba mwili wangu unahitaji kupumzika.

"Ninahisi vizuri sasa na ninatumaini kubwa kwa fainali hii."

CHEZA USHINDE JACKPOT

TZS. 1,000,0

JACKPOT
MECHI WIKI HII

BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE 13

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 28/05/22 | 17:00 | Hamarkameratene vs Odds BK | 2.43 | 3.30 | 2.80 |
| 02. 28/05/22 | 17:00 | Ghazl El Mahallah vs Talaea El Gaish | 2.95 | 2.47 | 3.10 |
| 03. 28/05/22 | 18:00 | Mansfield Town vs Port Vale | 2.65 | 3.10 | 2.70 |
| 04. 28/05/22 | 19:30 | Smouha SC vs Enppi Club | 2.60 | 2.90 | 2.95 |
| 05. 29/05/22 | 23:00 | Deportivo Madryn vs CA Guemes | 2.43 | 2.80 | 3.35 |
| 06. 29/05/22 | 02:00 | Toronto FC vs Chicago Fire | 2.50 | 3.45 | 2.65 |
| 07. 29/05/22 | 03:00 | Inter Miami CF vs Portland Timbers | 2.32 | 3.35 | 2.95 |
| 08. 29/05/22 | 07:05 | Vissel Kobe vs Hokkaido Consadole Sapporo | 2.50 | 3.25 | 2.75 |
| 09. 29/05/22 | 09:00 | Shonan Bellmare vs Cerezo Osaka | 3.20 | 3.15 | 2.28 |
| 10. 29/05/22 | 16:00 | Kuopion Palloseura vs HJK Helsinki | 2.55 | 3.15 | 2.80 |
| 11. 29/05/22 | 18:30 | Huddersfield Town vs Nottingham Forest | 3.40 | 3.20 | 2.16 |
| 12. 29/05/22 | 19:00 | Molde FK vs Bodoe/Glimt | 2.26 | 3.65 | 2.85 |
| 13. 29/05/22 | 19:00 | FK Haugesund vs Aalesunds FK | 2.20 | 3.45 | 3.05 |
| 14. 29/05/22 | 19:00 | Sandefjord Fotball vs Kristiansund BK | 2.22 | 3.55 | 2.95 |
| 15. 29/05/22 | 19:00 | Tromsoe IL vs Lillestrom SK | 2.25 | 3.45 | 3.00 |
| 16. 29/05/22 | 19:00 | Vaalerenga IF vs Rosenborg BK | 2.20 | 3.50 | 3.05 |
| 17. 29/05/22 | 21:00 | Coritiba FC PR vs Botafogo FR RJ | 2.32 | 3.15 | 3.10 |

PIGA *150*87#

Karibu SportPesa
1. Bet Sasa
2. Michezo zaidi
3. JACKPOT
4. Weka Pesa
5. Akaunti yangu
6. Toa Pesa
7. Matokeo ya Bet/Mechi
00. Toka

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ

HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, TUPIGIE:
18+ 0764115588, 0677115588
0685115588 GBT:0249

@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# MOURINHO: NABAKI AS ROMA

**TIRANA, Albania**

JOSE Mourinho ametangaza kuwa yeye ni "asilimia 100 AS Roma" baada ya ushindi wa 1-0 kwenye fainali ya Ligi ya Europa Conference dhidi ya Feyenoord, Jumatano.

Wakicheza kwa mara ya kwanza kwenye mashindano ya Ulaya tangu kupoteza fainali ya Kombe la UEFA mwaka 1991, Nicolo Zaniolo alifunga bao pekee la Giallorossi hao, akiweka mpira wavuni dakika ya 32 baada ya kuiwahi pasi ya Gianluca Mancini.

Ushindi huo kule Tirana uliipa klabu hiyo ya Serie A taji lao la kwanza kubwa la Ulaya.


Licha ya kuondoka katika msimu uliofuata baada ya kushinda Ligi ya Mabingwa Ulaya akiwa na Porto na Inter Milan, kocha huyo mwenye umri wa miaka 59 alisisitiza kwamba, anataka kubaki na kuendeleza mafanikio katika mji huo mkuu wa Italia.

"Ninabaki," alisema Mourinho. "Nataka kubaki Roma na tunatakiwa kuelewa nini wamiliki wetu wanataka kufanya katika msimu ujao, lazima tueleze mwelekeo wa msimu ujao.

"Ninahisi kama mchezaji wa Roma, nahisi kama shabiki wa Inter, Chelsea, nina wazimu kuhusu Real Madrid, lakini kwa heshima zote kwa klabu ambazo nimefanya kazi, ninahisi asilimia 100 hapa Roma.

"Jambo zuri kuhusu maisha yangu ya soka zaidi ya kushinda nikiwa na Manchester United, kushinda na Porto, Inter na sasa Roma ni jambo la kipekee.

"Kushinda wakati kila mtu anatarajia ni rahisi, wakati ni maalum kushinda unapofanya jambo la kihistoria. Natumai mashabiki watasubiri na kusherehekea nasi sote."



# Xavi ana matumaini Gavi atasaini

**BARCELONA, Hispania**

XAVI ana matumaini Barcelona wataweza kutangaza mkataba mpya wa Gavi "katika siku chache" zijazo.

Rais wa Barca, Joan Laporta wiki hii alisema hadharani klabu hiyo imechanganyikiwa kwa kuchelewa kwa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 17 kusaini mkataba mpya.

Laporta alipendekeza wakala wa Gavi, Ivan de la Pena alikuwa akimchelewesha mchezaji huyo wa kimataifa wa Hispania akiwa amebakiza mwaka mmoja tu kwenye mkataba wake.

Hata hivyo, Xavi ana matumaini kwamba Gavi atasaini mkataba mpya ndani ya siku chache zijazo.

"Mambo haya yanachukua muda, lakini nina matumaini kwamba baada ya siku chache tunaweza kutangaza kitu," alisema Xavi.

Bosi huyo Barca hakushawishika sana alipoulizwa kuhusu mustakabali wa Frenki de Jong.

De Jong amekuwa akihusishwa na kutaka kuondoka ili kuisaidia klabu hiyo kufadhili kumnunua Robert Lewandowski.

Xavi alisema kuhusu kiungo huyo wa Uholanzi: "Yeye ni mchezaji muhimu kwetu na ataendelea kuwa, lakini kila kitu kinategemea hali ya kifedha ya klabu. Tutaona kitakachotokea."

HABARI MICHEZO

000,000

# SPORTPESA YAZINDUA SUPA JACKPOT YA BILIONI MOJA

**Na Dennis Fussi**

KAMPUNI ya Michezo na Burudani SportPesa jana imezindua rasmi Jackpot mpya inayoitwa Supa Jackpot kama moja ya huduma yao nyingine kwa wachezaji wake.

Akizungumza na waandishi wa habari jana ofisini kwake, Oysterbay, Dar es Salaam, Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi, Tarimba Abbas alisema ilikuwa ni siku nyingine ambayo kampuni ya Sportpesa inatambulisha huduma hiyo.

''Najua bado watu wanashauku na Jackpot yetu ambayo imeliwa siku si nyingi zilizopita, kwa muktadha huo baada ya kuona wachezaji wetu wameanza kuzoea viwango vikubwa basi tumeonelea tuwaletee bidhaa ambayo inaendana na matamanio yao. Kwa hivyo tunazindua rasmi leo (jana) Jackpot hii ambayo itaanzia bilioni moja na itaenda kwa jina la Supa Jackpot.

Tarimba alisema Supa Jackpot hiyo itakuwa na jumla ya timu 17 na pia kiwango cha fedha ambacho mchezaji atatakiwa kuweka ni Tsh 1000 ili aweze kucheza.

Aliongeza kuwa Jackpot hiyo imegawanyika katika makundi au vipengele vitano vya zawadi ambavyo vyote mchezaji ana chaguo la kushiriki na kushinda.

"Kipengele namba moja ni cha timu 17 ambacho ukishinda unaondoka na kuanzia bilioni moja kutegemeana na Jackpot imesimamia kiasi gani. Kipengele hiki bonasi zake zinaanzia timu 16 hadi 12.

"Kundi la pili au Kipengele namba mbili ni cha timu 16 ambacho ukipatia mechi zote unashinda kuanzia Tshs milioni 750. Kipengele hiki bonasi zake zinaanzia timu 15 hadi mechi 11.

"Kundi la tatu au kipengele namba tatu ni cha timu 15 ambacho ukipatia mechi zote kwa usahihi unashinda kuanzia Tshs milioni 500. Kipengele hiki bonasi zake zinaanzia mechi 14 mpaka mechi 10. Kipengele cha nne cha Supa Jackpot ni cha timu 14 ambacho ukipatia mechi zote kwa usahihi utashinda kuanzia Tshs milioni 300. Kipengele hiki bonasi zake zinaanzia timu 13 mpaka timu 10

"Na kipengele cha mwisho hichi ni kipengele ambacho kimezoeleka kila siku ni cha timu 13 ambacho ukipatia kwa usahihi unashinda kuanzia Tsh mil 200. Cha ziada ambacho ni mabadiliko kidogo ni kwenye kombinesheni. Kama mtakumbuka Jackpot iliyoliwa ilikuwa unaweza kucheza dabo kombinesheni 7, kwenye hii kombinesheni zimeongezeka mpaka timu 10.

''Tumewaletea Jackpot hii ili wale wote wenye ndoto za kuwa mabilionea basi wapate nafasi ya kushinda kama ahadi yetu tuliyoweka hapo awali kuwawezesha Watanzania na kutengeneza mabilionea wapya kupitia mchezo wa ubashiri''. Na pia Jackot hii ina viwango tofauti vya zawadi kama ilivyoainishwa hapo juu.



Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi, Tarimba Abbas.

# Serengeti Lite yaridhishwa ligi ya wanawake

**Na Dennis Fussi**

MDHAMINI mkuu wa Ligi ya soka ya Wanawake Tanzania, (ligi ya wanawake ya Serengeti Lite), Kampuni ya Bia ya Serengeti (SBL) kupitia bia yake ya Serengeti Lite, imeelezea kuridhishwa na maendeleo pamoja na hatua zilizopigwa katika ligi hiyo.

SBL imetoa kauli hiyo siku chache baada ya ligi hiyo kumalizika msimu wa 2021/2022, ambapo Simba Queens waliibuka washindi kwa kuwafunga Mlandizi Queens 2-1 na kukabidhiwa ubingwa ikiwa ni kwa mara ya tatu mfululizo.

Mkurugenzi wa Mahusiano kwa Umma wa SBL, John Wanyancha amesema udhamini huo umesaidia kuibua vipaji vya wanawake katika soko na pia timu zenye ushindani mkali ambazo zimeweza kuitambulisha vyema ligi hiyo.

"Tunayofuraha kuona vipaji vipya vya soka kwa wanawake vinaendelea kujitokeza kutokana na udhamini wetu ambao umesaidia kuweka mazingira mazuri na wezeshi kwa wanawake kucheza mpira. Ushindi wa Tanzania kwenye mashindano ya COSAFA ni matokeo ya ligi yenye ushindani ambayo imezalisha wachezaji wazuri walioweza kutuletea ubingwa mwaka huu," alisema Wanyancha.

Wanyancha anasema Bia ya Serengeti Lite inajivunia kuwa mdhamini na kuongeza kuwa udhamini huo umeongeza ushiriki wa wanawake kwenye michezo na hususani mpira wa miguu.

Kwa upande wake msemaji wa TFF Clifford Ndimbo aliishukuru kampuni ya SBL kwa kuweza kutoa udhamini huo uliokuwa unakosekana kwa miaka mingi na kutaka makampuni mengine kuiga mfano.


LIVE IN PLAY

PATA ODDS ZAIDI UKURASA WA KATI

MECHI KALI LEO

DUNDALK FC

VERSUS

ST PATRICKS

1 | 2.13 X | 3.22 2 | 3.12

MECHI ZA USHINDI

"1" - NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA

"X" - NI TIMU KUTOKA SARE

"2" - NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

IJUMAA - 27/05/2022

| MUDA | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 14:45 | 5623 | Albirex Niigata (SIN) vs Geylang Int. | 1.42 | 4.76 | 5.44 |
| 15:15 | 3102 | J. Darul Takzim II vs Selangor Pkns | 1.55 | 3.90 | 5.06 |
| 16:00 | 4078 | Metalurgi R vs FC Norchi Dinamo Tbilisi | 2.49 | 3.51 | 2.42 |
| 16:00 | 4163 | Kelantan FA vs Kelantan United FC | 2.43 | 3.25 | 2.85 |
| 17:00 | 5193 | Otmk Olmaliq vs Neftchi Fargona | 1.44 | 3.98 | 6.59 |
| 17:00 | 5205 | Navbahor Namangan vs Lokomotiv Tashkent | 2.05 | 3.01 | 3.59 |
| 17:00 | 5738 | Isloch vs Dnepr Mogilev | 1.55 | 3.78 | 5.24 |
| 17:30 | 1220 | Mes Shahr - e Babak vs Vista Turbine | 2.80 | 2.65 | 3.00 |
| 17:30 | 2286 | Shams Azar Qazvin vs Shahrdari Hamedan | 2.33 | 2.48 | 3.75 |
| 17:30 | 3349 | Esteghlal Mollasani vs Shahin Bushehr | 1.28 | 4.38 | 10.71 |
| 17:30 | 3650 | Machine Sazi Tabriz vs Malavan Bandar Anzali | 18.51 | 5.45 | 1.16 |
| 17:30 | 4677 | Khosheh Talaei vs Rayka Babol | 2.26 | 2.72 | 3.45 |
| 17:30 | 4682 | Saipa Karadj vs Arman Gohar Sirjan | 2.96 | 2.62 | 2.62 |
| 17:30 | 4884 | Shahrdari Astara vs Sanat Mes Kerman FC | 5.26 | 2.97 | 1.74 |
| 17:30 | 5235 | Pars Jonoubi Jam vs Esteghlal Khuzestan | 2.48 | 2.53 | 3.31 |
| 17:30 | 5812 | Kheybar Khorramabad FC vs Ghasghaei Shiraz | 1.42 | 3.68 | 7.94 |
| 18:00 | 1855 | Karlovy Vary vs Pribram B | 1.67 | 4.00 | 4.50 |
| 18:30 | 4299 | NK Sesvete vs NK Jarun Zagreb | 1.78 | 3.60 | 4.40 |
| 18:45 | 2269 | NA Hussein Dey vs RC Arbaa | 5.45 | 3.75 | 1.54 |
| 18:45 | 2282 | Ol. Medea vs US Biskra | 1.62 | 3.22 | 5.85 |
| 18:45 | 2698 | CS Constantine vs HB Chelghoum Laid | 1.60 | 3.40 | 6.60 |
| 18:45 | 2782 | RC Relizane vs CR Belouizdad | 8.93 | 4.56 | 1.30 |
| 18:45 | 4409 | MC Magra vs MC Oran | 2.21 | 2.73 | 3.56 |
| 18:45 | 5062 | Paradou AC vs USM Alger | 2.10 | 2.83 | 3.71 |
| 19:00 | 1403 | Motorlet Prague vs Loko Vltavin | 2.75 | 3.40 | 2.43 |
| 19:00 | 3652 | Slutsk vs Gomel | 3.80 | 3.31 | 1.87 |
| 19:30 | 3016 | El Gouna vs El Ittihad Alexandria | 2.78 | 2.93 | 2.68 |
| 19:30 | 5490 | Karabakh Wien vs SV Stripfing | 6.22 | 4.76 | 1.37 |
| 20:00 | 2179 | Wiener Neustadt vs Bruck/Leitha | 2.78 | 3.31 | 2.28 |
| 20:00 | 2305 | FC Marchfeld Donauaue vs TWL Elektra | 2.46 | 3.75 | 2.50 |
| 20:00 | 2875 | FC Riga vs Rigas Futbola Skola | 2.40 | 3.10 | 2.76 |
| 20:00 | 3514 | SC Neusiedl vs Wiener Viktoria | 2.38 | 3.55 | 2.70 |
| 20:30 | 2252 | Universitatea Craiova vs Botosani | 1.77 | 3.33 | 4.67 |
| 20:30 | 5343 | Bloemfontein Celtic vs Orlando Pirates | 3.08 | 2.88 | 2.45 |
| 21:00 | 2214 | Dunajska Streda vs AS Trencin | 1.77 | 3.60 | 3.89 |
| 21:00 | 4933 | Albion FC vs Danubio FC | 3.20 | 3.11 | 2.15 |
| 21:45 | 2297 | Cobh Ramblers vs Longford Town | 3.46 | 3.55 | 1.89 |
| 21:45 | 2476 | Derry City vs Finn Harps | 1.26 | 5.05 | 9.13 |
| 21:45 | 2703 | UCD Dublin vs Sligo Rovers | 5.23 | 3.73 | 1.56 |
| 21:45 | 4222 | Bray Wanderers vs Athlone Town | 1.52 | 4.08 | 5.05 |
| 21:45 | 4260 | Dundalk FC vs St Patricks | 2.13 | 3.22 | 3.12 |
| 21:45 | 4325 | Waterford Utd vs Treaty United | 1.36 | 4.57 | 6.81 |
| 21:45 | 5034 | Bohemians FC vs Drogheda Utd | 1.39 | 4.39 | 6.64 |
| 21:45 | 5998 | Galway United vs Cork City | 2.53 | 3.07 | 2.63 |
| 22:00 | 2081 | Misr Lel Makasa vs Farco FC | 3.69 | 2.79 | 2.24 |
| 22:00 | 2775 | Real Sociedad B vs Zaragoza | 2.98 | 3.28 | 2.28 |
| 22:00 | 5539 | Shamrock Rovers vs Shelbourne | 1.31 | 4.48 | 8.97 |
| 22:00 | 5944 | Mirandes vs Fuenlabrada | 1.99 | 3.51 | 3.42 |
| 22:15 | 2978 | HK Kopavogs vs Afturelding | 1.58 | 4.40 | 4.80 |
| 22:15 | 5172 | UMF Selfoss vs Throttur Vogum | 1.39 | 4.74 | 5.81 |

CHEZA KWA WAJIBU | KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

Michezo
Ijumaa Mei 27, 2022
Nipashe



## Van Dijk fiti kuivaa Real Madrid UEFA



Viongozi, wachezaji na benchi la ufundi Yanga wakiwa pamoja na Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga, Sophia Edward Mjema, walipotembelea na kutoa msaada wa vitu mbalimbali ikiwamo chakula kwa shule ya awali na msingi ya Kitengo cha Elimu kwa Watoto wenye mahitaji Maalum ya Buhangija. **PICHA: YANGA**

# YANGA SC YAFUNGUKA KWA SAIDO, AMBUNDO

## ●●●Yakiri kuwasimamisha kutokana na utovu wa nidhamu, watakosa mechi ya FA dhidi ya Simba na...

**Na Adam Fungamwango**

KLABU ya Yanga imeamua kuweka hadharani na kukiri kuwasimamisha wachezaji wake Mrundi Saido Ntibazonkiza na Dickson Ambundo kupisha mechi ya nusu fainali ya Kombe la FA, Jumamosi dhidi ya Simba, kwenye Uwanja wa CCM Kirumba, Mwanza.

Hii ni baada ya juzi jioni mitandao ya kijamii kuchafuka kwa tetesi za kusimamishwa kwa wachezaji hao ambao wako Shinyanga kwa ajili ya kambi ya mchezo huo.

Msemaji wa klabu hiyo, Haji Manara alithibitisha rasmi jana kuwa Kocha Mkuu Nasreddine Nabi amewasimamisha wachezaji wao baada ya kutoroka kambini baada ya mechi kati ya timu hiyo dhidi ya Biashara United na kurejea kesho yake alfajiri.

"Kuna taarifa zimezagaa sana kwenye mitandao ya kijamii. Ni kweli Kocha Nabi ameamua kuwasimamisha wachezaji hao, Saido na Ambundo wiki hii kwanza kupisha mechi ya Jumamosi na baadaye tukirudi Dar es Salaam, viongozi na kocha watakutana kuangalia nini kitaendelea. Ni kweli baada ya mechi dhidi ya Biashara United waliondoka kambini na kurejea alfajiri, hivyo kitendo hicho kimemfedhehesha kocha na uongozi wa klabu ya Yanga kwa ujumla," alisema Manara. Hata hivyo, alisema hiyo ni kuwaondoa tu kambini kwa ajili ya mechi hiyo na haijawafukuza au kuwapa adhabu yoyote ile.

"Wamesimamishwa ili kupisha kwanza mechi kwa ajili ya kuleta morali kwenye timu, uongozi na Nabi wamefanya hivi ili ijulikane kama Yanga ni klabu ya watu na ya wachezaji pia, na singekuwa jambo jema kwa tukio kama hili kuendelea kukaa nao kambini. Yanga iko imara, imesajili wachezaji wengi, hivyo tunao wachezaji wa kutupa matokeo," alisema msemaji huyo.

Kwa siku za karibuni, Ambundo amekuwa kwenye kiwango cha hali ya juu, huku Saido akiwa msaada mkubwa wa kutengeneza mabao mengi kwenye timu hiyo.

Taarifa zinasema kuwa baada ya kusimamishwa, Saido amekwenda nchini Burundi kujiunga na timu ya taifa, huku Ambundo akibaki huko kwa sababu ndiyo nyumbani kwao.

# Pablo: Simba ipo tayari

**Na Saada Akida**

KOCHA Mkuu wa Simba, Pablo Franco amesema kikosi chake kipo tayari na watatumia uzoefu walioupata kwenye mechi za kimataifa kwa ajili ya kuwakabili Yanga katika mchezo wa nusu fainali ya kombe la FA.

Simba ambao ni mabingwa watetezi wa kombe hilo wamewekeza nguvu kubwa kutetea taji hilo na kuhakikisha kwenye mchezo huo kwa kuwafunga Yanga, mechi itakayopigwa Uwanja wa CCM Kirumba, Mwanza.

Akizungumza na gazeti hili, Pablo amesema wataingia na mbinu mpya pamoja na kutumia uzoefu wa michezo ya kimataifa kuhakikisha wanashinda mchezo huo.

Alisema morali ya wachezaji ipo juu na wanaonekana kuhitaji kujitoa kwa ajili ya kupata ushindi katika mchezo huo muhimu kwao msimu huu.

Alisema lengo la kwanza ilikuwa kutinga hatua ya nusu fainali jambo wanafanikiwa na sasa wanaingia katika mchezo huo kivingine na kutumia uzoefu ya michuano ya kimataifa kwa kucheza mpira mkubwa ili kutafuta ushindi kwa ajili ya kwenda kucheza fainali.

"Jambo zuri ni kuwa wachezaji wapo katika hali nzuri, morali ipo juu na watafanya vizuri mazoezini, tunahitaji kushinda mchezo wa Jumamosi ingawa tunajua utakuwa mgumu, tunaingia katika mchezo huo kwa mbinu tofauti na mechi zilizopita," alisema na kuongeza;

"Simba tumecheza mechi ngumu zenye ushindani mkubwa katika mashindano ya kimataifa, uzoefu wa mechi hizo kubwa tunahitaji kuona katika mchezo wetu wa nusu fainali na kupata ushindi dhidi ya Yanga."

Alisema wamepata muda wa maandalizi ya kujiandaa dhidi ya mchezo huo ambao kwao ni muhimu kutafuta ushindi ili kufanikiwa kutetea taji hilo la shirikisho baada ya kushindwa kutetea taji la Ligi Kuu Tanzania Bara.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042
9 770856 541002 >